

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 13 Aprili, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Doroth George Kilave Mbunge wa Temeke, sasa aulize swalii lake.

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Na. 49

**Madaktari Bingwa na Wataalam wa Vifaa Tiba**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa na Wataalam wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Malawi ambayo ipo Kata ya Buza Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo cha kutolea huduma za Afya cha Malawi bado hakijapandishwa hadhi kuwa Hospitali. Kwa sasa Kituo hicho kinatambulika kama Kituo cha Afya - Malawi ambacho hakijakidhi vigezo vya hitaji la kupelekewa Madaktari Bingwa kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa sasa inaendelea na taratibu za kuongeza Vifaa Tiba kwenye Kituo hicho. Aidha, Halmashari inaelekezwa kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu inayohitajika ili kiendane na hadhi ya Hospitali na kuombewa kupandishwa hadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na yote hayo utaona kwamba Hospitali ya Temeke sasa hivi ni hospitali ya Kimkoa. Kwa nini, sasa basi isiwe muhimu kituo hiki cha afya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

cha Malawi kipandishwe nakuwa Hospitali ya Temeke kwa sababu ile ya Temeke ni ya Kimkoa sasa hivi?

Swali la pili; Je, ni lini sasa Serikali itatutengea fedha ili tuweze kujenga mochwari katika kituo hiki cha Malawi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dorothy Kilave Mbunge wa Jimbo la Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dorothy Kilave kwa namna ambavyo anawasemea kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Temeke, nimhakikishie kwamba katika utaratibu ambao Serikali inaendelea kuufanya kila Halmashauri lazima iwe na hospitali ya Halmashauri, ni kweli kwamba hospitali ya Temeke ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa hiyo taratibu zitafanyika kufanya tathmini ya kituo cha afya cha Malawi kama eneo linatosheleza ili miuondombinu iongezwe ili baadaye iweze kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya Halmashauri ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jengo la mochwari tumeelekeza Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ianze kutenga fedha kwenye mapato ya ndani, ili ijenge jengo la kuhifadchia maiti na huduma hiyo iweze kuwa bora kwa wananchi wa Temeke.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swalii la nyongeza

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe ina tatizo kubwa sana la mashine ya X-Ray ni lini Serikali itapeleka mashine yakisasa ya X-Ray kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vifaa tiba zikiwemo *X-Rayza* kisasa ni moja ya vipaumbele ambavyo Serikali imeviweka na tunakwenda kwa awamu. Ninafahamu kwamba Hospitali ya Ukerewe ina *X-Rayya* zamani ambayo imekuwa inaharabika mara kwa mara na Mheshimiwa Mbunge amekuwa mara kwa mara akikumbusha na kuomba Serikali iweze kupeleka *X-Ray* hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba tunaendelea kutafuta fedha na ni kipaumbele tukipata fedha tutahakikisha tunapeleka *X-Ray* katika kituo cha afya hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi swalii la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Je, Serikali lini itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ubungo iliyopo Kata ya Kimara ili iweze kupokea wagonjwa wa aina zote badala ya kupokea wagonjwa wa *OPD* ilivyo sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipeleka fedha takribani shilingi bilioni moja na milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na kazi ile inaendelea, nimefanya ziara pale zaidi ya mara tatu na huduma za awali zimeanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, hospitali ile itakamilishwa kwa fedha za awamu ya pili ambazo zitakwenda kukamilisha miundombinu ambayo imebaki.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera haina Mtaalam wa Mifupa na wagonjwa wanalahazimika kupewa rufaa kwenda Bugando na hivyo kuwa na gharama kubwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka Mtaalam huyo kuwasaidia wananchi?(Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali zetu zote za Rufaa za Mikoa zimewekea mpango mkakati kwanza kwa kuhakikisha Wataalamu na Madaktari Bingwa wa yale magonjwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ambayo ni kipaumbele sana ikiwemo matatizo ya mifupa wanakuwepo. Kwa hivyo, tunapokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge ili tuifanyie kazi kama Serikali tupate Daktari kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, assante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Tabora na hasa Tabora Manispaa, bado wagonjwa wengi wa rufaa wanakwenda Bugando kwa sababu ya kuwa na upungufu mkubwa wa Madaktari Bingwa katika hospitali yetu ya rufaa ya Kitete, sijui Serikali ina mpango gani wa kutuletea Madaktari Bingwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu swali la Mheshimiwa Rwamlaza, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha hospitali zetu za Rufaa za Mikoa zinakuwa na Madaktari Bingwa. Kwa hivyo, nimhakikishiwa Mheshimiwa Mbunge kwamba Hospitali ya Mkoa wa Tabora nayo ni kipaumbele na tutahakikisha tunapata wataalam hao kwa ajili ya huduma katika hospitali ile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya cha Kata ya Malolo ni zaidi ya kilomita 150 mpaka hospitali ya Wilaya na kile kituo kimejengwa kwa nguvu ya wananchi na Waziri Mkuu amekichangia sana.

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba ili kituo hiki cha afya kianze kufanya kazi katika ubora wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) :** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo Mbunge wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninawapongea wananchi wa Kata ya Malolo kwa kujenga kituo cha afya kwa nguvu zao na Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kujenga vituo hivi kwa nguvu zao, Serikali ichangie nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba katika mipango ya kuhakikisha vituo hivi vinapata vifaa tiba, tumeanza na Hospitali za Halmashauri lakini tutakwenda kwenye vituo vyetu vya afya ili vitoe huduma na kituo hicho pia kitapewa kipaumbele.

**SPIKA:** Nadhani ni Kata ya Malolo lakini mwanzoni ulisema Kilolo, na Mheshimiwa Naibu Waziri akashika Kilolo ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae sawasawa.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, ni Kata ya Malolo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia swalii nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya cha Maskati Mkoani Morogoro kina Mhudumu mmoja wa afya. Je, ni lini Serikali itapeleka Wahudumu wa Afya katika kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba katika vituo vyetu vyote tunafahamu nchini kote kuna upungufu wa watumishi, ndiyo maana wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, alitoa tangazo kwamba tutakwenda kuendelea kuajiri watumishi wa kada ambalimbali ikiwepo wa afya, nikuhakikishie kwamba tutatoa kipaumbele katika kituo cha afya ambacho kinahitaji mhudumu wa afya.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kajege swalii la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Mkoani Mara mwezi wa Pili mwaka huu, alielekeza kwamba Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iweze kujengwa. Je, ni lini Serikali itajenga hospitali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni maelekezo ya kuyafanya kazi mapema iwezekanavyo na tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeshaanza kuweka taratibu ili tuanje ujenzi wa hospitali katika Jimbo la Mwibara. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba suala hilo tayari linafanyiwa kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaenda kwenye swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashariki.

Na. 50

### **Upungufu wa Nyumba za Walimu Halmashauri ya Ikungi**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga nyumba za Walimu katika Halmashauri ya Ikungi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Tais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya mahitaji ya Nyumba za Walimu Nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Ikungi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Ikungi ina mahitaji ya nyumba 454 na nyumba zilizopo ni 172, ili kukabiliana na upungufu uliopo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya Ikungi imetenga Shilingi Milioni 100 kwa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ajili ya ujenzi wa nyumba nne za Walimu katika shule za Mandigu Kata ya Munga, Nali - Kata ya Siyu, Mankumbi - Kata ya Kikio na Mau - Kata ya Ikungi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu kwa Halmashauri ikiwemo na Halmashauri ya Ikungi kadri fedha zitakavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu Jumanne, swalii la nyongeza

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake kama anavyosema mwenyewe Millioni 100 kwa upungufu ambao upo ambao ni zaidi ya asilimia 62 itatuchukua muda mrefu sana kukamilisha ujenzi wa nyumba hizi, kwa sababu walimu wetu wanafanya kazi nzuri na tuliwajengea madarasa mazuri huko vijijini mbapo tunatakiwa wakae karibu.

Je, ni mkakati upi wa haraka wa kutafuta fedha za kutosha kuweza kumaliza tatizo hili ambalo limekuwa kubwa na linapunguza ari ya walimu kufanya kazi? (*Makofii*)

Swali la pili ni pamoja na kwamba juhudii zinaendelea za kupata Walimu lakini walimu nao ni wachache sana ambao hawa-fit idadi ya wanafunzi ambao tunao, kwa sababu Serikali imetangaza ajira za Walimu na kwa sababu Halmashauri ya Ikungi ina upungufu mkubwa.

Ni nini Serikali itafanya kuhakikisha kwamba inapunguza kabisa tatizo la idadi ya walimu ambao wapo katika Halmashauri yetu ya Ikungi? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba kuna changamoto na fedha ambazo zimetolewa katika Halmashauri ya Ikungi ni ndogo. Mkakati wa Serikali kwa mfano, kama sasa hivi moja ya mikakati ya Serikali ni kuhakiksha kila sekondari mpya tunayojenga ama shule mpya tunajenga na nyumba za walimu na ninyi mmekuwa mfano *three in one*. Yote hii ni katika kukabiliana na changamoto ya nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, tuna mikakati mingi ikiwemo kutafuta fedha na jukumu letu kubwa la sasa ni kuhakikisha tunamaliza kwanza ujenzi wa madarasa na shule latika maeneo yote yenye uhitaji, mara baada ya kumaliza hiyo hatua yetu ya pili ni kuhakikisha tunajenga nyumba kwa Walimu hususan katika yale mazingira magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa Walimu katika Halmashauri ya Ikungi nimhakikishie tu Mhehsimiwa Mbunge katika hatua ambazo tumeshatangaza ajira, Ofisi ya Rais, TAMISEMI sasa hivi tutaajiri Walimu 9,800 na katika hizo ajira 9,800 tutakazoajiri sehemu ya Walimu tutapeleka katika Halmashauri yako. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuondoe shaka na hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa mliosimama niwakumbushe tu swali la msingi linahusu ujenzi wa nyumba za walimu Mheshimiwa Mwantum Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba za Walimu kidogo kidogo na kwa kuwa, zipo nyumba za Walimu ambazo zimejengwa kabla ya uhuru na mara tu hata baada ya uhuru na sasa hivi ni chakavu sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati angalau zile zilizopo ili kuboresha makazi ya Walimu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Zodo Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya maelekezo ambayo ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeyatoa katika Halmashauri zote nchini ni kuhakikisha wanatenga fedha za ndani katika mapato yao ya ndani ili kufanya ukarabati wa nyumba zote ambazo zipo za Walimu katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata hichi anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ninaendelea kuagiza Halmashauri kutekeleza yale maelekezo ambayo Ofisi ya Rais TAMISEMI iliyatoa ya kutenga fedha ili kukarabati hizo nyumba za Walimu katika maeneo yote ambayo zimechakaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nyumba za walimu ambayo iko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ni sawa na changamoto iliyopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ambapo angalau tumeanza hatua ya kwanza tumejenga maboma.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kukamilisha maboma haya ambayo ni nyumba za walimu kwa ajili ya kuwapatia malazi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati wa Serikali ni kuendelea kutoa fedha na tumekuwa tukifanya katika maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakijenga maboma, ikiwemo nyumba za walimu vituo vya afya pamoa na madarasa, kwa hiyo tumekuwa tukifanya hivyo. Hata hili analolisema ni kwamba Serikali tutaendelea kutekeleza na ndio maana moja ya kazi yetu kubwa sasa hivi ni kutafuta fedha kuhakikisha maboma mengi tunayafikia kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu katika Mkoa wa Simiyu kwenye shule za sekondari.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba, moja ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha ili tuendelee kujenga nyumba, hususan katika yale mazingira magumu huo ndiyo mkakati wetu.

Mheshimiwa Spika, hata katika bajeti ambayo tutakwenda kuipitisha kuna fedha tumetenga kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika maeneo yale ambayo ni magumu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kupeleka fedha kwa kadri ya mahitaji na tutagawanya kwa nchi nzima ili kuhakikisha tunaleta usawa kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo lkungi na Wilaya ya Mbogwe lipo. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea walimu wa Wilaya ya Mbogwe nyumba ili na wao wapate pa kuishi? (*Makof!*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemas Maganga Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, mkakati wa Serikali sasa hivi ni kutafuta fedha, kadri tunavyopata fedha maana yake tunajenga. Nimeainisha hapa kwamba siku hizi tunajenga Sekondari na kila Sekondari tunaweka nyumba za walimu *three in one*, yote hiyo ni mkakati wa kuondoa hii adha ya nyumba za walimu. Kwa hiyo. hata hapo Mbogwe nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, Serikali tutaendelea kuleta fedha kwa kadri zitakapopatikana, kwa hiyo aondoe shaka kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali hayo. Tunaelekeea Wizara ya Afya Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake

Na. 51

**Hitaji la Mashine ya Oxygen - Hospitali  
ya Rufaa ya Iringa**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** atauliza:-

Je, ni lini Serikali itafunga Mtambo wa Mashine ya *Oxygen* katika Hospitali ya Rufaa ya Iringa ili kuhudumia wagonjwa wa dharura?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalus, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 599.3 kwa ajili ya manunuzi ya mtambo wa kuzalisha Hewa Tiba ya Oksijen na ujenzi wa chumba cha kuhifadhiha mtambo huo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa na tayari hatua za manunuzi zimeanza na mradi huu utakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Nyalus swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, ni lini Serikali itapeleka mashine ya kupimia saratani ya matiti katika hospitali ya rufaa Mkoa wa Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nafikiri Mheshimiwa Mbunge hilo ni hitaji la msingi kwa sababu mashine hiyo iko kwenye Hospitali ya Kanda ya Mbeya, lakini ni vizuri ikapatikana kwenye hospitali ya Mkoa wa Iringa. Basi mimi na wewe tuje tukae tushirikiane na wenzetu ili tuone ni namna gani tunaweza tukaweka utaratibu wa mashine hiyo kupatikana kwa sababu fedha zipo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Halmashauri ya Ushetu imekamilika ujenzi wake, lakini wananchi bado wanatembea zaidi ya kilometra 80 kwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Je, ni lini Serikali italeta vifaa tiba katika hospitali hiyo ili wananchi hawa waanze kupata matibu karibu?

**SPIKA:** Sijui kama hili ni swali la Wizara ya Afya au ni la TAMISEMI? Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa pamoja lina *element* ya *MSD*.

**SPIKA:** Karibu kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Ahsante. Kwanza *priority* ambayo Mheshimiwa Waziri wa Afya ameelekeza sasa hivi ni kuhakikisha hospitali zote zile ambazo zimeshajengwa vituo vya afya, zahanati na hospitali za Wilaya na majenzi yote, kuhakikisha sasa vifaa tiba vinaenda kununuliwa. Kama ambavyo nilsema jana sasa hivi shida siyo fedha kwa sababu Rais wetu kama nilivoyosema tayari alishapeleka shilingi bilioni 333.8 na tayari kila mwezi kuna utaratibu wa kupeleka shilingi bilioni 15 *MSD*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwanza nitumie fursa hii kwa kushirikiana na wenzangu wa TAMISEMI kwamba *RMO* asimamie kwanza *OPD* kwenye hiyo hospitali ianze, kwa sababu inawezekana kuanza *OPD* mapema na kujipanga kwa ajili ya kuanza wakati tunangojea vifaa vya kuhakikisha hospitali hii inaenda kufanya kazi kama *full flagged* kama hospitali ya Wilaya. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mosho Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Tanganyika imekamilika kila kitu, tatizo liliopo ni ukosefu wa vifaa tiba ambavyo vinapelekea huduma ya upasuaji kukosekana katika hospitali hiyo.

Je, ni lini itakamilisha kuleta vifaa tiba ambavyo vimebaki katika hospitali hiyo?

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ni lini utapeleka vifaa kwenye hospitali ya Wilaya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza hospitali hiyo tulitembelea na nilitegemea Mheshimiwa Mbunge kwanza angeshukuru kwa *Digital X-Ray* ambayo tayari tulikabidhi pale siku ile, yeye hakuwepo lakini Mkuu wa Wilaya alipokea kwa niaba yake.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri subiri kidogo, Waheshimiwa Wabunge nilishatoa maelekezo hapa kwa hiyo usimuweke Mbunge mazingira kwamba yeye hatambui huo mchango uliotolewa, anatambua mchango ni kwa sababu maswali lazima yawe mafupi, kwa hivyo anaenda moja kwa moja kwenye swali na wewe nenda moja kwa moja kwenye jibu la swali alilouliza. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli anachokisema Mbunge kulikuwa na vifaa vya Shilingi Milioni 507 vilitakiwa zipelekwe vimepelekwa vifaa vya Shilingi Milioni 203 vitaenda kumaliziwa mwaka huu kuhakikisha vimepelekwa vilivyobakia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Je, ni lini zile mashine ulizokuja kukagua mwaka jana ukaniahidi baada mwezi utaleta Wataalam wa *dialysis* zitaanza kufanya kazi katika Hospitali ya Mkoa ya Iringa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nalipokea swali lake na kwa sababu tulienda wawili tukalitembelea

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

eneo, naomba tukutane tukae pamoja tuhakikishe hiyo kazi inaanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgali swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha taratibu za manunuzi ya mashine ya *CT-Scan* ambapo na tunategemea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi itapata mojawapo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge na tayari *CT-Scan* yao iko kwenye manunuzi kabla ya mwezi Juni itakuwa imefika *ST-Scan* ya hospitali ambayo Mheshimiwa Mbunge anaisema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la *MSD* kutokuleta dawa kwa wakati katika Mkoa wa Kigoma, hata wakileta wanaleta chini ya asilimia 50.

Je, nini kauli ya Serikali katika kutatua changamoto hii? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge na kama nilivyosema jana na nimerudia leo kwamba shida siyo fedha ni pale *MSD* Idara ya Manunuzi kumekuwa na tatizo ambalo Wabunge mmekuwa mkielezea.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, siyo Kigoma tu nilikwenda Mkao wa Lindi waliomba madawa 102 lakini ziko *item* 55 wakapewa Tano, kwa hiyo kuna tatzivo kwenye eneo la manunuzi na ndilo ambalo mmekuwa mkizungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wenzetu tutaenda kulishughulikia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunaelekea sasa Wizara ya Nishati Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalilake.

Na. 52

### **Mradi wa Umeme wa Upepo – Singida**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa mradi wa umeme wa upepo Singida utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swalilaka Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia *TANESCO* imikuwa ikifanya jitihada za kuendeleza miradi mbalimbali ya kufua umeme nchini, ikiwemo miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu ya upepo katika maeneo ya Mkao wa Singida inayotekelze na wawekezaji binafsi wenye nia ya kuzalisha umeme na kuiuzia *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni pamoja na mradi wa upepo *MW* 50 unaotekelze na Kampuni ya Upepo *Energy* eneo la Msikii Halmashauri ya Singida Vijijini, ambapo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

majadiliano ya mkataba wa kuuziana umeme (*Power Purchase Agreement*) kati yake na *TANESCO* yanaendelea. *MW 300* unaotekelawa na Kampuni ya *GEO Wind* eneo la Kititimo Halmashauri ya Singida Mjini ambapo majadiliano baina ya Mwekezaji na Mfadhilli *Green Climate Fund (GCF)* yanaendelea. Pia *MW 100* unaotekelawa kwa ubia wa *TANESCO* na kampuni ya Abu-Dhabi (*Masdar*) eneo la lkungi, Halmashauri ya Wilaya ya lkungi ambapo Upembuzi Yakinifu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hii inatarajiwa kukamilika kati ya mwaka 2023 na 2027.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba nasikitishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, mradi huu toka mwaka 2016 Mheshimiwa Waziri aliekuwepo alisema 2017 utekelezaji utaanza na utakamilika 2019 leo tunaambiwa mpaka 2027, nataka kujua sababu kubwa ya mradi huu kusucasua na hizi danadana inatokana na nini?

Swali la pili, najua kwamba kulikuwa kuna majadiliano kati ya Serikali na Benki ya *Exim* ya China kwa ajili ya mkopo wa Dola Milioni 132. Nataka kujua majadiliano haya yamefikia wapi ili mradi huu uweze kutekelezwa na wananchi wa Mkoa wa Singida tumechoka kudanganywa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jesca kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimetaja miradi mitatu iliyopo katika Mkoa wa Singida sasa sijui alitaka kujua upi kati ya hiyo lakini kwa swali la pili ninaamini alitaka kujua mradi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ambao unatekelezwa kati ya Mkandarasi anayeitwa *GEO Wind* ambaye kwa sasa *financier* wake ni *Green Climate Fund*.

Mheshimiwa Spika, miradi hii kama tulivyosema inatekelezwa na wawekezaji binafsi, Serikali tunaweka mazingira ya uwekezaji baada ya hapo yeye anatakiwa atafute mfadhlili atakayeweza kumfadhlili na kukamilisha eneo lake la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwenzetu wa *GEO Wind* huyu ni mfadhlili wake wa tatu, alienda *Exim* wakajadiliana lakini hawakukubaliana baadaye akapata mtu mmoja anaitwa Aplonia kutoka Hispania wakajadiliana hawakukubaliana, sasa saa hizi yupo na huyo ambaye tunamuita *Green Climate Fund* wanaendelea na majadiliano, watakapokamilisha na wakawa tayari kuwekeza upande wetu tumeshakamilisha, tumeshaweka masharti na tuko tayari kumpokea kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tukasema tunatarajia kati ya mwaka 2023 mpaka 2027 miradi hii itakuwa imekamilika baada ya kukamilisha upande wao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami niungane na Dada yangu Jesca Kishoa jambo hili limekuwa la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri kama atakuwa tayari yeye pamoja na hao wawekezaji *GEO Wind* na wengine tukutane kwa pamoja kabla Bunge hili halijaisha ili kuweza kujadili mstakabali wa mradi huu wa umeme wa upepo pale Singida Mjini? (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sima la nyongeza kwamba Wizara tuko tayari kufanya jambo hilo kwa maslahi ya wananchi wa Singida na Watanzania kwa ujumla.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Noah Olesaputu swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Naibu Waziri swali kwamba kulikuwepo na ulipaji wa fidia kwenye laini kubwa ya umeme katika Jimbo la Arumeru Magharibi, Halmashauri zingine zote zimeshalipwa hiyo fidia lakini Halmashauri ya Wilaya Arusha *DC* haikulipwa hizo fedha hadi leo.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwamba fedha hizo zitalipwa lini na kwa kwanini yenyewe haikulipwa mpaka sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Olesaputu swali lako hilo ni la msingi kabisa litajibowi kama swali la msingi na siyo swali la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma Mbunge wa Muheza, sasa aulizwe swali lake.

Na. 53

#### **Hitaji la Wawekezaji Katika Kilimo cha Muhogo**

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa maksudi wa kuwavutia Wawekezaji katika Kilimo cha zao la Muhogo Wilayani Muheza?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mkakati wa kuendeleza tasnia ya muhogo wa miaka kumi kati yam waka 2020 mpaka mwaka 2030 unaolenga kuimarisha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za zao la muhogo, kuongeza uzalishaji wa muhogo kutoka wastani wa tani 8.2 hadi tani 24 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Serikali inaendelea na jithada za kuwavutia wawekezaji ambapo mwaka 2018 kampuni ya *CMTL-Tanzania Limited* ilipatikana na kupewa eneo la ekari 10 katika Kata ya Mbaramo kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kuchakata muhogo. Serikali inafuatilia ili mwekezaji awekeze kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *MEDA* inasambaza jumla ya pingili 700,000 za mbegu za mihogo aina ya Mkuranga 1 na Kiroba katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa ajili ya kupandwa katika eneo la ekari 175.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Mwinjuma swalii la nyongeza.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu yanayotia moyo ya Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza: -

Kwanza; kwa muda mrefu kilimo cha muhogo kimekuwa kikifanywa kienyeji na kwa vile kwa sasa soko lake ni kubwa na la uhakika ni lini Serikali itaanza kuwekeza kwenye utafiti hasa kuititia kwenye kituo chetu cha *TAR/Mlengano* ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa zao hili?

Swali la pili; kutokana na uwezo mdogo wa kipato kwa wananchi wengi wa vijijini Muheza, hali inayokwamisha ushiriki wao kwenye kilimo chochote kinachohitaji muda mrefu na uwekezaji mkubwa.

Je, kwa vile nimeshasema kwamba soko la muhogo sasa hivi ni kubwa na la uhakika. Serikali haionti haja ya kuhimiza kilimo cha muhogo ambacho inachukua Miezi Tisa tu kuwa tayari ili kuongeza kipato cha wananchi hawa wa vijijini? Ahsante. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwinjuma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwanza kama nchi tun-import wanga zaidi ya tani 8,000 kwa mwaka, pamoja na tunatumia muhogo kwa ajili ya chakula vilevile tunatumia wanga kwa ajili ya viwanda hasa kwenye maeneo ya pharmaceutical, matumizi ya nguo na viwanda vyatkarasi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie kuhusu varieties sasa hivi tumeshatambua variety 10 katika utafiti ambazo zina uwezo wa kutuzalishia mpaka tani 20 mpaka 40 ambazo zimegundulika na watafiti wetu wa *TARI*. Hatua ya pili kumpelekea mkulima variety azalishe halafu hakuna uhakika wa soko ni jambo la hatari zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumechukua hatua kama Wizara tumeshaanza vikao na viwanda vyote vinavyotumia wanga kuweza kutambua ubora wa wanga wanaoutaka ili tuweze kuwapelekea wakulima na tutengeneze mfumo wa *contract farming* ili yale yaliyotokea Muheza mwaka jana na mwaka juzi yasiweze kujitokeza tena.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwelekeo wa Serikali kuhusu muhogo ni mwelekeo wa *industrial* pamoja na matumizi ya chakula

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ndani zaidi tunataka ku-*push* mwelekeo wa *industrial* na tumeanza kuchukua hatua hizo.(Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rungwe wakulima wa parachichi wako kwenye kilio kikubwa sana ambapo wameambiwa wanunuzi watanunua maparachichi kuitia *AMCOS*, *AMCOS* yenyewe Rungwe iko moja, masharti yamekuwa ni magumu kwamba lazima pesa wapeleke kwenye *AMCOS* ndio watatununulia maparachichi hao wanunuzi wa parachichi. Ni jambo la kusikitisha sana wananchi wanalia wanunuzi wote wamekimbia wameenda maeneo ya Njombe, Mbozi na maeneo mengine, pale Rungwe maparachichi yanaozea shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupata kauli ya Serikali; Je, wapotayari kuwalipa fidia wananchi ambaao maparachichi yao yanaozea shambani sasa hivi? Pia tupate kauli ya Serikali wanasema nini kuhusu kilimo cha parachichi?

**SPIKA:** Swali la nyongeza ni moja tu Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantona Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akilifuatilia hili jambo, tumeongea na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, *avocado* siyo korosho, *avocado* sio pamba, *avocado* siyo kahawa, hauwezi kulazimisha kununua *avocado* kwa kukusanya kwenye Chama cha

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Msingi, hauwezi kulazimisha *avocado* kuipeleka kwenye Chama cha Msingi kwa sababu ni *perishable*. Kwa hiyo, tumekubaliana na Mkuu wa Mkoa waufute huo utaratibu na wameshaanza kuufuta, wawaache wakulima wenye *contract* na wanunuzi wauze moja kwa moja kwa wanunuzi wao. Wahakikishe tu Serikali inapata ushuru wake stahiki katika njia halali na wafute tozo zote walizoziweka ambazo hazijaidhinishwa na Wizara ya Kilimo kwenye zao la *avocado*. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hilo katazo linafanywa lini, kwa sababu maparachichi yanaoza. Mkuu wa Mkoa hilo katazo atalifanya lini?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, katazo hili nimeongea na Mkuu wa Mkoa siku Mbili zilizopita na tumeshakubaliana na Wizara ya Kilimo imemwandikia barua Mkuu wa Mkoa siku ya jana kumueleza haya ambayo ninayasema. Kwamba, *avocado* haiwezi kuuzwa kwenye mfumo ambao unataka kufanyika Rungwe.

**SPIKA:** Hilo limeshaeleweka mmempa maelekezo ya hilo katazo lini, kwa sababu haya mazao yanaharibika. Kwa hiyo, kama atakuja kutoa hilo katazo baada ya miezi mitatu hiyo ndio hoja. Katazo linatoka lini? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, katazo limetoka juzi kwa simu jana limekwenda kwa barua. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile bei za miche ya kisasa ya kahawa, ya miparachichi hiyo tunayozungumza, ya migomba bei zake ni juu sana. Sijui Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa miche hiyo? (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka ujao wa fedha tutakapopitisha bajeti hapa mtaona kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo inatoa *guidance* juu ya *subsidy* kwenye zao la *avocado* na baadhi ya mazao na mazao haya kwa muda mrefu yalikuwa hayana *guidance*, hayajulikani nani mzalishaji kila mtu anajizationalia barabaranii.

Kwa hiyo, tunazindua *guiding* ya uzalishaji wa miche ya *avocado* na mazao ya miti na kutakuwa kama ambavyo mzalishaji wa mbegu anavyozalisha na hapo mtaona kwenye bajeti tutatenga fedha kwa ajili ya *ku-subsidize* uzalishaji wa miche millioni 20 kuanzia mwaka kesho kwa uwezo wa Mungu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika nchi yetu kati ya matatizo makubwa tuliyonayo ni tatizo la ajira hasa kwa vijana wetu na tunatambua kabisa kwamba Wizara ya Kilimo ndiyo inayoweza kupunguza tatizo hili.

Je, Mheshimiwa Waziri umejjipangaje katika Wizara yako kuhakikisha kwamba kilimo kinasaidia kupunguza ajira hasa kwa vijana wetu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Manyinyi Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ni sekta ambayo kweli inaweza kuajiri watu wengi sana lakini yapo mambo makubwa manne ambayo kwa muda mrefu yamewafanya vijana kutokuwa tayari kwenda kwenye sekta ya kilimo:

- (i) Upatikanaji wa ardhi,
- (ii) Upatikanaji wa mitaji,
- (iii) teknolojia, na
- (iv) soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, hii imewafanya vijana wengi kutokwenda huko. Kwa hiyo, kama Wizara tutakapokuja kusoma bajeti mwaka huu mtaona *tuna-launch* kitu tunaita '*building a better tomorrow*' na tutaitengea fedha katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunaanzisha *block farm system* ambako Serikali itachukua maeneo makubwa itayasafisha, itapima afya ya udongo, tutagawa *block farm* na kuwamilikisha vijana hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, kama ni eneo linahitaji fidia tutalipa sisi na yale maeneo yatakuwa *owned* na hao vijana ambao watakuwepo hapo na kuwaunganisha moja kwa moja na soko na kujua afya ya udongo na mazao yatakayozalishwa kwenye eneo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Sanga swalil ya nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Zao la parachichi ukienda kwenye soko la nje inaonekana parachichi nyngi zinatoka kwenye nchi ya jirani, lakini uzalishaji mkubwa unafanyika Njombe na Mikoa ya Tanzania. (*Makofi*)

Ni lini tutatengeneza *ownership* ya soko hili la parachichi lionekane ni la Tanzania na siyo la nchi jirani

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ambao wanunuzi wengi wanenanua Tanzania na wanafanya *packaging* kwa jina la nchi ya jirani? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sanga la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, sababu za parachichi zetu kuwa-*branded* nje ni kwa sababu sisi kama nchi tumekuwa kwa muda mrefu hatuna *infrastructure*. Kwa hiyo, watu wanakuja kununua *raw wanapeleka* wanakwenda *ku-brand* nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuanzia mwaka kesho tutatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa *common use facility* tatu, moja tutajenga Mkoa wa Iringa ambapo itafanya kazi ya *sorting, grading* na *branding* na ye yote anayenunua huko atanunua akifikisha pale atakuta hiyo huduma inafanyika na *itakuwa-branded* kama *produce of Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, vilevile, zipo kampuni ambazo sasa hivi zimeshaanza *ku-brand* parachichi yetu na *kui-brand* kama *produce of Tanzania* kama *Eat Fresh* na Kampuni zingine ambazo zipo katika Nchi yetu. Kwa hiyo, jambo hili lipo na Serikali tunachukua hatua kuanzia mwakani tutakuwa na *common use facility* tatu moja Dar es Salaam, moja Iringa na moja Kilimanjaro. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo; Je, Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kuhamasisha na kuimarisha uwekezaji kwenye zao la *vanilla* kwa Mkoa wa Kagera? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Wizara zao la *vanilla* halikuwa kwenye *map* ya Serikali na kuonekana kama ni zao ambalo *lina-attract* na kuweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge baada ya kujitokeza wanunuvi na wakulima wengi *either* kutapeliwa au kufanya nini, tumeanza kuchukua hatua sasa hivi na tunavyoongea sasa hivi timu yetu ya Wizara ya Kilimo iko Mkoa wa Kagera na wengine wameelekea Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kuweza kuangalia *map* na kuweza kulitambua vizuri na kulitengenezea mkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuanzia mwaka ujao wa fedha baada ya mwaka mmoja kutakuwa na mkakati rasmi wa nchi kuhusu zao la *vanilla*. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Hhayuma swalii la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu kwa kuwa mashamba ya Murujanda, Sechet ambayo yako chini ya Mwekezaji kwa sasa uzalishaji uko chini ya kiwango na aliahidi kwamba ndani ya mwaka mmoja ataboresha.

Wizara ina kauli gani katika kuhakikisha kwamba tunapata Wawekezaji ambao wako makini au kuwapatia wana Hanang' maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Hanang' kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mashamba yalichukuliwa na Wawekezaji mojawapo ni Ngano *Limited* katika Mkoa wa Manyara Wilaya ya Hanang' na uwezo wake wa kuyatumia hauzidi asilimia 30. Aliingia makubaliano nasi kama Wizara ya Kilimo na kutuambia kwamba tumpe *span* ya mwaka mmoja, atawea kufanya matumizi kwa kiwango cha asilimia 100 mpaka sasa amefeli.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Wizara sasa hivi tunawasiliana na wenzetu wa *T/C* na kuwasiliana na wenzetu wa Hazina ili tumuite Mwekezaji huyu, tukae naye aweze *ku-offload* hekari zaidi ya 30,000 ambazo ameshindwa kuzitumia mpaka sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninatumia Bunge lako Tukufu kuwaambia Halmashauri ya Hanang' kwamba eneo la Basutu lisibadilishwe matumizi litabaki kuwa eneo la uzalishaji wa ngano. Hili ni jambo muhimu sana na Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani, wahakikishe hawababidilishi eneo la Basutu kulipelekea matumizi mengine isipokuwa kwa ajili ya matumizi ya ngano. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swalii la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na unyanyasaji sana kwa wanunuvi wa parachichi wanachagua wao kusema haya yamekuwa *reject*, haya yamekuwa mazima.

Serikali inasaidia nini wakulima kuonesha kama kweli yale ni *reject* kwa sababu, wanawaonea ili wao wakapate faida zaidi? (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, labda tu niseme kitu kimoja kwamba ninamuomba Mheshimiwa

Mwakagenda na nitumie nafasi hii kama kuna wanunuzi wowote wanatumia hiyo nafasi kwa ajili ya kuwadhlumu wakulima na kuzitaka Halmashauri zote kuhakikisha kwamba mnunuzi yejote anayeingia kununua parachichi katika Mkoa au Wilaya husika afuate *guiding* na *manual* ambayo Wizara ya Kilimo imeitoa. Kama kuna *special case* kwenye maeneo maalum ofisi yetu iko wazi tunaomba hizo taarifa tutachukua hatua. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye swalii la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema.

Na. 54

### **Kutokamilika kwa Miradi ya Umwagiliaji - Sengerema**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza: -

Je, ni lini miradi ya umwagiliaji katika Vijiji vya Nyamterela na Katunguru pamoja na Vijiji vya Kwinda na Isole itakamilika Wilayani Sengerema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kuititia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bwawa na miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya Katunguru yenye hekta 600 iliyopo kijiji cha Nyamterela Wilayani Sengerema.

Vilevile Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya Usole yenye hekta 1,000 iliyopo katika kijiji cha Kishinda.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Ni kwamba Sengerema inazo skimu Tano, katika hizi skimu Tano skimu Mbili ndiyo zimepata fedha. Sasa, nataka kupata majibu ya Serikali skimu Tatu zilizobakia; Je, lini zitapata fedha kwa ajili ya kufanya usanifu?

Swali la pili, Sengerema tunao Ushirika wetu wa Nyanza ambako kuna viwanda vitatu viko katika Wilaya ya Sengerema. Hatujawahi *ku-gin* pamba leo ni miaka 20.

Je, Wizara ina mpango gani kuhusiana na Ushirika katika Wilaya ya Sengerema? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Sengerema kwamba mwaka ujao wa fedha tunajenga skimu mbili katika Wilaya ya Sengerema. Vilevile, tutatenga fedha zaidi ya Shilingi Milioni 300 kwa ajili ya kufanya usanifu kwenye skimu zilizobaki, ambazo zitatengewa fedha mwaka unaofuatia. Kwa sababu, hatuwezi kujenga skimu zote tano, kwa wakati mmoja. Kuhusu suala la Ushirika nataka nitumie nafasi hii na ninapongeza baadhi ya Vyama vya Ushirika katika nchi yetu ambavyo vimeweza kufufua *ginneries*. Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza kwa mwaka huu tumekubaliana Nyanza na Tanzania *Agricultural Development Bank* na sasa hivi ninavyoongea *TADB* wanafanya survey Nyanza, wanafanya survey *SIMCU*, wanafanya survey *SHIRECU* kwa ajili ya kufufua *ginnery* za vyama hivi vitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba mfumo huu wa kuwa na *ginnery* zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika na Vyama vya Ushirika kuwa na kampuni zao narudia. Vyama

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

vya Ushirika kuwa na kampuni zao ambazo zinaingia kwenda kununua pamba kuongeza ushindani inamsaidia mkulima.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya *surveyya TADB* katika *ginneryza Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza*, tutakutaarifu kwamba ni *ginnery gani ya Nyanza* inafufuliwa sasa hivi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Waziri. Tunaelekeea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Hassan Zidetu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 55

### **Kufungua Tawi la Chuo cha Sua – Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafungua tawi la Chuo Kikuu cha Sokoine Wilayani Tunduru kwani majengo yamekamilika kwa asilimia 65?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
aliibju:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidetu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kilikabidhiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru majengo na ardhi kwenye eneo lilitokuwa Kambi ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara katika Kijiji cha Darajambili tarehe 17 Agosti, 2018.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilianza kutumia majengo ya kampasi ya Tunduru kama kituo cha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Usimamizi wa Wanyamaporini na Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Misitu mwaka, 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na mpango wa kufanya ukarabati wa miundombinu na kuanzisha shughuli mbalimbali za kitaaluma, utafiti na ushauri wa kitaalam kwa lengo la kuiwezesha kampasi hiyo kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Zidadi Kungu swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itafanikisha kampasi ya Tunduru kuanza rasmi masomo ya muda mrefu badala ya ilivyo sasa kwa masomo ya vitendo ambayo ni ya muda mfupi? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kungu Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba kampasi ile tayari ilishaanza kazi toka mwaka 2018/2019, lakini kozi ambazo zinatolewa pale ni zile za muda mfupi wanafunzi wetu wanapokwenda kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022 tumetenga zaidi ya Shilingi Milioni 250 kwa ajili ya kuongeza miundombinu kwenye eneo lile. Katika mwaka ujao

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wa fedha tutatenga tena fedha zaidi ya Shilingi Milioni 300 kwa ajili ya kuongeza miundombinu ambayo itasaidia sasa chuo kile kiweze *ku-operate* katika masaa 24 kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya michakato hii kukamilika tunatarajia baada ya miaka hii Miwili hadi Mitatu tutaweza kuanza kozi pale za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Maboto swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisangwa kilichopo Bunda ndicho chuo pekee kinachotoa fani mbalimbali za ufundi na tatizo kubwa pale ni mabweni.

Je, ni lini Serikali itatusaidia kupata mabweni hayo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Elimu na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maboto Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna changamoto kwenye Vyuo vyetu vya *FDC* lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 tumefanya ukarabati pamoja na upanuzi wa vyuo hivi vya *FDC* 54 kote nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie katika kipindi kijacho tunaendelea na upanuzi huo ambapo

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

tunaamini kabisa, chuo hiki cha Bunda kitazingatiwa katika ukarabati na upanuzi pamoja na haya mabweni tutaweza kuyafikia. Nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhata swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Katika Kijiji cha Maneme Wilayani Nanyumbu kuna majengo ambayo yaliachwa na Kampuni ya ujenzi wa barabara na Serikali ya Kijiji iliyakabidhi majengo yale Wizarani.

Je, ni lini Wizara itatekeleza ahadi yake ya kufungua Chuo cha Ufundu katika Wilaya yangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Elimu na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mhata Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo hili la Mtambaswala ambapo Kampuni yetu ya ujenzi wa barabara ilikuwa na kambi, tayari imekabidhiwa kwa Wizara ya Elimu kupitia Mamlaka ya Ufundu Stadi (*VETA*). Mwaka jana mwezi Novemba, 2021 timu yetu ya wataalam ilikwenda kufanya tathmini ya eneo lile namna gani tunaweza tukaboresha, kwa maana kwamba ya kufanya ukarabati pamoja na kuongeza baadhi ya miundombinu ili kiweze kufunguliwa.

Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari tathmini tumeshafanya na tunatarajia katika mwaka ujao wa fedha, eneo lile tutakwenda kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba Chuo kile kinafunguliwa. Nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, sasa ni miaka miwili toka Serikali itoe fedha za ukarabati wa Chuo cha Maendeleo Tango - *FDC* Mbulu na kwa kuwa tayari mradi wa awali umeshatekelezwa.

Je, ni lini Serikali yetu itatoa tena fedha ya ukamilishaji wa majengo hayo ya Chuo cha Tango *FDC* kwa awamu ya pili? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yaliyopita katika Chuo cha *VETA* kule Bunda ni hivyo hivyo kwa upande wa wenzetu wa Tango.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza katika fedha ambazo tulizipata za UVIKO – 19 zaidi ya Shillingi Bilioni 6.8 zimekwenda kununua vifaa kwa ajili ya vyuo hivi vya *FDC* (54) kote nchini, ambapo Chuo hiki cha Tango nacho vilevile kimezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, vifaa hivi tayari tunavipeleka kwenye maeneo haya ya vyuo, vilevile upanuzi wa vyuo hivi tumeuingiza kwenye bajeti yetu ya mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, maeneo haya yote tutakwenda kuyafanyia kazi kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinatoa taaluma ile ambayo inatakiwa katika maeneo husika.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nyamoga swalii la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru: -

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa chuo cha ufundi VETA kwa Wilaya ya Kilolo kitajengwa kama ambavyo zimekuwa ahadi za Serikali kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni sera ya Wizara ya Elimu kwamba, katika kila wilaya tunakwenda kujenga chuo cha VETA. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa vile sasa tumekamilisha ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya 29 na vile vinne vya Mikoa ambavyo tunakadiria kunako mwezi Mei tutakwenda kumaliza katika mwaka ujao wa fedha tutaendelea na ujenzi katika maeneo ambayo bado vyuo havijawea kujengwa. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swalii la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujuu ni lini Serikali itafungua au chuo kikuu au tawi la chuo kikuu Mkoani Kagera kwa kuwa limekuwa ni hitaji la muda mrefu na ukizingatia tuna ardhi ya kutosha? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wetu wa *heat ambao tunataraji tutaanza kuutekeleza* katika mwaka ujao wa fedha, mionganini mwa maeneo ambayo ni *focused zone* ni katika Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ambayo tunaenda kujenga *campus* nadhani ilikuweko *campus* pale ambayo baadae ilikuja kufungwa, tunaenda kuifufua ili kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kagera unakwenda kupata chuo hiki.

Vilevile tunafungua chuo kikubwa sana cha *VETA* katika Mkoa wa Kagera ambapo tunaamini chuo kile kitakuwa na hadhi vilevile ya chuo kikubwa hapa nchini. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunakushukuru.

Tunaenda Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Kuunda Bodi ya Wataalamu wa Ugavi na Ununuzi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunda tena Bodi ya Wataalamu wa Ugavi na Ununuzi (*PSPTB*) baada ya kuvunjwa kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi uliofanywa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara iliteua Wajumbe wa Bodi ambapo uteuzi wao ulianza Desemba 19, 2021. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa jibu zuri ambalo nimelipata:-

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati upi ambao imeuweka wakati mwingine isijirudie kukaa muda mrefu bodi za wataalam kutokuwepo?

Mheshimiwa Spika, Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejiandaa na imeweka mipango, mikakati na taratibu maalum ambazo zitakuwa ni suluhisho sahihi la kutokuwa na muda mrefu wa kuunda ama kuteuwa bodi hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango tunakushukuru kwa majibu yako. Tunaelekeea Wizara ya Maji. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Udhibiti wa Uharibifu wa Vyanzo vya Maji  
Manispaa ya Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti uharibifu wa vyanzo vyta maji katika Manispaa ya Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la kusimamia rasilimali za maji ni kudhibiti uharibifu kuhakikisha vyanzo vyta maji vinahifadhiwa kwa ajili ya uendelezaji na uharibifu unadhibitiwa wakati wote. Katika Manispaa ya Morogoro, Serikali inaendelea na utambuzi wa maeneo ya vyanzo vyta maji, kuweka mipaka na kuyatangaza kuwa maeneo tengefu. Hadi Desemba 2021, vyanzo vyta maji kumi vimewekwa mipaka, hii ni pamoja Bwawa la Mindu ambacho kimetangazwa kuwa eneo tengefu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, jumuiya za watumia maji Saba zinashiriki katika uhifadhi wa vyanzo vyta maji katika maeneo yao. Pia, vilabu 10 vyta michezo vyta watoto vimeundwa katika Shule za Msingi ili elimu ya utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vyta maji na mazingira inatolewa kwa jamii. Aidha, hadi Machi 2022 jumla ya miche ya miti 96,500 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya vyanzo vyta maji.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa muda mrefu wa kudhibiti uharibifu wa vyanzo vyta maji ni kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde ili ziweze kutekeleza Mipango ya Uhifadhi wa Vidakio vyta Maji nchini kwa Mabonde yote likiwemo Bonde la Wami-Ruvu. Mipango hiyo imeainisha maeneo ya vipaumbele kwa ajili ya shughuli za uhifadhi wa vyanzo vyta maji ikiwemo kupanda miti rafiki kwa maji kwenye maeneo ya vyanzo vyta maji, kilimo cha makinga maji, urejeshaji wa uoto wa asili kwenye kingo za mito na udhibiti wa utirishaji wa majitaka kwenye mazingira.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili mafupi ya kuongeza: -

Mheshimiwa Spika, kupanda miti na kutunza miti ni mambo mawili tofauti. Hata hivyo, na mimi nilishiriki kupanda hiyo miti Wami-Ruvu. Je, kuna mpango gani ambao umewekwa madhubuti wa kutunza hiyo miti 96,500 iweze kustawi angalau asilimia 70?

Swali la pili; Chuo cha Kilimo *SUA* mnakishirikishaje katika utunzaji wa vyanzo vya maji na pia katika utunzaji wa uoto wa asili, hasa kwenye milima ya Uluguru ambako ndio kuna vyanzo vya maji ambavyo vimeharibiwa kwa wingi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charistine Ishengoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ambaye pia ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ambayo inafanya vizuri sana. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kama alivyosema naye alishiriki kupanda miti, hii miti sote tumepeana majukumu kuona kwamba haifi na itapona zaidi ya asilimia hizo 70 ambazo amezitolea mfano.

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishaji wa Chuo cha *SUA* Wizara tumekuwa tukishirikiana na wataalam mbalimbali katika makongamano na namna ya kuona tunabadilishana uzoefu. Hata hapa juzi tulikuwa na kongamano zuri pale Dar-es-Salaam, yote ni kuona kwamba, tunashirikisha wataalam mbalimbali ili tuweze kuona tunapata elimu nzuri kwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

watendaji, vilevile kutoa elimu kwa wananchi kuona vyanzo vya maji inakuwa ni jukumu la wote, tunavitunza na vyanzo hivi vinabaki kuwa ni endelevu kwa sababu tuna miradi mikubwa ambayo inaendelea kutekelezwa kwa kupitia fedha za Wizara. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MONDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Sikonge, Urambo, Kaliua na Ulyankhulu pamekuwa na shida kubwa sana ya maji kwa muda mrefu, Serikali ilituambia imeshamaliza mchakato wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria.

Je, ni lini kazi hiyo itaanza ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Majimbo hayo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swali litaulizwa kama swali la msingi. Kwa hivyo, Serikali ilete majibu kwa ajili ya Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah kwa ajili ya vyanzo vya maji kwenye hayo maeneo.

Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Nduku – Ntobo unaopatikana katika Halmashauri ya Msalala umechukua muda mrefu sana. Sasa ni lini Serikali italeta fedha ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali hilo ni la msingi kwa hivyo, litajibowi na Serikali kama swali la msingi.

Mheshimiwa Mtemvu, swali la nyongeza.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na miradi karibu mitatu katika Jimbo la Kibamba iliyaoahidiwa itakamilika mwezi Desemba, 2021 mbele ya Mheshimiwa Waziri na mpaka sasa hajakamilika. Miradi hiyo mitatu ni pale Kitopeni kwa ajili ya Msumi, Msakuzi na Makabe, lakinia pia Mabwepande kutoka Malolo kwenda Mpiji Magoe na Kwembe kwenda King'azi A.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kutokamilika kwa miradi hii kwa wakati?

**SPIKA:** Haya, hilo nalo ni swali la msingi kwa hivyo, linapaswa lijibiwe kama swali la msingi. Waheshimiwa Wabunge swali la msingi linauliza kuhusu uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi la uharibifu wa vyanzo vya mito ya maji katika Wilaya ya Namtumbo kutokana na mifugo. Vyanzo hivyo vya maji ndivyo vinatiririsha maji katika Mto wa Luwebu, mto mkuu ambao unakusanyika na kukutana na Mto Kilombero ambao una-form Mto Rufiji na maji yake yanaenda kwenye mradi wa umeme.

Je, Serikali inaweza kusaidia kwenda kudhibiti uharibifu wa mifugo katika vyanzo hivyo vya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote anayoyataja tayari Bonde la Mto Ziwa Nyasa linafanyiwa kazi na tayari mipaka inaendelea kuwekwa ili kuzuia shughuli za kibinadamu kwa wafugaji na wale wanaofanya ukulima mdogomdogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Sikunge unategemea sana Bwawa la Maji la Utyatya ambalo lilijengwa mwaka 1959, kuna uchafuzi mwingi kwa kipindi kirefu, uchafu mwingi umeingia kwenye hilo bwawa. Mwaka 2017/2018 Serikali ilipanga shilingi millioni 400 kwa ajili ya kulisafisha hilo bwawa, lakini haikuleta fedha kwa sababu kuna maeneo ambayo yalitakiwa Halmashauri iweze kuyalinda vizuri na mpaka sasa hivi yameshalindwa vizuri.

Je, hizo fedha zitakuja lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph, Mbunge wa Sikunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, chanzo hicho tutaendelea kuja kukifanya kazi na Bonde husika tayari limeshapewa maagizo. Nami kwa kupitia Bunge lako tukufu naomba niendelee kusisitiza Wakurugenzi wote wa Mabonde waweze kuwajibika kwa sababu vyanzo hivi ni mkakati wetu kama Wizara kuona kwamba, tunavilinda ili viweze kutuletea uendelevu wa miradi ambayo tunaendelea kujenga. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante: -

Mheshimiwa Spika, kuna korongo la Mto Barai katika Kijiji cha Durgeda ambalo linaleta uharibufu katika chemchemi ya Mto Durgeda. Waziri alitoka mwezi huu wa Tatu katika neo lile alisema kwamba, utekelezaji ungeanza ndani ya mwezi mmoja.

Je, lini utekelezaji wa Mto huu Barai utaanza ili kuokoa chemchemi ya Mto Durgeda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel AwaCk, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, korongo hili ni moja ya maeneo ambayo Bonde la Mto Pangani wanashughulika nalo. Hivyo, niseme tu kwamba, shughuli zitaendelea na sasa hivi wapo kwenye maandalizi wanakuja kutekeleza majukumu yao.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mbali ya watu kuharibu mazingira, /mean miti na kadhalika kwenye vyanzo vya maji, kumekuwa na wimbi kubwa la watu kwenda kujenga kwenye vyanzo vya maji kwenye mito na maeneo mengine hatimaye kusababisha maji kushindwa kupita kwenye mikondo yake na wengine ni vigogo tu.

Je, Wizara yako kushirikiana na NEMC mna mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha watu hawaendi kujenga kwenye vyanzo vya maji?(Makof)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Ester kwa kuweza kufuatilia vyanzo vyetu vya maji. Maeneo haya namna yanavyojengwa tunayafanya kazi siyo tu na *NEMC*, tuna Wizara ya Kisikta sasa hivi tunapita huko. Moja ya shughuli tunayofanya ni kukataza na kuondoa wale wote ambao wamejenga kandokando ya vyanzo vya maji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako ya maswali hayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu kutoka Serikalini.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete matangazo ya wageni niliyonayo hapa mbele, lakini kabla sijawatangaza wageni, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge mliosimama sasa mkae, Mheshimiwa Mwijage.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaleta tangazo la wageni kwenu, kwa namna ya kipekee kabisa nitambue uwepo wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa heshima hiyo mliyompa Mheshimiwa Spika mstaafu ambaye yuko nasi siku ya leo. Karibu sana Mheshimiwa Mbunge mwenzetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete kwenu matangazo ya wageni. Tutaanza na wageni walioko jukwaa la Spika.

Wageni 35 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na baadhi ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ruangwa Mheshimiwa Andrew Chikongwe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni 24 wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo, hawa ni wadau wa zao la tumbaku kutoka Tabora na Kahama wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku Ndugu Stanley Mnozya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Nicodemus Maganga ambaao ni marafiki zake kutoka Mbogwe, Mkoa wa Geita, wakiongozwa na ndugu Amani Arson Swila. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambaao ni wanafunzi kutoka Msalala, Shinyanga. Karibuni sana. Tunao pia Madaktari na watoa huduma za macho kutoka hospitali ya macho ya Dkt. Agarwao ya Jijini Dar-es-Salaam ambaao wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kutoa huduma hizo wakiongozwa na Dkt. Emilius Chibuga ambaye ni Daktari Bingwa wa macho. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni ambaao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wageni 59 wa Ruangwa *Students Organisation*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hawa Madaktari waliotangazwa hapa wa macho wanatoa huduma hapa Bungeni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tUende tutumie fursa hii ya kuangalia afya ya macho yetu.

Baada ya tangazo hili la wageni kuna mgeni mwingine wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, huyu ni Brigedia Jeneralist Mstaafu Aloyce Mwanjile ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho. Karibu sana Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho katika Bunge letu. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha  
2022/2023 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Ole Shangai, Mheshimiwa Agnes Hokororo ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi leo kuwa wa kwanza kuchangia bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwanza kwa kuishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa Tabora tulikuwa na ufunguzi wa mradi mkubwa wa reli iendayo mwendo kasi (*SGR*). Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutujali wananchi katika miradi ambayo ni mingi sana kwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ofisi yake hii kwa jinsi ambavyo anachapa kazi na Watendaji wake. Nitakuwa na machache ya kusema, kwenye suala la kuwawezesha vijana kuna miradi ile ya vitalu nyumba na wengine wamewahi kuongelea hapa. Vile vitalu nyumba gharama yake ni kubwa, vitalu nyumba vyta kawaida vinafika mpaka Milioni 12 ambavyo vijana wa kawaida hata wakimaliza kujengewa ule ujuzi hawana uwezo wa kumudu kununua vile vitalu nyumba. Kwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hiyo, ninaomba Serikali iangalie hawa vijana watawezeshwa kwa nchi nzima namna gani wanaweza kupata vile vitalu nyumba kwa bei ambayo ni *affordable*, hawa vijana kila wakimaliza mafunzo wasikae tu bila kazi yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulizungumzia suala pia la bajeti ya wenzetu upande wa *DPP*, wenzangu wengi waliongelea, kwenye ukomo wa bajeti tuliomba waongezewe hata Shilingi Bilioni 10 kwa ajili ya kuwezesha hizo Ofisi za *DPP* ziweze kufanyakazi, kwa sababu kwa kweli mashtaka mengi yanakawia kusikilizwa ni kwa sababu ofisi nyingi Mikoani hazina hawa wenzetu wa ofisi ya *DPP*. Kwa hiyo, mara nyingi wanatumika Askari wale wale wafanye upelelezi, Askari hao hao na waendeshe mashtaka. Sasa nimewahi kusema hawa Askari wakati mwingine wakifika vituoni wanapangiwa kazi zingine, inakuwa siyo rahisi wakafanyakazi za aina mbili. Kwa hiyo, Ofisi ya DPP kwa kweli inahitajika kuwa na usaidizi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sintalisema hili ambalo nimelikuta jana Tabora. Nimekwenda Tabora kushuhudia uwekaji wa jiwe la msingi la *SGR*nimekuta bomoa bomoa ambayo siyo ya kawaida, kwa kweli wananchi wa Tabora Manispaa Mheshimiwa Waziri Mkuu wamebomolewa sana vibanda vyao, hatukatai mimi siungi mkono Miji yetu kuwa michafu, siungi mkono kabisa, Serikali kuisafisha Miji yetu inafanya vizuri ninaunga mkono kabisa kuweka Miji yetu katika hali ya usafi. Kitu ambacho kinanisikitisha ni namna mazoezi yenye weyanavyoendeshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Tabora Manispaa, kwanza wale wa kubomoa wameenda usiku, asubuhi wananchi wale wajasiriamali na wengine wanaamka wanakuta vibanda vimebomolewa, yanatumika matingatinga usiku lakini hata kipindi chenyewe, sasa hivi watu wako kwenye mfungo wa Ramadhani, watu wako kwenye Kwaresma wanamalizia, hivi kulikuwa na haraka gani hawa wananchi wakiwa katika hali hii Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado tuna majibu ambayo tunatakiwa kuwajibu

ugumu wa maisha unaoendelea kipindi hiki na Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea hilo suala, maisha yamepanda tunafahamu vita ya Russia, tunafahamu hiyo Ukraine tunajua kinachoendelea, maisha yamepanda, sasa wananchi wanapobomolewa bila hata kusubiri basi huu mfungo basi upite. Hili limekuwa na haraka gani katika kipindi hiki? Watoto wao wanaowategemea hawa wajasiriamali wamekosa nini sikukuu wote zitakuwa ni mbaya kwao, hawa watoto wamekosa nini?

Mheshimiwa Spika, nafikiri hii *approach* Mheshimiwa Waziri Mkuu tuiangalie kwamba hawa tunawasaidiaje, mbona tunawasaidia hata wahalifu?

Mheshimiwa Spika, niliuliza Mtaalam mmoja wa Manispaa alinijibu kwamba walishirikishwa walikuwa wabishi kwa hiyo tumeamua tena tuwabomolee usiku, kwani kumshirikisha mtu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nini? Wangapi wanashirikishwa hapa wanaambiwa msie, msizini, msifanye hiki na wanaendelea kama kawaida, lakini tunawawekea mpaka Mawakili kuwatetea. Kwa mfano, kesi za mauaji bado zipo tunawawekea Mawakili, kwa nini hawa akina Mama Lishe tusiwatetee? Tuangalie *approach* ya namna gani tunaweza tukafanya, hawa ni Watanzania wenzetu, nchi hii ni ya kwetu sote, tuangalie *approach* ambayo haitakuwa ya kuwaumiza kiasi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yake sisi wengine tofauti na Watendaji wa Serikali hawa waliokuwa wananiambia jana wao ni Watendaji wa Serikali tena mmoja ni Mteule wa Rais, mimi siyo Mteule mimi wanaonifanya niwepo hapa ni wale wananchi lazima niwasemee. Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatukatai kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Tabora Manispaa walioomba wanafika zaidi ya Elfu Moja, maeneo yametengwa yako kama 500, ni kama nusu tu, hawa wengine wanapelekwa wapi? Matokeo yake sasa kila siku tutakuwa ni kuombwa mitaji tu, Wabunge hawa ndiyo wanaoombwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mitaji, maana yake wale sasa kwa kuwabomolea hawana tena mitaji.

Mheshimiwa Spika, kwenye huu mradi ambao unaendelea nchi nzima huu wa *SGR* kwenye ripoti ya watu wa reli watajenga sehemu mbalimbali majengo na hasa kwenye vituo vikubwa yatakuwepo majengo ya biashara, mpaka *shopping malls* zitakuwepo mle, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu imekuwa ni kawaida hata kwenye Halmashauri kunapotengwa maeneo ya nyumba za kufanya biashara au vibanda vya kufanya biashara, wanaanza wao wenyewe Watumishi wa Serikali kuanza kujigawia vile vibanda.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye huu mradi mkubwa hawa wananchi ambao mradi huo wa reli wa *SGR* utapita basi, wapewe kipaumbele kwenye maeneo ya vile vyumba ambavyo vitakuwepo kwa ajili ya biashara ili vijana wetu nao wapate ajira, kuliko hawa wenzenetu wenyewe wa Serikali kuanza kuandika majina mbalimbali na kuchukua vile vibanda halafu wao ndiyo wanafanya biashara.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nirudie kusema kwamba ofisi yako inafanyakazi nzuri na nchi yetu kwa kweli kwa kiwango kikubwa inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Ole Shangai atafatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi na mimi kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya. Kule Ngorongoro kazi kubwa

imefanywa sana na Serikali kwa kutupa miradi mikubwa ya maji, hasa mradi wa vijiji Name ambao unaitwa ni mradi wa Mageri. Nimpongeze na Waziri wa Maji kwamba ameweza kufika na kufuatilia kwa kila hatua, amefika zaidi ya mara tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijawatendea wananchi haki nisipozungumzia suala la bei ya mafuta na vyakula. Kwa sasa hivi kule nje maisha ya wananchi ni magumu sana, kule Loliondo sasa hivi watu wanunuia mafuta ya dumu la lita tano kwa Shilingi 40,000, sukari imeenda Shilingi 3,500 lakini tunakaa huku tunajifungia tunasema ni kwa sababu ya vita vya Ukraine, kuna tatizo kule nje.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali na ninaishauri Serikali ni wakati muafaka sasa Serikali kupita kwa wazalishaji wote na kuangalia kwamba bei ya vyakula na bei ya mafuta je, ni uhalisia au ni *artificial*? Ni muhimu sana Serikali kuliangalia hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo tunalizungumzia la barabara, Wilaya ya Ngorongoro haijaunganishwa na Mkoa wa Arusha haijaunganisha na nchi ya Jirani. Tunaishukuru Serikali kwamba imetupa barabara ya lami ya Kilomita 50 kutoka Loliondo mpaka Sale, lakini bado tunahitaji barabara ya lami kutoka Sale mpaka Mto wa Mbu au Kigongoni. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweze kuiangalia Wilaya ya Ngorongoro kwa sababu maisha ya wananchi yanakuwa magumu kwa sababu hatujaunganishwa na Mkoa wetu wa Arusha na ndio maana hata bei ya vyakula inapanda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya kule Ngorongoro, ninashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amekubali kupokea maoni ya wananchi kuhusiana na eneo la pori tengefu na Ngorongoro. Hiyo ni nia njema ya Serikali na nimshukru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu amekuwa tayari wakati wote tukizungumza na yupo tayari kuwapokea watu wangu, aliwapokea Maleigwanani, akazungumza nao na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tukakubaliana kwamba tutamletea maoni ya wananchi. Kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hilo. Hiyo ni nia njema ambayo itatusaidia kutatua matatizo yaliyopo Ngorongoro. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kulielezea Bunge lako na kuelezea masikitiko yangu kwa mbaadhi ya mambo yanayoendelea sasa hivi. Wananchi wa Ngorongoro hawana shida na mtu yeyote ambaye ana hiaru ya kutoka Ngorongoro naomba niweke wazi hilo, hakuna mtu mwenye shida na mtu yeyote pale. Wale wote waliojiandikisha kwa ajili ya kuondoka kama Serikali ilivyosema hakuna mtu ambaye anawazuia, ninawashangaa waliojitokeza kusema kwamba wanaomba ulinzi wasipewe ulinzi hakuna shida wataondoka kwa amani.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja kwa sasa hivi wale wanaobaki ambao watakuwepo Ngorongoro inaonekana kwamba Serikali inawawekea vikwazo vya kimaendeleo, kuna fedha ambazo zilipelekwa kwa ajili ya vituo vya afya, kwa ajili ya maji, kwa ajili ya madarasa, inaonekana sasa Serikali inahamisha zile fedha kwenda Halmashauri ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, Walimu wameandikiwa vituo vya afya wameandikiwa kwamba hizo fedha zihamishwe ziende Handeni. Ninachojiliza sasa Serikali imeona watu wa muhimu pale Ngorongoro ni wale wanaohiari kuondoka? Wale wanaobaki maisha yao yatakuwaje kama tunawanyima vituo vya afya, kama tunawanyima maji, kama tunawanyima shule; Je, wale wananchi watakuwa sehemu ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwenye zoezi ambalo linaendelea chini ya ofisi ya Mheshimiwa Nape la anuani ya makazi, kule Ngorongoro hakuna zoezi hilo, Tarafa ya Ngorongoro hakuna zoezi hilo kwanini tusiwhahesabu wananchi tukaendelea na *program* zingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake mzuri, lakini ninapenda kumuondoa wasiwasi, wananchi wote ni wa kwetu kule Handeni tunapeleka miradi lakini hata Tarafa ya Ngorongoro kazi inaendelea. Kwa hiyo asubiri bajeti yangu tutamuonesha ni namna gani ambavyo tumejipanda kuhakikisha hata Tarafa ya Ngorongoro miradi inaenda kama kawaida. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa silpokei.

Mheshimiwa Spika, kwa nini sipokei taarifa hiyo, wananchi gani hawa ambao unawasubirisha bajeti nyingine, wakati fedha ambazo zipo kwenye akaunti unaondoa kupeleka Handeni. Leo fedha Shilingi Milioni 500 ambazo zilikuwa kituo cha afya Nainokanoka mnahamisha kupeleka Handeni, fedha Shilingi Milioni 600 kwa ajili ya maji Kata za Alaitolei, Masamburai, Oloirobi na maeneo mengine mnahamisha kwa ajili ya kuwawekea wananchi vikwazo vyatimaendeleo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

anayoifanya katika Jimbo lake, lakini nataka nimhakikishie kwamba hakuna maelekezo yoyote ambayo Wizara ya Maji tumepewa tusiendelee na shughuli za maji pale.

Mheshimiwa Spika, tuna mitambo ambayo ipo inatekeleza uchimbaji pale katika Jimbo lake, nami kama Waziri wa Maji nimefika. Nataka nimhakikishie na shughuli zinaendelea na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupa maelekezo mahsusи ya kuhakikisha visima vile vinakamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Taarifa hiyo naipokea lakini anachozungumza Mheshimiwa Waziri ye ye anazungumzia miradi ya maji inayoendelea Tarafa ya Sale na Loliondo siyo Tarafa ya Ngorongoro, hakuna mrdi wowote wa maji unaoendelea Tarafa ya Ngorongoro hakuna! Sasa hivi miradi yote imesitishwa na Serikali kwa sababu ya kuwawekea wananchi vikwazo nya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunawawekea vikwazo? Wananchi hawa wamekuwa pale kwa miaka 60, *is it a nightmare* tukawaondoa kwa siku moja? Kwa mfano, hospitali ya Endulenii likuwa inapata shilingi milioni 500 kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa ajili ya kuwatibu wananchi imeondolewa pia.

Kwa hiyo, watoto wadogo akinamama wanakufa kwa kukosa huduma!

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali gani hii sasa ambayo inawawekea wananchi vikwazo? Kama tunataka kupunguza watuNgorongoro siyo kwa namna hiyo ya kuwawekea vikwazo nya kimaendeleo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze mwenzangu kwa mchango wake mzuri, lakini nimhakikishie tu na nimuondoe wasiwasi kwamba hata jana Shilingi Milioni 321 zimetengwa kupitia *Global Fund* kuelekea kwenye eneo analolitaja la Endulen. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi kimsingi inawezekana *source* za taarifa zimemtisha lakini nikuombe tu kwamba hilo jambo litasimamiwa na uamini ambacho Waziri wa TAMISEMI amekisema na wengine wanachokuambia, tuanze kushirikiana kuanzia sasa tuone tunaenda Pamoja. Kama ambavyo Waziri Mkuu amekuwa akishirikiana na ninyi basi na hayo mengine tushirikiane kwa pamoja tutakwenda vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai unapokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa hiyo kwa masharti, nendeni kwa wananchi mkawaambie mnachosema hapa. Kwa sababu, kinachosemekana hapa ni ili tu tumalize hapa, lakini kinachoendelea Ngorongoro kama walivyoshauri Wabunge wakati mwingine ni bora Bunge hili likajiridhisha kwamba yanayoendelea Ngorongoro siyo haki kwa wananchi wale!

Mheshimiwa Spika, wakinamama mpaka wasafiri Karatu wakapate huduma za afya sasa hivi, vituo havina dawa wananchi tunawawekea vikwazo vyta kimaendeleo kwa ajili gani?

Mheshimiwa Spika, leo ukijaribu kwenda pale kupita kwenye geti la Ngorongoro wameweka vikwazo kibao, wananchi ili uingie ni lazima uperekuliwe na wengine wanarudishwa hawajui pa kwenda kulala Karatu, unakuta ni mgonjwa alikuja Karatu anazuiliwa getini.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa Serikali inayojali utu, kwa Serikali inaowajali wananchi wake, ni muhimu sana tusifanye zoezi hili la watu kuhiari kutoka Ngorongoro kama

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ndiyo njia ya kuwaumiza wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro wanaobaki. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa ni taarifa ya mwisho kwa mchangiaji Ole Shangai, Mheshimiwa Kundo. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge katika yale ambayo anatamani wananchi wake wafanyiwe. Bahati nzuri tulifika katika Jimbo lake na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwa sababu ni Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wake wanasogezewa huduma za msingi na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, upande wa mawasiliano tunapeleka huduma ya mawasiliano kujenga minara zaidi ya 24 ndani ya Jimbo la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge awe na amani kabisa kwamba ndani ya Jimbo lake la Ngorongoro tunakwenda kufanya kazi nzuri sana, asiwe na wasiwasi kuhusu anuani ya makazi na *Postcode*. Nashukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Shangai unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, sasa taarifa iliyotolewa na Naibu Waziri, Ngorongoro kuna Tarafa tatu, Tarafa ya Loliondo, Tarafa ya Sale na Tarafa ya Ngorongoro ambayo ndiyo naizungumzia. Kama Naibu Waziri ana uhakika kwamba anazungumzia Tarafa ya Ngorongoro naomba *list* ya Kata ambazo utapeleka minara hiyo, ziwe kwenye Tarafa ya Ngorongoro na siyo Tarafa ya Sale na Loliondo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala ambalo lipo liliwasilishwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kwamba, sasa hivi tunaanzisha mashamba darasa ya kulima nyasi kwa ajili ya mifugo. Wakasema kuna moja lipo Loliondo, mimi ninaamini

kwamba Serikali inatakiwa kutatua matatizo ya wananchi wake na tunatakiwa kutatua matatizo kwa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba kwa eneo letu la Loliondo, wananchi wataleta maoni yao chochote kile ambacho kinatakiwa kufanyika tuache mpaka maoni ya wananchi yafike kwanza, tuone wananchi wanavyofikiria kuhusiana na eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nashukuru lakini wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro wasiwekewe vikwazo vyta kimaendeleo. Nashukuru sana (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha Mheshimiwa Abbas Tarimba ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoendelea kuchapa kazi na kuhakikisha maendeleo yanapatikana kila uchao, niwaombe tu tuendelee kumuombe sana Mama yetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kupongeza kazi nzuri zinazofanywa na ofisi ya Waziri Mkuu kwenye maeneo mbalimbali, naomba nitoe ushauri kwenye Wizara ya Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, hasa kwenye eneo la vijana.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwa mwaka wa fedha 2021/2022 fedha ya Mfuko wa Vijana iliyokuwa imetengwa ilitolewa yote Shilingi Bilioni Moja, lakini kwa masikitiko makubwa kwamba fedha hizo ambazo kila mwaka Waheshimiwa Wabunge walivyokuwa wanachangia huku tulikuwa tunasikia kwamba walikuwa wanaomba hizo fedha ziongezwe.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti ya 2020/2021 fedha hizo hazikuwa zimepatikana na mwaka huu ambao tunamalizia sasa Shilingi Bilioni Moja iliyokuwa imetengwa yote ilipatikana lakini matumizi yake kwa vijana ni Shilingi Milioni 205.

Mheshimiwa Spika, lazima kujiuliza na ukiuliza unaambiwa kwamba vijana wa Kitanzania waliokuwa wametengewa fedha Shilingi Bilioni Moja hawakukidhi vigezo vyta kuweza kuitumia hiyo Shilingi Bilioni Moja. Sasa hivyo jukumu la kuwawezesha hawa vijana wakatumie fedha Shilingi Bilioni Moja iliyokuwa imetengwa na imepatikana ili waweze kujikwamua kiuchumi ilikuwa ni jukumu la nani?

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kuwajenjea uwezo na hivyo vigezo vilivyokuwa vimewekwa na Serikali ni vigumu kiasi gani kiasi kwamba vijana wa Kitanzania hata wale wahitimu wa elimu ya juu na kati hawawezi kuvikidhi? Nilikuwa nadhani Serikali kuititia Wizara husika inayo sababu ya kuhakikisha kwamba hivyo vigezo vinajulikana lakini na kuweka utaratibu rahisi ili hao vijana waweze kutumia ama kupata hizo fedha ambazo kimsingi mwisho wa bajeti zitabaki na sijui kama hiyo itakuwa imekuwa ni lengo la kutengwa kwa hizo fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kama jumla ya Shilingi Bilioni Sita imetumika katika *program* ya kukuza ujuzi kwanini isiwiane na Bilioni Moja iliyokuwa imetengwa kwa vijana ili waweze kujikwamua kiuchumi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanyika ya kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa vyo 72 na mafunzo ya usoefu wa kazi kwa wahitimu 2,215 nilikuwa najiuliza fedha hizo zisingeweza kutumika kwa mfano kwa vyo vyta maendeleo ya wananchi, vijana ambao wanahitimu kwenye chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Newala pale Kiduni, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi pale Mtwara – Mtawanya, ili vijana hawa wanapokuwa wamepata huo ujuzi ambazo wamekwenda kujifunza, wakapata mitaji ambayo

itawawezesha kujikwamua kiuchumi, kwa hiyo pengine kuna haja ya kuongeza ama kuweka mipango zaidi ya kuwawezesha vijana kutumia hizo fedha Shiliingi 795,000,000 ambayo mpaka sasa haijaweza kutumika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi, imeonekana kwamba Milioni 25.9 ya Watanzania ndio wanauwezo wa kufanya kazi na kati ya hao Vijana ni Milioni 14.2. Hata hivyo, inaonesha ukosefu wa ajira kwa vijana ni takribani asilimia 12.2, hasa nikawa najiuliza hivyo kweli kama vijana asilimia hii 12 wenye umri wa miaka 15 mpaka 35 tunaamini wengi wao watakuwa wameshamaliza vyuo vikuu na vyuo vya kat, kwanini hii Bilioni Moja isishe yote, ikawapatia ajira wakaweza kujajiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Je, Maafisa Vijana tulionao kwenye Serikali za Mitaa kwenye ngazi ya Mikoa na Wilaya wanatimiza wajibu wao kuhakikisha hizo fedha zinatumika na vijana wanaweza kujajiri?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani hapo kuna kazi ya kufanya ili tuweze kimsingi kuwawezesha vijana kiuchumi na hatimaye suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili nichangie kwenye eneo langu Mkoo wa Mtwara. Nilikuwa naangalia kwamba tunapoelekea sasa hivi tunaanza kuandaa mashamba yetu ya Korosho, lakini changamoto kubwa pamoja na mambo mengine ni ukosefu ama uhaba wa vifungashio kwenye zao la Korosho hasa magunia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kwa vile tunajua Watanzania wote tunategemea kilimo na wananchi wa Mkoo wa Mtwara tunajitahidi kupambana katika kuhakikisha kwamba hicho kilimo cha Korosho kinatukwamua na umaskini, sasa hii changamoto ya mifuko ambayo kimsingi inaonekana kama haijapata tiba kwamba kila inapofika msimu kila mwaka kunakuwa na changamoto ya magunia. Je, hatuwezi

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

tukapanga kabla, hatuvezi tukafanya maoteo ya kupata hayo magunia ili kuondokana na hivyo changamoto. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa na hiyo ingewezekana kama tungweza kutumia viwanda vya ndani, kama kuna hiyo Mikao ambayo inalimwa zao la kimkakati Mkonge tunashindwaje kupata magunia ya kufungasha korosho na hivyo kupelekeea Korosho kurundikwa chini na kukosa ubora kila msimu tunapokuwa tumevuna hizo korosho, ni imani yangu kwa mwaka huu na kwa vile Waziri wa Kilimo anafanyakazi vizuri ni imani yangu kabisa kwamba hiyo changamoto haitatokea tutakapokwenda kwenye msimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niongeze pia na Mnyororo wa thamani tunaposema kwamba korosho lazima ibanguliwe ili bei yake iweze kupanda sasa hata vile viwanda ambavyo tumekuwa tukivilalamika kwamba viboreshwe na vile vilivyokufa vihuishwe, mpaka sasa hivi hatujaona hata kiwanda kimoja ambacho katika Mkoa wa Mtwara kilikuwa kimekufa kimeanza kuboreshwa, sasa huu mnyororo wa thamani hatutaweza kuufanya wala kufikia, kwa hiyo ninaiomba Serikali, naamini Serikali yangu ni sikivu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokwenda katika bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri Mkuu na unajua kabisa namna ambavyo wananchi wa Ruangwa Mkoa wa Lindi na Mtwara hatuna zao lingine zao letu sisi ni korosho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukiimarisha kwenye eneo hili tunauhakika nyumba hizo za nyasi, sijui na nini, wananchi wote watakuwa wanaishi kwenye makazi ya kisasa na tutakuwa pia tuna uwezo wa kuhakikisha kwamba tumejikwamua na tupo kwenye maisha bora na salama.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niunge mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajlandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo matatu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anaendelea kuiongoza nchi yetu kwa hekima na busara ya hali ya juu sana, hivi karibuni Rais Samia aliamua fedha za mkopo wa UVIKO-19 zihadiliwe na kupangiwa matumizi yake katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limetupa sisi kama Wabunge heshima na hadhi tunayostahili, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, vilevile Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha dhamira ya dhati ya kutekeleza kwa kitendo miradi ambayo iliasisiwa na mtangulizi wake marehemu Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Mradi wa bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Reli ya Kisasa, na ujenzi wa daraja la Busisi unaendelea kupatiwa fedha na inatekelezwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Mheshimiwa Rais anaendelea kuzungumza na Viongozi wa Vyama vya Siasa ili kuzungumzia mustakabali wa Taifa letu na kuzungumzia maendeleo ya demokrasia, jambo hili ni muhimu sana katika kuleta umoja, maelewano na amani katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapana shaka tunahitaji sana maridhiano na kama Biblia Takatifu inavyosema ni ‘heri wapatanishi maana hao wataitwa wana wa Mungu’. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili mwaka 1962 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Singapore Lee Kuan Yew aliwahi kutembelea nchi ya Nigeria na Ghana na katika kitabu chake cha kutoka nchi maskini kwenda nchi tajiri alisema, aliona mambo ya kushangaza Nigeria na Ghana na aliporudi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nyumbani kwao Singapore alifanya mukutano na Waandishi wa Habari na akasema maneno haya, ningepewa nafasi ya kuzishauri nchi za Bara la Afrika nini kifanye ili watokomeze umaskini basi ningewashauri mambo mawili:

Kwanza, waimarishe kilimo kwa sababu wanazo fursa kubwa sana za kilimo, wanayo mito, wanayo maziwa, wanayo ardhi, wanayo hali ya hewa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, ningewashauri waimarishe utalii kwa sababu wanavyo vivutio vingi vya utalii. Ninachokiona sasa kinafanywa na Rais Samia Suluhu Hassan hapana shaka inadhihirisha anatekeleza mawazo na fikra hiyo iliyoelezwa na Ndugu Lee Kuan Yew. Hivi karibuni Serikali yetu Tukufu imeonesha dhamira ya dhati ya kutaka kuwekeza kwenye Kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji. Jambo hili ni jambo ambalo linanipa faraja sana kwa sababu nimekuwepo kwenye Bunge hili kwa takribani vipindi vitatu, zimekuwepo kelele za Waheshimiwa Wabunge kuitaka Serikali yetu Tukufu iwekeze kiasi cha kutosha katika kilimo cha umwagiliaji, kile kilio ambacho hakijasikilizwa ipasavyo na kusema kweli jambo hili limekuja katika wakati muafaka sana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi yetu ina eneo lipatalo takribani hekta Milioni 22 linalofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji, lakini kwa bahati mbaya sana mpaka sasa tumewekeza chini ya eneo la ekari 600,000 nadhani hazifiki 600,000. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali kwa mawazo hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wazo hilo la kuwekeza sana kwenye kilimo cha Umwagiliaji, ipo haya ya kuwekeza kwenye vyuo vya utafiti wa kilimo ili tuwapatie vijana wetu maarifa na ujuzi, katika masuala ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameonesha dhamira na nia ya kutekeleza wazo la Lee Kuan Yew ni hili hivi karibuni alishiriki katika kipindi kiitwacho *Royal Tour*, kipindi chenye lengo la

kuitangaza nchi yetu nje ya nchi, kwa ajili ya kuvutia watalii, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, mwaka 1978 aliyekuwa kiongozi wa China Ndugu Deng Xiaoping alizungumza na Rais *Jimmy Carter* wa Marekani na kumuomba aipatie nchi yake nafasi 5,000 za masomo kwa ajili ya vijana wake. *Jimmy Carter* alilikubali wazo hilo, akamwambia nimekubali wazo hilo lakini badala ya kukupatia nafasi 5,000 nitakupatia nafasi 100,000 na kuanzia hapo nchi ya China imeendelea kupeleka vijana wao nchini Marekani ili kuwapatia vijana wao ujuzi na maarifa.

Mheshimiwa Spika, China hii inayoonekana hivi leo ni matokeo ya uamuzi huo, ninaiomba Serikali yetu Tukufu tufanye kila linalowezekana tuwekeze katika sekta ya elimu hasa kama tunataka kuharakisha maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mwanafalsafa mmoja wa zamani wa China aliwahi kusema, ukitaka maendeleo ya muda mfupi panda maua, na ukitaka maendeleo ya miaka 10 panda miti, lakini ukitaka maendeleo ya karne moja somesha watu wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yetu Tukufu ifanye kila linalowezekana aghalau igharamie kuwapeleka vijana masomoni wapatao 1,000 vijana ambaao walifanya vizuri sana katika masomo yao, napendekeza sisi hatuna uwezo wa kupeleka vijana wetu wengi Marekani lakini badala yake angalau tunaweza kuwapeleka vijana wetu Korea, China, India, mahali ambapo gharama za masomo zipo chini kidogo ukilinganisha na Marekani na nchi nyininge za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu moja ya matatizo makubwa sana yanayolikabili BARA la Afrika ni ukosefu wa ujuzi na maarifa na kama Biblia Takatifu inavyosema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe ajandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nimepewa salamu na wananchi wa Kinondoni nimletee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wao wanafurahishwa sana na utendaji wako wa kazi. Wanakuona kila mahali kwenye migogoro kwenye utatuzi wakasema huyu Waziri Mkuu tulienaye anafanana sana kama ile timu iliyotengeneza *gap ya point 10* haishikiki! Mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uendelee na kasi hiyo hakuna mtu atakayekugusa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Rais, alipokuja pale Kinondoni kwa ajili ya kuzindua yale majengo ya *Magomeni Quaters* ambapo wananchi 642 wamepata makazi mapya, hakika wananchi wa Kinondoni wamefurahia sana na sikuwa nimepata nafasi ya kuzungumza, lakini nataka nimwambie kupitia Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais wananchi wa Kinondoni wamefurahi sana na wanamuombea kila la kheri, Mwenyezi Mungu amjalie afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanasema haya kutokana na jinsi Serikali inavyofanya kazi yake kwenye eneo hili la Kinondoni, tunasubiri mradi ambao utaanza mwezi wa Julai *inshallaah* ambao ni mradi wa Mto Msimbazi, maeneo ambayo yalikuwa yanapata mafuriko kila wakati, maeneo ya Kigogo, maeneo ya Mzimuni, maeneo ya Magomeni, yanakwenda kupata sura mpya kwa mradi wa Shilingi Bilioni 240 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wale wanachokiomba Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba hili uli-note, kwamba zitakapokuja taratibu za kulipa fidia basi zifanywe kwa wakati. Kwa sababu wana hofu na lile lillilotokea katika Kata ya Magomeni, Mtaa wa Suna, Kata ya Hananasifu, Mtaa wa

Kawawa na Mtaa wa Hananasifu yenyewe na Mkunguni, wananchi wamevunjiwa njia nyumba zao Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Wizara ya Afya pamoja na watu wa mazingira walikwenda kuvunja zinazofikia 945 wananchi wale mpaka leo wanapata shida, hakuna wakuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, sitaki niyazungumze haya mengi nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu unipe nafasi nikutane na wewe ili nilete hiki kilio cha wananchi wa maeneo kwako na uone jinsi gani utaweba kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, Kinondoni tuna mtandao wa barabara za lami wa kilomita 165 na kwenye Jimbo langu barabara za lami ni kilomita 95.35 na hapa nataka nizungumzie kitu kinachoitwa *spot maintenance* ule ukarabati wa mashimo katika barabara. Eneo hilli ni *gray area* Mheshimiwa Waziri Mkuu, linatisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu Serikali imetenga Shilingi Bilioni 5.6 kwa ajili ya kutengeneza mashimo. Najua Wabunge wengi waliomo humu ndani wanaishi Kinondoni au wanapita Kinondoni. Tuna barabara ambazo zinapata mashimo mara kwa mara, sasa fedha zinazotengwa ni fedha nyingi sana 5.6 *billion Shillings* ni hela nyingi sana kwa ajili ya kuziba mashimo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini naliletu suala hili mbele yako na mbele ya Waziri Mkuu ni kwamba mashimo yale kila siku yanakuwa ni yale yale, huu ni mradi. Leo likitengenezwa shimo lile baada ya miezi mitatu litatengenezwa tena shimo lile lile. Huu ni mradi, kwa sababu fedha nyingi kama zile zinamalizika namna gani? Kwa viraka vidogo vidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka na naiomba Serikali kwanini isiflikirie utaratibu wa kurudi kizamani angalau kwa majaribio katika Jiji la Dar es Salaam, tuna karakana kule llala, tuna karakana pale Mwananyamala pale Kinondoni, kwanini Serikali isitumie na kuwa na vifaa na mafundi wetu wa kutengeneza mashimo yale ili tukaondokana na huu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

utaratibu ambao sasa hivi watu wanatumia fedha nyingi kuziba mashimo yale yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano upo mzuri sana, ukitembea Kinondoni utaona, ukiweka alama pale kuna barabara inaitwa *Tarimba Road* ambapo napita kila siku, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kila baada ya miezi mitatu, lazima itatengenezwa eneo lile lile, hivi hatuoni? Kwenye hilo, nitakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ulisimamie, kwa sababu yawezekana tunaweza tuka-save fedha nyingi kwa utaratibu ambao nimeupendekeza, kwa sababu zamani ulikuwepo utaratibu huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alichukue hili aweze akalifanyie kazi ili aweze kuliangalia, si vibaya ukafanya utafiti *cost benefit analysis* kuweza kujua kama tukiendelea na utaratibu wa sasa hivi ama tukiendelea na utaratibu wa kuwa na karakana zetu kipi kitaifaidisha Serikali na kuweza kuipa thamani ya fedha kwenye maeneo haya. (*Makofi*)

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpembenwe.

### **TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba anachokisema ni kitu sahihi kwa sababu hata pale katika barabara ya Msimbazi kuna wawakilishi ambao wanaiwakilisha nchi mashindano ya kimataifa, barabara pale siyo nzuri. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, malizia mchango wako.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa sababu hii taarifa siwezi nikaipokea kwa sababu sijapita hiyo barabara bahati mbaya niko Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuliseme ni usimamizi wa miradi ambayo Serikali inawekeza fedha nyingi sana. Pale Kinondoni, kuna maeneo ambayo yanapata sana mafuriko wakati wa mvua. Kata za Dugumbi, Kata ya Tandale, Kata ya Makumbusho, Kata ya Magomeni, Kata ya Mwananyamala na Kata ya Hananasifu, kuna Mto ambao unaanza Sinza kwa Mheshimiwa Profesa Kitila, ule mto unakuja unapita unaitwa Mto Ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 2019 ilipata Mkandarasi anaitwa *CHICO* kampuni moja ya Kichina, kwa thamani ya Shilingi Bilioni 32.5. mpaka tunavyozungumza mradi huu ultakiwa umalizike mwaka 2019 ambapo ndiyo umeanza na umalizike Desemba, 2020.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mradi huu haujamalizika, Mkandarasi hayupo katika eneo la kazi na ameshalipwa shilingi bilioni 20 kati ya zile Shilingi Bilioni 32. Kazi iliyo fanyika ni asilimia 76 na ameongezewa muda mpaka mwaka jana tarehe 31 Desemba, 2021 bado hakuna kinachofanyika, mvua zinaweza zikaja, wananchi hawa wakaendelea kupata matatizo, ninaiomba Serikali iingilie kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haiyumkiniki Kinondoni mahali ambapo kuna watu wengi, mahali ambapo pana shughuli nyingi na wananchi wale wanaendelea kupata shida katika mafuriko wakati Serikali ilishatenga fedha na ilishalipa fedha asilimia zaidi ya 76.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wananchi wa Kinondoni wameniambia, Serikali Sikivu kama hii na hasa wewe ambaye uko tayari kwenda kila mahali penye matatizo. Juzi ulikuwa Bukoba, kwenda kutatua matatizo ya kilimo ninakutarajia siku moja uibukie pale Kinondoni, ulione hili suala. Naamini kabisa ukionesha rangi yako tunayokujua, siyo rangi ile nyekundu hapana! Rangi yaani kwa maana *your true colors* za uchambaji kazi naamini kabisa wasimamizi wa miradi hii wataona naam! Sasa Serikali iko *serious*. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba kwa sababu pale tulio wengi ni wacha Mungu, tukiomba dua mara nyngi Mwenyezi Mungu anasikia. Tunataka tukuombee Mungu katika eneo hili kwamba na ninyi mnuse nusu fainali, hebu tufanyie hii kazi. Mkitufanyia hii kazi sisi tutakwenda kukesha msikitini tarehe 17 Mwenyezi Mungu awajalie mambo yenu yawe mazuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, unajua mimi ni ‘Walii’ nikizungumza niko katika swaumu basi mambo haya Mwenyezi Mungu atakwenda kuwajalia, mimi ni mtu mwema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa mara nyngine pamoja na Serikali zima kwa kazi nzuri unayofanya na niwatakie kila la heri, Mwenyezi Mungu atujalie, kwa wale ambao wanafunga, Kwaresima Karim, basi Mungu awajalie kila jema na wale walio katika mfungo wa Ramadhani Mwenyezi Mungu awajalie. Hizo ndizo salamu kutoka Kinondoni, nawashukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani atafuatiwa na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigae, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa nafasi hii ya pekee kuendelea kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu. Pia nikupongeze wewe mwenyewe kwa ushindi mnono uliouputa na namna unavyoliendesha Bunge hili kwa hekima na busara na kutambua nafasi za Wabunge wako. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya bajeti

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

aliyoitoa. Kwa kweli, iligusa kila mahali, imegusa uhitaji wa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyoipambania nchi yake, kwa jinsi ambavyo halali anatafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wake wanafaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana kwa upande wa Jimbo la Ushetu, katuletea shilingi 3,200,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya, katuletea Shilingi 1,590,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, katuletea Milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Ulewe. Kweli mama anapambana sana. (*Makofi*)

Mheshimia Spika, Jimbo la Ushetu, liko sehemu ya Wilaya ya Kahama, na Jimbo la Ushetu lina changamoto kubwa sana ya maji. Nikuambie kutoka Ushetu kwenda Kahama ambako mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria upo ni kama kilomita 12 tu, lakini wananchi hawa na Kata zao hawana maji kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya Ushetu ni maji, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya Wizara ya Maji, nakuendelea kuleta watafiti wa maji katika Jimbo la Ushetu, changamoto iliyopo ni maji hayapatikani na wanapochimba wanakutana na vumbi pale chini. Kwa hiyo, ningeomba maji ya Ziwa Victoria yaweze kuletwa kwa wananchi wa Ushetu.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, nadhani unapotoa taarifa utafuata ile miongozo ya taarifa unayoweza kutoa na siyo kwamba unataka kuchangia, Mheshimiwa Iddi Kassim.

## TAARIFA

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka nimpe taarifa mchangia kwamba mwezi wa kumi mwaka jana Wizara ilitenga kiasi cha Shilingi 99, 225,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, mpaka sasa tunazungumza ni kwamba bado hata ule mchakato wa kumpata *consultant* haujakamilika.

**SPIKA:** Hizo Shilingi Milioni 99 ni kwa ajili ya Jimbo lake la Ushetu?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, la Jimbo la Ushetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii naipokea kwa mikono miwili na kwa sababu hiyo, kuna watu walikuja pale kipindi cha nyuma pale baada ya kuuliza sana tukaambiwa kwamba ujazo wa maji ya Ziwa Victoria kwa upande hayawezi kupata uelekeo wa Jimbo la Ushetu, ni jambo la kushangaza, lakini maji hayo ya Ziwa Victoria ambayo yamechukuliwa kutoka Kahama yameenda Nzega, yameenda Tabora, yanaendelea kwenda maeneo mengine zaidi ya kilomita 200, yashindweje kuja kwa wananchi wa Ushetu ambao wanahangaika na kununua maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, toka uhuru kuna Kata hazijawahi kupata hata maji ya kisima, mfano Kata ya Bukomela, Kinamapula, Kata ya Ulewé, Kata ya Ubagwe, Kata ya Ulowa, Kata ya Ushetu, Kata ya Mapamba, Kata ya Ukune. Pamoja na hali ngumu ya maisha ya kupanda kwa vitu hawa wananchi wanunuua maji dumu moja Shilingi 500. Hebu niambie maji yamepanda bei, mafuta yamepanda bei, mafuta ya kula yamepanda bei, sukari imepanda bei, lakini

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wananchi hawa bado wanahangaikia maji ya kunywa.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba suala hili Serikali ilifanyie kazi kwa udharura wake, wananchi hawa wanapakana sana na vijiji vilivyoko katika Wilaya ya Kahama, katika Jimbo la Kahama Mjini. Maji ya Ziwa Victoria yapo, wanashindwa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwa wananchi hawa waweze kufaidika? Wanashindwaje kufanya upembuzi yakinifu kwa haraka na fedha zipo kwa ajili ya Jimbo la Ushetu na wananchi wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana hili nakujua uchapakazi wako, Mama Samia namjua uchapakazi wake, Waziri Mkuu namjua uchapakazi wake, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Maji nawajua uchapakazi wao, naomba suala hili walifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ushetu ni jimbo ambalo pia ni la wakulima kwa kiasi cha asilimia 90, ni kati ya wazalishaji wakubwa sana wa mazao ya mahindi, mpunga pamoja na tumbaku lakini changamoto ni miundombinu.

Mheshimiwa Spika, eneo la Ushetu, lina wafanyabiashara wanaokuja kununua mahindi yao, wanununa mpunga wao hasa katika barabara muhimu sana ambayo tunaomba sana hii barabara itengewe fedha haraka. Barabara inayotoka Masumbwe, kilomita 124.01 inayopita Mwawomba, inayopita Nyankende, inayopita Ulewe, barabara inayopita Ubagwe na inapita Ulowa na inaunganisha Mikoa ya Shinyanga, Geita pamoja na Tabora mpaka eneo la Uyowa. Kwanini barabara hii isianze angalau kutengewa fedha za dharura ifanyiwe matengenezo ya dharura? *(Makofi)*

**MHE NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

## TAARIFA

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka tu nimpe taarifa mchangiaji kwamba barabara anayoizungumzia, inaunganisha mikoa mitatu, kwa hiyo, ni ya muhimu sana hiyo barabara maana inatoka Masumbwi, Mkoa wa Geita, inakuja Ushetu ambaao ni Mkoa wa Shinyanga, inakuja Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo, tunaitegemea sana hiyo barabara Serikali ione kila namna iweze kurekebishwa hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena masharti ya taarifa. Hapa mbele mtaanza kusikia mtu akiaambiwa hiyo siyo taarifa. Mheshimiwa Cherehani, malizia mchango wako.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru lakini pia taarifa hizi ziendelee kuzipokea kwa sababu wananchi hawa sasa tunaelekea kwenye masoko, masoko ya tumbaku, ambapo magari ya wanunuzi wanahitaji watumie hizo barabara kupeleka tumbaku sokoni. Barabara ya kilomita 47 ambayo inatoka Kata ya Ulewe, inapita Kata ya Bulungwa, inaenda moja kwa moja Kahama Mjini maeneo yetu ambapo wakulima wetu wanafanya masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bado kuna kilomita 30 zinazotoka Kata ya Ulowa, kupita Kata ya Ushetu mpaka Uyogo. Barabara hizi magari yanaanguka sana ya wanunuzi, inafika mahali wanunuzi hawa wanaongeza gherama za uendeshaji kwa sababu ya magari yao kukaa muda mrefu kwenye maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana eneo hili barabara hizi muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Ushetu na wananchi wote wanaozunguka maeneo hayo ziweze kutengewa fedha za matengenezo ya dharura. Nimpongeze sana Mheshimiwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuzipandisha barabara hizi hadhi, kuzipeleka kuwa ni za *TANROAD*, ziweze sasa kufanyiwa matengenezo ya dharura, maeneo yote ambayo hayapitiki ili wakulima hawa waweze kusafirisha mazao yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo nataka nijikite kulichangia ni suala la ushirika. Nimpongeza sana Waziri wa Kilimo kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye ushirika. Nimpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa pikipiki zaidi ya 6,000 kwa Maafisa Ugani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala hili tulipe kipaumbele sana hasa kwenye upande wa vyama vyaa ushirika. Tunahitaji wakulima wetu inapopanda bei ya pamba kwenye soko la dunia, inahitaji pia waweze kufaidika wakulima wetu. Wakati mwingine inapopanda bei ya pamba wanashindwa kufaidika wakulima wetu kwa sababu mara nyingi fedha hizi tunazolipa ziweze kulipwa moja kwa moja kwenye akaunti za wakulima wenyewe badala ya kupeleka kwenye *AMCOS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu fedha zinapopelekwa kwenye *AMCOS* unakuta mkulima wa pamba ameshapeleka pamba yake, amelipwa, amepewa *receipt*, lakini mnunuzi anapokuja kupeleka fedha anakuta pamba iko kwenye godauni imejaa, bei imepanda kutoka 1,400 kwenda mpaka 1,700, mfano 1,750 mkulima afaidike na bei hii. Sasa mkulima angelikuwa analipwa kwenye akaunti moja kwa moja, mnunuzi angekuwa anapeleka fedha moja kwenye akaunti ya mkulima. Kwa hiyo, mkulima angekuwa anafaidika sana na kupanda kwa bei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala hili liangaliwe sana, namuamini sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo najua atalifanya kazi, ninamwamini sana Waheshimiwa Waziri Mkuu najua atalifanya kazi na nimpongeza tu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri alizofanya kwenye ushirika, amefanya kazi nzuri sana, amerudisha mali nyingi sana za ushirika, amerudisha mali nyingi, magodauni mengi, viwanda vingi,

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ningeoma sasa viwanda hivi viweze kufufuliwa wananchi hawa waweze kufaidika na mali ambazo zimerudishwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mali hizi zimerudishwa lakini bado hazijaanza kuwafaidisha wana ushirika wetu, kwa sababu bado hati nyingi zimeshikiliwa na benki na ningeomba benki zitumie busara sana, kwa sababu wanashikilia hizi hati kwa sababu vyama vinadaiwa lakini wameshikilia hati sasa vyama vinashindwa kujijendesha vyama vinashindwa kutumia hivi viwanda, kwa hiyo mali zinachakaa sasa kwa nini wasikae chini wakubaliane utaratibu wa kulipa madeni yale halafu viwanda hivi vifufuliwe viendelee kufanya kazi badala ya kuendea kuvizua matokeo yake mali zinachakaa umeshikilia hati, lakini hivi viwanda vinaendelea kuchoka na kupunguza thamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo najua hili analiweza lipo ndani ya uwezo wake afuatilie hivi viwanda vyote ambavyo vimeshikiliwa hati zake na mabenki ili wakae wazungumze namna nzuri ya kuweza kufanyakazi na kuanza kurejesha ile mikopo taratibu huku wakiendelea kufanyakazi huku kuendelea kuimarishe viwanda na wakulima wanaendelea kufaidika na ushirika wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru sana lakini niendelee kurudisha shukrani zangu pia kwa mawaziri wanafanyakazi nzuri sana, naendelea kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyogusa maeneo yote muhimu kuhusu mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu kisiasa, kiuchumi,

kijamii na kiutamaduni. Kwa ufupi, utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM, kama inavyoonesha katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaendelea vizuri sana ingawa kumezuka vikwazo ambavyo havikutarajiwa hususan mlipuko wa virusi vya corona, uhaba wa mvua na vita huko Ulaya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye eneo la hali ya uchumi nchini. Kuhusu hali ya uchumi, naishauri Serikali kuwalinda na kuwawezesha wazalishaji wadogo hasa katika sekta za viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi. Ulinzi wa kisera na kisheria kwa wazalishaji wadogo ujikite zaidi kwenye maeneo ya ulinzi wa masoko dhidi ya walangazi na wanyonyaji, ulinzi wa kazi za ubunifu na teknolojia na ulinzi wa rasilimali za ardhi na ikolojia zinazotumiwa na wazalishaji wadogo.

Aidha, wazalishaji wadogo wanahitaji pia kuwezesha na Serikali hasa kwenye masuala ya upatikanaji wa mitaji ya gharama nafuu, utafiti na mafunzo, upatikanaji wa pembejeo na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao, usafirishaji, nishati na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya kiuchumi kwa wazalisaji wadogo inaweza kudorora zaidi pengine kwa muda mrefu kutokana na athari za UVIKO-19, mabadiliko ya hali ya hewa na mfumuko wa bei ya mafuta duniani. Kwa muktadha huu, Serikali inatakiwa kufanya tathmini ya haraka ili kuweza kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu za kulinda na kuwawezesha sekta ya wazalishaji wadogo kulingana na mazingira yaliyopo sasa. Kwa kuwa sekta ya wazalishaji wadogo ndio mhimili wa uchumi wa nchi yetu hasa katika nyanja za ajira, usalama wa chakula, kodi na tozo na kwa kuwa kuna changamoto mpya zilizozuka ghafla katika sekta hii, ipo haja kwa Serikali kuchukua hatua za haraka kuilinda na kuiwawezesha sekta ya wazalishaji wadogo kwa maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huu naomba kuunga mkono hoja.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa maandalizi ya hotuba nzuri ambayo imegusa maeneo mengi ya maisha ya wananchi. Nina ushauri/mchango katika baadhi ya masuala kama ifuatavyo:-

Kwanza, ujuzi kazi ukurasa wa 62-63; kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Elimu, katika nchi yetu asilimia 79.9 ya nguvu kazi yetu ni *low skilled labour* ambao *majority* ni wale waliomaliza darasa la saba. Asilimia 16.6 ni *middle skilled labour* wakati asilimia 3.6 ni *high skilled*.

Hata hivyo kazi kubwa ya shughuli za uzalishaji zinafanywa na hawa asilimia 79.9 ambao tukiwapa ujuzi kazi kama ambavyo inafanyika kupitia ile programu ya kukuza ujuzi tutakuwa tumewasaidia na tumelisaidia Taifa. Nafahamu juu ya ile *national skills development through green house* ambayo inajielekeza zaidi kwenye ujuzi kazi wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tupanue wigo wa mafunzo na hapa nawasilisha ombi mahususi kwa ajili ya mafunzo ya ujuzi kazi kwa vijana wa maeneo ya Kilolo, Mafinga, Mufindi na Njombe ambako uchumi wetu unategemea sana mazao ya misitu. Vijana wetu katika maeneo hayo wakipata mafunzo ya ujuzi kazi katika suala la kuungeza thamani katika mazao ya misitu wanaweza kupata ajira rasmi katika viwanda na hivyo wakawa na mchango kupitia *PAYE/SDL*, lakini pia wanaweza kujajiri wakajijengea uwezo hati wa kuajiri wenzao.

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yanaweza kufanywa kwa kushirikiana na *TFS* na asasi za kijamii kwa maana ya *NGOs* zinazojishughulisha na masuala ya misitu kama vile Panda Miti Kibiashara na *Forestry Development Trust of Tanzania*. Aidha, kupitia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji kwa vijana, tunaweza kuwasaidia vijana hao kwa kuwapa mikopo ya vitendea kazi ili kusaidia ushiriki wao katika uchumi wa mazao ya misitu kwa kuungeza thamani. Kwa mfano hivi sasa zaidi ya asilimia 60 ya mti unapotea kama

waste, lakini wakipata ujuzi kazi na vitendea kazi tunaweza kuhakikisha kuwa *recovery rate* kwa kila mti inapanda kutoka asilimia 40 ya sasa hadi asilimia 90 kwa sababu katika mti ukiacha mbao kuna bidhaa nyingine kama *MDF*, *Plywood* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimeona benki za CRDB na NMB zimetenga fedha kwa ajili ya kilimo kwa mikopo ya riba kati ya asilimia tisa hadi kumi mikopo ambayo tungeweza pia kuelekeza katika sekta ya mazao ya misitu.

Pili ni kuhusu kushirikisha JKT katika uzalishaji wa bidhaa muhimu kama mafuta ya kula na sukari. Wakati wa usalama ni vema vyombo vyetu vikawezeshwa ili kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Ninaamini mabilioni tunayotumia kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi tunaweza kuepuka na kujitosheleza kwa chakula ikiwa tu tutawezesha JKT na Magereza kuzalisha alizeti na ufuta kwa ajili ya viwanda vya ndani. Tukiwa wakweli wa nafsi ni aibu kama Taifa kushindwa kujitosheleza kwa mafuta ya kula wakati ardhi yenyе rutaba tunayo bali ni suala la kuamua tu, tunahitaji *political will* katika suala hili, kama ambavyo tumewashirikisha JKT katika miradi ya ujenzi na tukiwakabidhi jukumu hili ndani ya muda mfupi tutakuwa tumejikwamua na tunaweza kuuza nje na pia kukabiliana na kilio cha kupanda bei kiasi ambacho *we have less control* na yawezekana ni mchezo wa waagizaji. Naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusimamia masuala ya kazi sehemu za kazi kama vile masuala ya OSHA na kadhalika, ninaamini Ofisi ya Waziri ni kichocheo cha uongezekaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *TANESCO* wanasesma wataanza kuagiza nguzo za umeme kutoka nje ya nchi, suala hili litaathiri sana ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Sekta ya mazao ya misitu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa mgeni rasmi kwenye Kongamano la Mazao ya Misitu mwezi Novemba 2021 ni sekta ambayo imeajiri watu wengi vijana kwa wanawake,

Kwa hiyo, hatua ya kuamua kuagiza nguzo za umeme nje ya nchi itaathiri ajira za vijana na wanawake wa mikoa ya Njombe na Iringa na maeneo mengine ya nchi, kuna mnyororo mkubwa wa ajira na kipato, kuna wenyewe mashamba ya nguzo ambaao ni wananchi lakini pia kuna Shamba la Serikali la *Sao Hill* ambalo ndio muuzaji mkubwa wa nguzo. Suala hili litaathiri kipato cha wafuatao; wenyewe mashamba ambaao ni wananchi, Wakala wa Misitu (*TFS*) ambaao wanamiliki Shamba la Serikali la *Sao Hill*, wakataji na wanaomenya nguzo, wanaopakia kwenye malori madogo, wanaosafirisha nguzo kutoka mashambani kufikisha kwa wenyewe viwanda, walioajiriwa na wenyewe viwanda, Halmashauri kwa sababu asilimia 30 ya mapato yetu ya *own source* ni kutokana na nguzo na pia Serikali kwa sababu katika shughuli za nguzo kuna sekta ya usafirishaji ambapo Serikali inapata fedha kupitia *fuel levy*.

Mheshimiwa Spika, ushauri; hoja za *TANESCO/Serikali* kwamba wazalishaji hawana uwezo sio sahihi kwa sababu kutoka viwanda vitano sasa kuna viwanda 18 ambapo uzalishaji kwa mwaka ni mpaka nguzo milioni tatu wakati uhitaji kwa mwaka ni wastani wa nguzo milioni moja, maana yake kuna ziada ya nguzo milioni mbili.

Suala la ubora, sio kweli kwa sababu kuna mfumo wa kupima ubora wa kwanza ukiwa ni *moisture content* ambapo haipaswi izidi asilimia 25 lakini pia suala la *treatment*, viwanda vina mitambo ya kisasa ambayo hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembela moja ya viwanda hivyo cha *Sao Hill Industries*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo na kama kweli tuko *serious* na uchumi wa viwanda, nashauri Serikali iondokane na wazo la kuagiza nje ya nchi nguzo za umeme, nimetaja hapo juu mnyororo wa mapato ya sekta hii, kama Taifa kuanza kuagiza nguzo nje sio tu tunarudi nyuma bali pia tunaathiri suala zima la kazi na ajira. Katika hotuba ya Waziri Mkuu mmezungumzia ujuzi kazi kama kuna mapungufu ndio maana nmeshauri kuwa pamoja na vitalu shamba kwa maana ya ujuzi kazi katika kilimo, Serikali itusaidie kuwa na

programu maalum ya mafunzo ya ujuzi kazi kwa ajili ya sekta ya mazao ya misitu. Naomba kuwasilisha

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyojalia nchi yetu baraka zake katika ustawi wa jamii, amani, demokrasia, uchumi, diplomasia ya mashirikiano na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ilivyotatua changamoto zinazowakabili wananchi katika sekta za elimu, afya, maji, barabara na vitendea mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha binafsi ninakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyezi Mungu akujalie mafanikio mema.

Sasa naomba nitoe mchango wangu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwanza Serikali itazame kwa upana suala la kukabiliana na majanga kutokana na matukio mbalimbali kwa kuja na mkakati wa kukabiliana na matukio yanayojiteza kama vile corona, moto, ukame, mafuriko, viwavi jeshi na milipuko ya magonjwa, kwa kuandaa rasilimali wataalam fedha na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ifanye tathimini ya kina kuhusu mafanikio ya viwanda 100 kwa kila Halmashauri ili kuleta tija zaidi kwenye ajira kama ilivyo kusudia awali; tatu, Serikali ifanye mapitio ya kina ahadi za viongozi wakuu wa Serikali walizotoa wakati wa uchaguzi na ziara wanazofanya mfano ni miaka saba sasa ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John P. Magufuli ya lami kilometra tano, Mbulu Mji ni kilometra 2.5 mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza mwaka mmoja wa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka. Tathmini zinathibitisha mafanikio mazuri ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu. Kutokana na taarifa za Benki ya Dunia, ni Tanzania pekee ambayo uchumi wake umekua kwa asilimia 4.9, wakati nchi karibu zote za Afrika Mashariki zimekua na ukuaji hasi (*negative GDP growth*).

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Nailbu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura zote asilimia 100. Pia napenda kupongeza uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa (*National Competitiveness*). Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 mpaka Februari, 2022 Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa mafanikio mkubwa sana na utekelezaji huu unaonekana mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri zetu. Mafanikio makubwa yamejikita kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, mtandao wa mawasiliano na uboreshaji wa usafiri wa anga. Napongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115). Miradi hii miwili ya *SGR* na umeme, ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wetu na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, uchumi wa dunia umekumbwa kwa kiasi kikubwa na athari za UVIKO-19 na hivi sasa kuathirika zaldi na vita ya Urusi na Ukraine. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Januari, 2022 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kupungua hadi kufikia asilimia 4.4 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka 2021. Hali hiyo inatarajiwa kusababisha kuvurugika zaidi kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma na athari hizo zinaikumba hata Tanzania. Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa za uhaba na upandaji wa bei kwenye bidhaa za petroli, ujenzi, vyakula, nishati na hata pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za UVIKO-19 na vita ya Urusi na Ukraine, Serikali inatakiwa kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana hasa na mfumuko wa bei na kuporomoka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu kuu zingine. Kwa kuzingatia kuyumba kwa uchumi wa dunia, dajeti hii ijielekeze kuchukua hatua za kuimarisha pato la Taifa kupitia sekta za kilimo, madini, utalii na uchukuzi. Hatua hizi ziende sambamba na kuimarisha mazingiara ya uwekezaji hasa kwenye sekta ya kilimo na madini. Kutokana na mfumuko wa bei kwenye bidhaa za petroli na mtikisiko wa thamani ya shilingi, kutapelekea mahitaji zaidi ya fedha za kigeni na hivyo msukumo uwepo kwenye kuongeza uzalishaji wa madini na mazao ya kilimo.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Hatua hizi ni muhimu kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa hasa kwenye kigezo za ulipaji wa deni la nje kwa kulingamisha na uuzaajii wa bidhaa nje (mapato ya fedha za kigeni).

Mheshimiwa Spika, pamoja na msukumo kwenye kilimo, madini na utalii, Serikali inatakiwa kuwekeza hasa kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara, reli, bandari na usafiri wa anga hasa kwa mizigo. Katika Halmashauri zetu tumekuwa tunakabiliwa na changamoto hasa kwenye miundombinu ya barabara. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, barabara zinazohudumiwa na *TARURA* kwa asilimia zaidi ya 80 zipo kwenye hali mbaya sana kutoka na mafuriko. Maeneo mengi ya vijijini barabara hazipitiki kutokana na madaraja kusombwa na mafuriko. Naomba Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru hali hii ili wananchi waweze angalau kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke msukumo zaidi kwenye kuboresha miundombinu ya barabara kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo. Kutokana na fursa za uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza muendelezo wa uboreshaji wa barabara za *TANZAM* kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya Mbalizi - Shigamba - Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi - Galula - Makongorosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje - Kikondo - Makete ambayo ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya kilimo ikiwemo maua, parachichi na viazi kwa soko la nje. Uboreshaji wa barabara hizi pamoja na uwanja wa ndege wa Songwe ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje, na kwa kiasi kikubwa utaongeza mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za vita ya Urusi na Ukraine, bado kuna fursa kubwa kwa Tanzania hasa kwenye uzalishaji wa ziada wa mazao mbalimbali na hasa nafaka kuziba pengo la nafaka kutoka Urusi na Ukraine kwenda nchi kadhaa za Afrika na mabara mengine. Serikali iimarishe upatikanaji wa pembejeo bora kwa bei nafuu na

kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika. Kutokana na jitihada walizofanya Wizara ya Kilimo kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ugani, ichochee kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka uzalishaji wa sasa ambao upo chini sana ikiwemo uzalishaji wa kilo 1,000 za mahindi kwa eka mpaka kilo 4,000 kwa eka ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuongeza pato la fedha za kigeni, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja yakiwemo reli ya *SGR*, kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapo kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana milima ya *Panda Hill Wilaya ya Mbeya*, na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000.

Mheshimiwa Spika, mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 (dola za Kimarekani milioni 220) ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 (dola za Kimarekani milioni 22) uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kwanza Afrika (*Modern Manufacturing Plant and Smelter*). Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi (*skills transfer*) pia itakuwa itachangia huduma za kijamii (*Corporate Social Investment in Community*) na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu umejielekeza katika ukurasa wa kumi na moja ambapo hotuba hii imejielekeza katika kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga miundombinu rafiki ya usafirishaji abiria na mzigo. Ujenzi wa meli mpya ijuilikanayo kwa jina la Hapa Kazi Tu unaoendelea Mwanza kwa sasa umefikia asilimia 65; ushauri wangu kwa Serikali wale vijana wetu wazawa ambao wameshiriki katika utengenezaji wa meli hiyo itakapomalizika kutengenezwa ni vema kupewa kipaumbele kwa kupatiwa ajira katika meli hiyo kwa sababu ninaimani kubwa pindi wakipatiwa ajira katika meli hiyo watakuwa na uzalendo mkubwa kwa kuitunza ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na pia naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa mambo yafuatayo; kwanza Sheria ya Mfuko wa Maafa, hivi sasa mfuko huu hautumiki au hausaidii maafa yanayotokana na shughuli za uchaguzi jambo ambalo linavunja moyo wa kazi kwa Maafisa Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi, pamoja na wagombea wa ngazi mbalimbali. Mfano katika uchaguzi wa mwaka 2020 katika Wilaya ya Liwale, magari ya Serikali matatu, ya watu binafsi yaliyokodiwa na wasimamizi matatu na magari ya Mbunge matatu, hivyo kufanya magari zaidi ya tisa na mali zingine. Lakini hakuna aliyepata japo kifuta machozi, pamoja na uharibifu huo mkubwa.

Pili, miradi ya kimkakati kwenye Halmashauri zetu nchini; miradi hii ilibuniwa ili kuongeza mapato kwenye Halmashauri zetu, lakini sasa kwenye utekelezaji wa miradi hii inaenda kwa kusuasua sana na pengine haitekelezwi kabisa. Mfano katika Wilaya ya Liwale kulikuwa na mradi wa soko na mradi wa *stand*. Mradi wa *stand* fedha zilikuwa, kutokana kuchelewa kuanza kwa mradi fedha zilirudishwa Hazina. Hadi leo hatujui hatima ya mradi huu.

Tatu, suala la wanyamapori kwenye vijiji au kata zinazopakana na hifadhi hapa nchini imekuwa ni kero kubwa sana juu ya wanyama hao kujeruhi na kula mazao ya wananchi katika maeneo hayo. Nashauri Serikali ione umuhimu wa kuwa na askari wa wanyamapori katika kila kata zilizoko mipakani na hifadhi kama ilivyo kwa polisi kata ili kusaidia kudhibiti wanyama hao na kupunguza madhara. Jambo hili liende sambamba na kulipa kifuta machozi kwa wakati kwa wale waliopata madhara mbalimbali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa njia ya maandishi pamoja na kwamba nimeomba kuchangia lakini napenda kuwasilisha mchango pia kwa sababu ya ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa chama chetu Chama cha Mapinduzi kwa usimamizi imara kabisa wa ilani, mengi yanayofanyika majibu sisi sote na wananchi ni mashuhuda, jimbo la Ndanda lenye kanda mbili hivi sasa kuna miradi mingi inaendelea tena kwa kasi ambayo haijawahi kutokea, miradi ya maji, zahanati, vituo vya afya na mingine mingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri hayo kuna mambo machache ya kurekebisha; kwanza ni suala la *Mtwara Corridor*; nini msimamo wa Serikali kwenye utekelezaji wa mradi huo mkubwa ambao kimsingi ni mhimili mkubwa sana kwenye ujenzi wa uchumi wa Mikoa ya Kusini, kwani inagusa mradi mkubwa wa Liganga na Mchuchuma, uendelezaji wa bandari ya Mtwara na ustawi wake, reli ya Kusini na maboresho ya barabara Mtwara Mbambabay.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeona mambo mengi mazuri ambayo ni kama maono ya binafsi ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hivi ni kwa nini Serikali isifikirie kuona namna ya kuwa na Sheria ya Kilimo kwa ajili ya kulinda mawazo mazuri yote yanayoletwa hapa ndani na Waziri wa Kilimo, kwa sababu siku akibadilishwa inawezakana akaja Waziri mwininge akawa naye na maono yake, lakini mazuri yote

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kama yatalindwa kisheria basi yatakuwa na tija na muendelezo kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili. Tumeona namna alivyohangaika awamu hii Wizara ya Fedha kuhakikisha pesa ya *export levy* inarejeshwa kwa wakulima na amefanikiwa, sasa ije kwenye *Finance Bill* na liwe jambo la kudumu badala ya kuwa ni la matakwa ya mtu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na udhaifu mkubwa sana kwa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Korosho, tumekuwa na kikao na wewe hivi karibuni, tumeongea suala la matumizi mabaya ya ofisi, naamini pia Mwenyekiti wa Bodi anafanya kazi mambo ambayo tuliyasema wakati wa mukutano huo, lakini kwa kifupi waangalie namna anavyofanya kazi zake, kuna watu wamekuwa na madai ya muda mrefu ya *bonds* akiwemo ndugu Kapwapwa kwa jina la Kampuni *TF Commodities Ltd.* ambaye kwa sasa anadaiwa na benki hivyo naye anakusudia kuishtaki *CBT*. Nilitoa mapendekezo kama amekuwa Kaimu kwa miaka mitatu au athibitishwe au aondolewe kwani bodi iliyoko sasa ni mpya.

Tatu, kumekuwa na suala la namba za vijiji kwa muda mrefu sasa, vijiji vya Mkalinga, Sululu ya Leo, Chipunda na vingine vingi, hivi kuna ugumu gani kutoa hizo namba za vijiji wakati vitongoji hivyo vimetimiza vigezo vyote, kuna maombi pia ya kata ya Nambawala ili wananchi waweze kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala pia la mgogoro wa ardhi katika Kata ya Moanyani, umekuwa ni mgogoro wa muda mrefu kama Wizara ya Mambo ya Ndani (Magereza) hawana uwezo wa kulipa fidia wananchi basi watangaze na kuliachia eneo hilo kwani kumekuwa na migogoro kila mara ya maeneo hayo. Bodi pia ina migogoro na wazabuni wa pembejeo kwenye zao la korosho mambo ambayo yanahitaji akili kubwa zaidi kuyatatua kabla hayajaleta migogoro mikubwa uko mbele.

Nne, kuna suala la *inflation*, Serikali iangalie tena uwezekano wa kulirekebisha suala hilo kwani linaleta mzigo mkubwa sana kwa wananchi sambamba na bei ya mafuta,

kwani sehemu karibu nusu ya bei hizo ni tozo, kwa hiyo Serikali iliangalie vyema.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata fursa ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo; hivi mkulima ni nani? Ni vigezo vipi vinafanya umuite mkulima? Je, ile asilimia 76 au 65 ya ajira za wakulima huwa mnaitoa wapi? Je, mnayo orodha ya wakulima wa nchi hii kwa asilimia? Mmewaa nisha kila daraja? Tunalenga kuwa na wakulima wangapi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ije na majibu hayo, tumeona Mheshimiwa Rais ametoa vifaa kwa Maafisa Ugani, ni jambo jema. Tunaitaka Serikali kuitia maafisa hao watuletee sasa majibu hayo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; Serikali ihakikishe wakulima wanapata mafunzo juu ya kilimo bora. Tuwekeze *TAR*/kwenye tafiti ili kupata mbegu mpya na bora, vinginevyo hatutaweza kushindana na wenzetu nchi nytingine. Tuwekeze katika mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ukurasa 26 imeeleza hali ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Takwimu za Wizara zinaonesha mahitaji ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea nchini hadi tarehe 28 Februari, 2022. ni kama ifuatavyo; makadirio ni tani 698,280, jumla ya upatikanaji ni tani 480,848, kilichouzwa ni tani 283,411. Hii inaonesha kuwa pamoja na upatikanaji huo wa mbolea bado wakulima wanashindwa kununua sababu ya gharama hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupanda bei ya mbolea, Urea mfuko kilo 50 imeongezeka kwa wastani wa shilingi 55,000 hadi 130,000 sawa na ongezeko la asilimia 120; CAN

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mfuko mmoja shilingi 34,000 hadi 125000 sawa na ongezeko la asilimia 150; DAP sh 60000 had 120000 ongezeko la asilimia 100. Mfumuko huu utasababisha kuingia kwa baa la njaa siku za usoni na uzalishaji utapungua. Nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka ili kunusuru mfumuko huu wa bei, pia Serikali itoe motisha maalum kwa wawekezaji wa viwanda vya mbolea nchini. Aidha, Serikali ipunguze kiwango cha tozo za mrahaba kwenye malighafi za mbolea zinazochimbwa nchini. Serikali itoe ruzuku kwenye mbolea ili kushusha gharama na bei iwe nafuu kwa wakulima na Serikali iweke bei elekezi ya usambazaji hadi mwisho.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuagiza nguzo nje wakati tuna miti ya kutosha na kuna Kiwanda Dar es Salaam cha nguzo za *cement*, hiyo Italeta upigaji wa hali ya juu.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa ytendaji mzuri katika Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo; miundombinu, afya, maji na elimu.

Mheshimiwa Spika, nianze na miundombinu; naomba Serikali iangalie upya mradi wa *DMDP*, uangaliwe upya kwa umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam na hasa Wilaya ya Kigamboni na Ubungo ziwe kipaumbele. Lakini pia barabara ya Nzasa - Kilungule nayo sasa ikamilike. Mradi umechukua muda mrefu sana. Barabara hii ni muhimu sana kwa wakazi wa Buza na wale wanaoenda Mbande na Kongowe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa vituo vya afya, naomba Serikali iangalie jinsi ya kupanua Hospitali ya Mbagala Zakhiem kwani imezidiwa, idadi ya wagonjwa ni kubwa sana.

Kwa upande wa elimu, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa madarasa mapya, lakini niiombe Serikali sasa iangalie ukarabati wa shule kongwe na hasa maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Kuhusu suala la maji, niiombe Serikali waendelee na mpango wake wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ndio suluhisho la upatikanaji wa maji kwa muda wote katika Mkoa wa Dar es Salaam. Naomba sana Serikali itekeleze mradi huo. Mradi wa Visima vya Kimbiji na Mpera sasa ukamilike ili wananchi wa Kigamboni na Mbagala waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia njia ya maandishi naomba nichangie makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Awali ya yote niunge mkono mwelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mipango na mategemeo yalivyobainisha utekelezaji wake kama tulivyodhamiria utasukuma maendeleo ya Taifa letu kwa kasi kubwa zaidi na kwenda hatua nyingine bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunapoelekeza nguvu na jitihada zetu katika sekta za kiuzalishaji, nichangie suala la migogoro ya ardhi inayohusisha sekta tunazozitegemea zituvushe.

Mheshimiwa Spika, nianze na utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayotegemea sekta za kiuzalishaji; jambo muhimu linalopaswa kuzingatiwa ni kuondoa na kuzuia migogoro kati ya wananchi na wananchi au na wananchi na taasisi za Serikali au wawekezaji. Njia rahisi na ya haki ya kusimamia sekta hii muhimu ni kuzingatia sheria za nchi na kama sheria zina mapungufu basi ziboreshwé.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ya kutolea mfano ambayo migogoro inaibuka kila kukicha na usuluhihi wake unachukua miaka bila kupata muafaka ni ile ya Wilayani Muleba. Mgogoro wa ardhi katika Kata ya Rutoro, kata yenye vijiji vinne na vitongoji 16 chimbuko lake ni utendaji usiozingatia sheria za nchi zilizopo. Mwaka 2005/2006 Serikali ilipopima eneo lenye ukubwa wa hekta 50,000 na kutenga vitalu 18 kwa ajili ya kuwakodisha wafugaji vijiji tajwa hapo juu vilikuwepo. Vijiji vilikuwepo vikiwa na watu ambayo ndiyo rasilimali kuu na namba moja ya Taifa, pamoja na kuwepo vijiji hivyo wakati huo vilikuwa vimesajiliwa kisheria. Kijiji cha Rutoro mwaka 1976 kilikuwa Kitongoji cha Kijiji cha Rwigembe wakati Kata ya Ngenge ilianzishwa toka kata mama ya Rushwa. Wakati huo huo vijiji vya Kyobuheke na Misambya vilikuwa vitongoji vilivyosajiliwa chini ya Kijiji cha Ngenge mwaka 1976. Mwaka 1999 Rutoro ilipandishwa hadhi na kuwa kijiji kwa kufuata sheria za nchi. Lakini kwa kufuata sheria za nchi yetu vijiji vinne vya Rutoro, Kyobuheke, Misambya na Byengerere vikasajiliwa na kuunda Kata ya Rutoro.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa hata kwa mtu mgeni wa sheria usimamiaji mbovu wa sheria ndilo chimbuko na kichocheo cha mgogoro wa Rutoro. Kama ilivyo kwa mgogoro wa Rutoro, MWISA //nayo mgogoro wake umeibuka kwa makosa yale yale yaliyofanyika mwaka 2005/2006 Kata ya Rutoro. Mradi wa NARCO kupima vitalu ili kuwagawia wachungaji wa ng'ombe kwenye kata saba zenye vijiji 12 na vitongoji 19 bila kuzingatia sheria ni kuzalisha mgogoro mpya. Utawala bora kwa kuzingatia sheria unaelekeza matumizi bora ya ardhi na uhaulishaji pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, kiu ya NARCO na Wizara mama yake ya kuwa na maeneo mengi ya kufuga inachochea migogoro kutokana na utendaji wake usiozingatia shughuli zenye tija kubwa. Kimsingi NARCO anachofanya ni kuvamia maeneo, kupima, kuwakodisha wachungaji na kudai kodi. Shughuli yenye tija inapashwa kuanza na utendaji unaozingatia sheria, uendelezaji wa maeneo kwa kulenga ufugaji wenye tija au kuwawezesha wawekezaji wazawa ili waendeshe shughuli kwa tija au na kutafuta wawekezaji

wenye uwezo mkubwa wa kiuwekezaji ili shughuli iwe na tija kwa manufaa ya wadau wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa. Namuombea kila la kheri katika kazi zake.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni Benki ya Maendleo ya Kilimo; napenda kutoa shukurani zangu za dhati kuishukuru Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza mpango wa kuipatia fedha benki hii kwa ajili ya mikopo ya wakulima hasa wadogo wadogo. Benki hii ni mategemeo makubwa kwa wakulima wetu katika ukombozi wa kujinasua kiuchumi.

Ushauri wangu katika jambo hili Serikali iendelee kuhakiki aina ya wakulima wanaostahii kupata mikopo hiyo ili kuepuka kila mwaka kurejea makundi hayo hayo na kuwaacha wengine.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uvuvi; napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada yake kubwa inayochukua katika kuimarisha sekta hii ya uvuvi. Sekta hii ni mionganoni mwa sekta inayowagusa moja kwa moja wananchi wa kipato cha chini. Ushauri wangu kwa Serikali

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

katika sekta hii ya uvuvi ni kuwaendeleza wavuvi hasa wadogo kwa kuwapatia mitaji, aidha kwa njia ya mikopo au kwa ruzuku ili kuweza kujiedeleza na kuweza kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tatu ni uwekezaji; napenda kuipongeza Serikali yetu kwa mipango yake yenye azma ya kutekeleza na kukuza uchumi wa nchi kwa kuvutia wawekezaji katika nchi yetu. Uwekezaji ni jambo jema, likisimamiwa vizuri kwa kuliwekea mazingira mazuri ambayo yatawawutia wawekezaji wa ndani na nje.

Ushauri wangu kwa Serikali juu ya sekta hii ya uwekezaji ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Bado mpaka leo kuna manung'uniko yasiyo rasmi kwamba upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji sio rafiki. Wawekezaji wanachukua muda mrefu kupata maeneo hayo hasa ardhii. Urasimu bado unawasumbua wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Waziri Mkuu wetu kwa hotuba yake nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania na pia niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutupa pesa nyingi za miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Lushoto lina changamoto kama ifuatavyo; kwanza kuna changamoto ya vituo vitatu vya afya ambavyo ni Kata ya Gare, Kata ya Kwai na Kata ya Makanya. Kata zote hizi wananchi wameshaanza kujenga kwa kutumia nguvu zao wenyewe, kwa hiyo wanasubiri tu Serikali nayo iingize nguvu zake kwa kuwapa pesa kama vituo vingine hapa nchini vilivyopata pesa. Takribani ni miaka sita sasa vituo hivi havijapewa pesa yoyote, hivyo basi niiombe Serikali katika kipindi hiki cha bajeti Serikali

itenge fedha za kumalizia vituo hivi ili kuunga mkono juhudii za wananchi wetu na kama unavyojuu ni ahadi tulizowaahidi kwenye kampani zetu.

Mheshimiwa Spika, pili ni changamoto ya maji; katika Jimbo la Lushoto lina kata 15 kati ya kata hizo zenye changamoto ya maji ni kama ifuatavyo; Kata ya Gare yote, Kata ya Kwai hasa Kijiji cha Kwemakame, Kata ya Makanya yote, Kata ya Kwekanga yote, Kata ya Kilole yote, Kata ya Ubiri yote, Kata ya Malibwi yote na Kata ya Migambo yote.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika ya kuwa barabara nazo ndiyo zenye kuchangia pato la Taifa, lakini barabara nyingi za vijiji zina hali mbaya, pamoja ya kwamba *TARURA* wanajitahidi sana, lakini bajeti yao ni ndogo, ushauri wangu Serikali iipatie *TARURA* pesa za kutosha ili ikatatuue matatizo ya barabara hasa katika Jimbo la Lushoto kuna changamoto ya barabara zifuatazo; Doch - Ngulwi hadi Mombo; Mbwei hadi Mavului; Kibao cha Mazumba - Ntambwe hadi Ngalo; Kizara - Ngulu hadi Kwemashai - Kwelugogo; Mmanyai hadi Kwezinga na Kwekanga hadi Mlola.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali yetu tukufu kwa kusambaza umeme katika kila Kijiji pamoja ya kwamba kuna changamoto ya mkandarasi kutoendeleza mradii, kwa maana mradii umesimama, sambamba na hayo katika Jimbo la Lushoto mpaka sasa kuna vijiji zaidi ya 15 na vitongoji ambavyo vimepitiva na umeme 26 havijapata umeme mpaka leo, na kusababisha kero kubwa sana kwa wananchi. Kwa hiyo niiombe Serikali katika kipindi hiki cha bajeti, Serikali itengete pesa ili vijiji hivyo pamoja na vitongoji vyake viweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna maboma mengi ya maabara yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi lakini mpaka sasa maboma yale yanaanguka na katika Jimbo la Lushoto kuna maboma ya maabara zaidi ya 26 bado hayajaendelezwa. Niiombe Serikali itengete pesa za kutosha ili kwenda kumalizia maboma haya ya maabara yaliyoko nchi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nzima ambayo yametumia nguvu za wananchi. Sambamba na hayo Serikali isisahau kujenga nyumba za walimu ili kuwapunguzia kuishi katika nyumba zisizo bora na hatarishi pamoja na kuongeza watumishi wa kada zote.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika kuwa Wilaya ya Lushoto ni ya wakulima wa matunda, lakini mazao haya hayajapewa ruzuku za pembejeo wakati ni mazao ambayo yanaingiza pesa katika Halmahauri zetu, niiombe Serikali iangalie upya ili kuwapatia pembejeo wakulima hawa, sambamba na hayo Lushoto inazalisha kahawa lakini zao hili linakufa kwa sababu wakulima hawajawahi kupewa pembejeo pamoja miche bora. Niiombe Serikali iende Wilayani Lushoto ikafufue zao hili kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanzা kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri walio kwenye Ofisi yake kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao. Nimpongeze yeye binafsi kwa kuwasilisha vyema hotuba ya bajeti na kwa usimamizi mzuri wa shughuli zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye hatma ya wavulana kielimu kutokana na uwepo wa shule chache zilizojengwa maalumu na mahsus kwa ajili ya kuwawezesha wavulana.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini Tanzania mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa fedha za kujenga shule moja maalumu ya sayansi kwa ajili ya wasichana katika kila mkoa. Ujenzi huu haujafanyika kwa wavulana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upendeleo nilioeleza hapo juu, hapa nchini kuna uwekezaji mkubwa sana kwenye shule bora za wasichana. Uwekezaji mkubwa umefanywa na taasisi za dini na watu binafsi. Kutokana na uwekezaji huu,

shule hizi za wasichana zina ufaulu mzuri sana kwenye matokeo ya kidato cha nne na sita. Mfano wa shule bora binafsi zeny ufaulu mkubwa ni pamoja na *St. Fransis Girls - Mbeya*, *Barbo Johansson Model Girls - Dar es Salaam*, *St. Christian Girls - Tanga*, *Loretto Girls - Mwanza*, *Samaritan Girls Secondary School - Shinyanga*, *Anwarite Girls Secondary-Kilimanjaro*, *Precious Blood - Arusha*, *Bethel Sabbs Girls Secondary School*, *St. Theresa of Avila Girls Secondary*, *Hekima Girls Secondary School - Kagera*, *Visitation Girls School - Kilimanjaro*, *Kandoto Science Girls Secondary - Kilimanjaro*, *Marian Girls - Pwani*, *Feza Girls - Dar es Salaam*, *Kibosho Girls Secondary - Kilimanjaro*, *Mazinde Girls - Tanga*, *Kifungilo Girls - Tanga*, *St Mary's High School - Dar es Salaam*, *John the Baptist Girls Secondary School - Dar es Salaam*, *Kunduchi Girls Islamic High School - Dar es Salaam*, *Bethsaida Girl's Secondary School - Dar es Salaam*, *St. Marie Eugenie Girls Secondary School - Kilimanjaro*, *Joyland Girls Secondary School - Kilimanjaro*, *St. Christina Girls Secondary School - Tanga* na *St. Clara Girls Secondary School - Kilimanjaro*.

Mheshimiwa Spika, idadi ya shule binafsi za wasichana ni kubwa, na hapo juu nimetoa mifano michache.

Kwa upande wa wavulana, uwekezaji wa kimkakati ni mdogo sana. Shule zinazomilikiwa na kuendeshwa na taasisi na watu binafsi zeny majina makubwa ni chache. Ninazoweza kuzitaja ni zile za seminari, *Marian Boys*, *Feza Boys*, *Tengeru Boys* na nyngine chache ambazo sijazitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, idadi kubwa ya wasichana wanaosoma katika hizi shule binafsi nilizotaja hapo juu hufaulu vizuri na wengi wao hufanikiwa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hapa nchini. Kwa kifupi, mazingira ya kuwasaidia wasichana kujiendeleza zaidi ni mazuri kuliko ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, tusipochukua hatua za kimakusudi kusaidia watoto wa kiume kwa kuwajengea shule maalumu, huko mbele ya safari uwepo wao katika vyuo vya elimu ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

juu utakuwa na walakini. Dalili za awali zinaonesha kuwa idadi ya wavulana wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu inapungua na ya wasichana inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya hapo juu, ninaishauri Serikali yafuatayo; kwanza ijenge shule maalumu za sayansi za wavulana kila mkoa kama walivyofanya kwa wasichana na pili, iwasiliane na wadau wa maendeleo na kuwashawishi wajenge shule maalumu zenyenye hadhi kubwa kwa ajili ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, wavulana watakuwa wametendewa haki kama ilivyofanyika kuwajengea watoto wa kike shule maalumu katika kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wa maandishi kuhusu tohara ya kitabibu na natambua juhudhi za Serikali katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wanaume wengi kujitokeza kufanya tohara lakini bado baadhi wanaona aibu, nashauri *campaign* iendelee pia kwa kuwashirikisha wale wanaume waliofanyiwa tohara wakiwa na umri mkubwa na pia Wabunge na viongozi wanaotoka maeneo yasiyofanya tohara kwa wanaume wafanye *campaign* hiyo ili kupunguza maambukizi mapya ya *VVU*. Hali kadhalika ushauri utolewe kuwa watoto wa kiume watahiriwe wakiwa wadogo ili kuwaondolea kadhia ya kutahiriwa katika umri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa miradi mikubwa Wilayani Muleba katika nyanja za afya, elimu, maji, miundombinu, umeme na kadhalika. Kwa niaba ya Wanamuleba namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake, namshukuru kwa mikutano wake alioufanya Wilayani Karagwe kwa ajili ya kuboresha bei ya zao la kahawa, hakika wakulima wa zao la kahawa wanatoa pongezi nyingi sana kwa kufuta tozo 42.

Mheshimiwa Spika, nachangia hoja ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 42 kifungu cha 75 kuhusu ardhi. Wilaya ya Muleba ina migogoro miwili mikubwa ya ardhi baina ya Kampuni ya Ranchi (*NARCO*) na wakulima katika Kata ya Rutoro na eneo la *MWISA II*. Nitajikita kwenye mgogoro wa *MWISA II*.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa *MWISA II* ulianza mwaka 2016 baada ya *NARCO* kuvamia eneo la *MWISA II* na kuanza kupima vitalu kwa ajili ya kukodisha wafugaji. Upimaji huo ulihusisha na kuathiri ardhi ya vijiji na vitongoji ambavyo vimepimwa na kusajiliwa kisheria. Huu mgogoro unahuishwa kata saba (Kyebitembe, Karambi, Kasharunga, Mubunda, Burungura, Ngenge na Rutoro) vijiji 12 na vitongoji 19. Upimaji huu unakiuka Sheria ya Ardhi ya Viji, kuna taaruki kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwezi Julai 2021, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvvi alifika Muleba kwa ajili ya kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Baada ya mikutano na kwenda kujiridhisha na hali halisi, tulifikia maridhiano kuwa *NARCO* wasiingilie maeneo ya vitongoji na vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria. Hii ilikuwa faraja kwa wananchi wa vijiji hivyo 12 na vitongoji 19.

Mheshimiwa Spika, *NARCO* wameanza na wanaendelea kuingilia mashamba ya wananchi katika vitongoji vya Kabwensana na Mahigabili katika Kijiji cha Kakoma, Kata ya Burungura na kuanza kuhamisha watu kwa nguvu, kuwanyang'anya mashamba yao na/au kuwagawia watu wengine heka sita kwa kisingizio cha kupanga makazi. Kuna sintofahamu na taharuki kubwa sana. Kulingana na mila na desturi zetu, tunazika wapendwa wetu kwenye mashamba yetu karibu na nyumba zetu. Hamishahamisha

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

hii haizingatii hata sheria ya kuhamisha makaburi ya wapendwa wetu *"The Graves (Removal) Act, Act No. 9* ya 1969.

Naomba Ofisi ya Wazir Mkuu itusaidie kumaliza mgogoro wa MWISA //ambao unahusisha kata saba, vijiji 12 na vitongoji 19. Ni mgogoro unaohushisha eneo kubwa na watu wengi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri. Pia na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo matatu; kwanza *Finance Bill* ijayo ilete na mabadiliko ya matumizi ya fedha za *export levy* kwenye zao la korosho ili zitumike pia kuendeleza sekta ya korosho.

Pili, miradi ya gesi asilia na *LNG* ianze kutekelezwa ili kuinua uchumi wa watu wa Lindi na Mtwara na Watanzania kwa ujumla. Mazungumzo yanayoendelea yaharakishwe na utekelezaji uanze.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Maafa kishughulikie maombi ya Wabunge wa Nanyamba na Tandahimba na barua ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara yanayohusu wananchi wa vijiji viliviyovamiwa na kikundi cha maharamia kutoka Msumbiji wapewe msaada wa kibinadamu. Vijiji hivyo ni Kitaya, Kilimahewa (Nanyamba) na Kilimahewa (Tandahimba).

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza katika eneo la uwezeshaji wananchi kiuchumi, kwanza niipongeze Serikali kwa kuendelea kuratibu programu ya kuongeza ujuzi kitaifa kwa vijana ambayo imekuwa na tija kwa vijana wengi na wananaufaika na fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa tuliyonayo ni vijana hawa wakishahitim masomo yao, kujajiri au kuajiriwa; natambua juhud za Serikali kwamba baadhi ya wahitim wamekuwa wakitafutiwa na kuunganishwa na waajiri wao lakini bado kuna vijana wengi hawajaweza kupata ajira au kuajiriwa kutokana na changamoto ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa vijana Mwanza na Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alituarifu kuwa wataunda benki ya vijana wajasiriamali hapa nchini ili kutatua tatizo la mtaji kwa vijana, na ningeomba kuishauri Serikali; benki hiyo tunaomba izingatie vigezo na masharti nya nafasi ya vijana ambao wengi hawana dhamana ya kukopa, tunaiomba sana Serikali izingatie nafasi ya uchumi wa vijana wengi ambao hawana kazi rasmi na iweze kuwasaidia kuitia mawazo yao ya biashara, matamano ya vijana wengi ni kuona benki hii inakuwa suluhisho la mtaji kwa vijana wengi.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa mtoe hoja wakati anahitimisha hoja yake atueleze mchakato wa kuunda benki ya vijana wajasiriamali umefikia wapi.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuongeza bajeti katika miradi ya maendeleo na maeneo mbalimbali hii inadhilihirisha kuwa kweli uchungu wa mwana aujuae mzazi na hasa mama.

Mheshimiwa Spika, nipende kutoa shukrani kwa Serikali kwa kuongeza bajeti ya maendeleo inayogusa moja kwa moja kwa wananchi hasa bajeti ya Mradi wa TASAF, ujenzi wa barabara za vijijini, upimaji wa ardhi na miradi ya maji. Pia niipongeze sana Serikali hasa kwa kuongeza bajeti ya kushughulikia masuala ya maafa, wote ni mashahidi kuwa nchi yetu hivi karibuni ilikumbwa na maafa, hivyo niipongeze sana Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa ushauri wangu; kwanza mchakato wa kuchagua wanufaika wa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mradi wa *TASAF* uongezwe umakini ili tuweze kupata wanufaika wanaostahili, tofauti na sasa maana kuna baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu wamekuwa wanaingiza wasiostahili bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi, kumekuwa na migogoro mingi japo utatuzi wa migogoro umekuwa wa kusuasua na baadhi ya Mabaraza ya Ardhi yamekuwa chanzo cha migogoro kuongezeka, hivyo nashauri Serikali kuangalia mabaraza haya kwa jicho la kipekee ili yatende haki.

Kuhusu sekta ya afya nazidi kuipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga hospitali kwa kila Wilaya, vituo kwa kila kata na zahanati kwa kila Kijiji. Katika mkoa wetu wa Simiyu tunaomba sana kupewa watalaam zaidi wa afya ili wawewe kuendana na mitambo mipya na ya kisasa ambayo Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa ikileta mkoani kwetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la pamba; hili ni moja ya zao la mkakati ambapo kwa asilimia 50 linazalishwa katika mkoa wa Simiyu, pia niipongeze Serikali hasa Wizara ya Kilimo kuititia Waziri Hussein Bashe na wenzie kwa kugawa vitendea kazi kwa Maafisa Ugani nchi nzima. Nashauri pia motisha iende pia kwa wakulima wa pamba kwa kupandisha bei ya kununulia zao hilo ili kuleta tija kwa wakulima kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeweza kuitekeleza ajenda 10 kwa 30, kilimo ni biashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nashukuru sana na naunga mkono bajeti hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Mheshimiwa *Engineer Andrea Mathew Kundo*, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika mijadala inayoendelea moja ya hoja kubwa ambayo imejadiliwa ni kuhusu mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali hapa nchini na hasa katika kipindi hiki ambapo tupo katika majanga mbalimbali ikiwemo iliyokuwa *UVIKO* pia na yale yanayoendelea huko katika nchi za Ukraine na Urusi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii ya mfumuko wa bei siyo ya Tanzania tu ni maeneo yote au dunia nzima na Serikali tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kuona namna gani tunapunguza makali ya maisha ya wananchi katika kuhakikisha bidhaa nyingi zinapatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa sera ya nchi yetu ni kuona tunaachia nguvu za soko huria katika kuendesha biashara. Hiyo haiachi jukumu la Serikali la kuhakikisha tunalinda ushindani wa haki kwenye soko pia kuhakikisha mlajilae analindwa.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka sote kwamba bei za bidhaa mbalimbali kuanzia mbolea pia bidhaa muhimu kama sukari lakini pia na vifaa vyatya ujenzi, mafuta ya kula na kadhalika vilipanda bei sana, ilianza mwaka jana mwezi wa Desemba.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali tulianza kuchukua hatua za awali za haraka kuhakikisha tunapunguza makali hayo ambayo yanatokana na bei hizi kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, moja ya vitu ambavyo tumefanya kwanza ni kukaa na wazalishaji kuongea nao hasa wale wanaoanzisha bidhaa za ndani. Bidhaa ambazo zilikuwa zimepanda bei sana mwaka jana na hata hivi karibuni zimeendelea nyingine ni pamoja na vifaa vyatya ujenzi. Mtakumbuka vifaa vyatya ujenzi vilikuwa vimepanda sana pia vinywaji baridi, tulipokaa na wazalishaji tulikubaliana na kuona maeneo mahsusini ambayo yalikuwa si sahihi na hasa kupitia Tume ya Ushindani ambao wanajukumu la kuhakikisha sheria ya ushindani inatumika kudhibiti vitendo vyatya kuvuruga mwenendo wa soko au bei ya bidhaa sokoni.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, ninyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge wataona kwamba bei za saruji angalau zimepungua kidogo, ingawaje bado tunaendelea kufanya kazi lakini pia na bei za vinywaji baridi zilipungua lakini pia tunaendelea na kazi hiyo kwa sababu kazi ya kuhakikisha ushindani wa haki na kulinda mlaji ni endelevu siyo kazi ya siku moja.

Mheshimiwa Spika, hivyo tunaendelea kuhakikisha kwamba bei za bidhaa mbalimbali zikiwemo, sasa tumeona bei za vyakula vya kawaida kwa maana ya mchele, maharage na kadhalika navyo pia vimepanda bei. Moja ya changamoto tuliona katika kukaa na wazalishaji na wasafirishaji ilikuwa kwenye eneo la usafirishaji ambalo kimsingi tunaendelea kulifanya kazi ili tuone ni namna gani ya kuhakikisha tunadhibiti upandaji holela wa bei za bidhaa katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mfupi ni hizo lakini pia hatua za muda wa kati ni pamoja na kuendelea sasa kuhakikisha tunaendelea kuweka vivutio au motisha maalum kwa ajili ya uzalishaji wa ndani, kuhakikisha tunawezesha viwanda vyetu vya ndani vinavyozalisha ili viweze kuendelea kuzalisha kwa tija, hii tumeendelea kuchukua hatua ikiwemo tarehe 25 Machi tuliweza kutia saini mikataba ya utekelezaji kati ya makampuni ambayo yapo kwenye miradi ya kimkakati au mahiri hii ikiwemo *Intracom* ambaao wapo hapa Dodoma watazalisha mbolea, pia Bagamoyo *Sugaramba* wataenda kuzalisha sukari pia *Taifa gas*, Kagera *Sugar*, Mtibwa *Sugar* na wale wenzetu *NAFO* ambaao watazalisha *Gypsum Board* na *Gypsum Powder*.

Mheshimiwa Spika, hii mahsusii kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa unaoweza kufanyika ndani ufanyike kwa tija ili kuhakikisha tunapunguza utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunakuwa na uhakika wa kuwa na bidhaa hizi muhimu tunaendelea sasa kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi na bora ili tuweze

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kupata wawekezaji wengine kutoka nje kuhakikisha kwamba bidhaa nydingi tunakuwa na uwezo wa kuzalisha nchini badala ya kutegemea kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeona kwamba mfumuko huu wa bei maeneo makubwa mengi yametokana na tunasema *imported inflation* ambao umetokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali huko nje, hata kwa malighafi ambazo zinatumika katika viwanda vya ndani lakini ambazo zinatoka nje, zile malighafi ambazo zipo ndani tutaona ni namna gani tutahakikisha tunaweka mazingira ili ziweze kuzalisha bidhaa ambazo zitakuwa hazina bei ghali.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**  
Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Omari Kipanga atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Andrea Mathew Kondo*, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alioitoa hapa Bungeni wiki iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tumepokea hoja, mapendekezo na ushauri karibu katika maeneo makubwa manane. Tunaomba tu niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hoja zile na kama Wizara kama Serikali, tumezipokea na tutakwenda kuzifanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe ufanuzi kwenye baadhi ya maeneo machache ambayo tungependa kutoa ufanuzi mbele ya Bunge lako Tukufu. Eneo la kwanza ni kwenye mapitio ya mitaala yetu ni sera pamoja na sheria,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mchakato huu wa kufanya maboresho kwenye mitaala pamoja na sheria yetu unaendelea vizuri, tunataraji mpaka kufika mwaka 2023 mwishoni nadhani tutakuwa tumekamilisha ili kuweza kupata mtaala ambao ninyi Waheshimiwa Wabunge mnadhani ndijo ambao unaweza kusaidia Taifa letu.

Kwa hiyo mchakato huo unaendelea vizuri na niwaondoe wasiwasi, kwa namna moja au nyingine tutaendelea kushirikiana nanyi kuhakikisha mawazo pamoja na ushauri wenu unaweza kuzingatiwa katika mitaala hii mipya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niombe kuchukua hoja ya Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei ambae alizungumzia suala la upungufu wa wafanyakazi au wa walimu katika vyuo vyetu vya ufundi. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Kimei Waziri wa Utumishi jana ametangaza nafasi mbalimbali za ajira na mionganoni mwa nafasi hizo zaidi ya nafasi 2,035 tumepewaa sisi Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie tu Mheshimiwa Kimei na Bunge lako Tukufu kwamba katika maeneo ambayo tutakwenda kuyafanya kazi ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kupunguza upungufu wa Walimu katika vyuo vyetu vya ufundi lakini Wahadhiri katika vyuo vyetu vikuu pamoja na Walimu katika vyuo vyetu vya *FDC* na maeneo mengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kimei jambo hili tunakwenda kulizingatia kwa ukaribu kabisa kuhakikisha kwamba upungufu huu tunakwenda kuupunguza kwa kiasi kikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili; Mheshimiwa Shigongo amezungumzia habari ya uanzishwaji wa Mfuko wa Ubunifu (*National Innovation Fund*), napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Shigongo kwamba mwaka 1995 Serikali kuititia *COSTECH* ilianzisha mfuko huu wawabunifu ambao ulikuwa unaitwa *MTUSATE*. Kwa hiyo, jambo hili tayari Serikali imeshalifanya kazi na kila mwaka Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wabunifu mbalimbali.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 zaidi ya Shilingi Bilioni 3.5 zilitengwa kwa ajili ya mfuko huu lakini kwa mwaka 2022/2023 tumekwenda kutenga zaidi ya Bilioni Tisa kwa ajili ya kuuboresha na kuusimamia mfuko huu ili bunifu zetu zilete tija na kutoa majawabu katika changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho alizungumza Mheshimiwa Kishimba suala la kuwahusisha Askari katika usimamizi wa mitihani. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu katika taratibu zetu za mitihani hasa ile mitihani ya Shule za Msingi pamoja na Sekondari tuna Kamati zetu za Mitihani za Taifa, Kamati za Mitihani za Mikoa pamoja na Kamati za Mitihani zile za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la Halmashauri huwa tunawahusisha Askari katika ulinzi wa mitihani hii la siyo usimamizi wa mitihani kule darasani.

Mheshimiwa Spika, ifahamike tu mitihani wa Darasa la Saba kwa ujumla wake unagharimu zaidi ya Shilingi Bilioni 38.6 sasa tukisema tu kwamba tuuache ule mitihani uende ukafanyike katika mazingira ambayo siyo ya usalama, patakapotokea uvujaji wowote wa mitihani tafsiri yake ni kwamba Taifa linakwenda kuingia hasara ya zaidi ya Shilingi Bilioni 38.6. Kwa hiyo, Askari hawa tumekuwa tukiwahusisha kwenye usafirishaji wa mitihani kutoka katika Mikoa kwenda Halmashauri lakini kutoka Halmashauri kwenda katika *center* ambazo mitihani inafanyika lakini siyo kwamba Askari anaingia katika chumba cha mitihani na kujihusisha moja kwa moja katika usimamizi wa mitihani. Kwa hiyo, Askari wale wapo katika muktadha wa kuhakikisha kwamba usalama wa mitihani wakati inahifadhiwa lakini usalama wa mitihani wakati inafanyika unaenda sawa sawa ili kutoliingiza Taifa kwenye hasara hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho amezungumza mzungumzaji wa mwisho hapa, amezungumza suala la uwekezaji katika elimu na sisi Serikali yetu imewekeza katika eneo hili la elimu, pia amezungumza suala la *scholarship* na

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

vitu vingine hili tutakwenda kuliona katika bajeti yetu ya mwaka 2022/2023 kwamba tumetoa kipaumbele kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba tunapata *scholarship* kwa ajili ya vijana wetu kwenda kupata umahiri na utalaam nje ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu nilikuwa naomba kutoa ufanuzi katika maeneo hayo, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Andrea Mathew Kundo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa ajandae.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOGIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili katika nafasi mbalimbali niweze kutoa ufanuzi katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuyagusa katika Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, nimepitia hoja ya Mheshimiwa Mhata Mbunge wa Nanyumbu kuhusiana na masuala ya ujenzi wa mkongo wa Taifa ambapo matarajio yake ni kwamba mkongo huu unapokamilika basi alitarajia mabadiliko ya bei yatokee katika Jimbo lake la Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ilianza kuwekeza katika ujenzi wa mkongo wa Taifa mwaka 2009 ambapo kufikia mwaka 2021 tayari kilometra 8,319 zilikuwa zimejengwa nchi nzima kwenye Mikoa 25 vilevile Wilaya 43.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha bajeti mwaka jana ya ujenzi wa mkongo wa Taifa takribani Bilioni 170 ambazo ni uwekezaji ambao unaenda kukamilika katika mwaka huu wa fedha ambapo takribani kilometra 4,442 zitawezekana kukamilika, maana yake itakuwa tumefikia asilimia 85 ya lengo la kufikia kilometra 15,000 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, *implication* yake nini ni kwamba tunaweza tukaangalia bei ya mawasiliano kuanzia mwaka 2009 na mpaka sasa mwaka 2022 ili kuona nini Mkongo wa Taifa umesaidia. Mwaka 2009 Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote watakumbuka kupiga simu ilikuwa ni Shilingi 147 kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine hiyo ni kwa wastani, lakini kulikuwa na makampuni mengine ambayo ilikuwa zaidi ya hapo. Vile vile kupiga simu kutoka mtandao mmoja wa *Vodacom* labda kwenda *TiGO* gharama ilikuwa inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, leo hii kutokana na uwekezaji huu wa Serikali kilichofanyika ni mpaka sasa ukipiga simu bila kujunga na kifurushi chochote kile utaweza kutumia Shilingi 30 peke yake bila kujali unapiga kutoka mtandao wa *Vodacom* kwenda *TiGO*, unapiga *TiGO* kwenda *Halotel*/kwa wastani ni Shilingi 30. Hayo ni mapinduzi makubwa ambayo yametokana na Serikali kuwekeza katika ujenzi wa mkongo wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa upande wa Mangaka kwenda Mtambaswala ambapo Serikali imejenga takribani kilometra 72. Lengo kuu la ujenzi wa mkongo ule ni kuhakikisha kwamba tunaenda kutoa huduma katika nchi jirani ya Msumbiji ili tuhakikishe Serikali inajipatia mapato yanayotokana na fedha za kigeni ambapo tukiwa tunatoa huduma ya mkongo wa Taifa, ndiyo maana pale tumeweka *POP* pale Mtambaswala mpakani.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine ambayo yamejitokeza ambayo yamejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, ambayo sana sana ni upatikanaji wa mawasiliano katika maeneo yao. Hili ni takwa la Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 61 (J) ambapo inahitaji Serikali kuhakikisha kwamba inafikisha mawasiliano kwa wananchi wote vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kwa kuona hilo kupitia Sheria Namba 11 ya Mwaka 2006 ambapo mfuko wa mawasiliano kwa wote ulianzishwa mahsusili ili kuondoa pengo lilokuwepo la mawasiliano kati ya Vijijini na Mijini.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa imeshaanza kuwekeza katika maeneo ambayo yameonekana na changamoto ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kuititia mradi wa Tanzania kidigitali, ifikapo mwezi wa Tano inaenda kutangaza zabuni ya maeneo 778 ambapo maeneo haya yote yataenda kufikishiwa huduma ya mawasiliano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ni pamoja na maeneo ambayo Mheshimiwa Shangai Mbunge wa Ngorongoro ambaye alihitaji kutajiwaa maeneo ambayo kuna Kata ambazo hazijafikiwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie uwekezaji ndani ya Wilaya ya Ngorongoro na Kata ambazo Mheshimiwa Mbunge anazihitaji tuko Tayari kumpatia ili ajiridhishe maeneo yake yanaenda kufikishiwa huduma ya mawasiliano. (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa ajiandae, Mheshimiwa January Yussuf Makamba ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, pili nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na maoni waliyoyatoa kwenye hotuba wakati wanachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na niwape tu *commitment* kwamba maoni yao na ushauri wao Wizara tunachukua na kwenda kuufanya kazi na mengi tutayajibu kwenye hotuba yetu ya bajeti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninataka tu niongelee eneo la kwanza kuhusu suala la upandaji wa bei ya mafuta ya kula. Pamoja na kuwa kwamba kuna vitu viwili ambavyo vinasababisha moja ni *production* yetu ya ndani kuwa ndogo hasa kwenye maeneo ya mafuta kama ya alizeti, lakini kama

Serikali tumechukua hatua ya kwanza mwaka huu timesambaza mbegu zaidi ya tani 2,000 na tunaraji kwamba kwenye eneo la uzalishaji katika Mikoa mitatu ya *pilot* tunaweza kuongeza katika uzalishaji wetu wa ndani kwa sababu uzalishaji wetu wa ndani ni wastani wa tani 240,000 za mafuta ya kula, wakati mahitaji yetu ni wastani wa tani 600,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Singida peke yake mbegu za alizeti zitakazozalishwa kutokana na mbegu tani 1,000 tulizopeleka katika Mkoa wa Singida tunataraji uzalishaji wa wastani wa mbegu mpya tani 300,000 ambazo zitatuingizia kwenye uzalishaji wa mafuta lita 100,000 ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba mwakani kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mwaka huu tulisambaza *standard seeds* mwakani tutasambaza *certified seeds* tani 5,000 za alizeti ambayo itakuwa *subsidized*. Kwa hiyo, ninaamini kwamba kufika mwaka 2024/2025 tutakuwa tuna uhakika wa kujitosheleza mafuta ya kula ndani ya nchi na hasa kwa kutumia zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, zao la mchikichi tumeamua kwamba tu-*encourage* uzalishaji wa mashamba makubwa. Tayari tumeshapata wawekezaji wakubwa wawili. Mmoja atawekeza katika eneo la Rufiji na mwingine atawekeza katika Mkoa wa Kigoma na wameshaanza kufanya *soil analysis* na Wizara tunaendelea kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili kama Serikali tunatafakari na kuangaia *tax framework* ambayo inaweza kupunguza gherama ya mafuta. Mojawapo viwanda vyatani ili tuweze kuvipunguzia VAT na kuzifanya kuwa *zero-rated* ili gherama ya mafuta ya viwanda viwe *competitive* na viweze kupunguza bei ya mafuta siku ya mwisho na kuvifanya kuwa *competitive*. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itakapo-*table* bajeti mwezi wa Saba mtaona *measures* mbili za upande wa uzalishaji, vilevile mtaona *measure* za kidodi ambazo zitaweza kusaidia uzaishaji wa ndani lakini vile vile hata mafuta tunayo-*import* kutoka nje kuweza kuyapunguzia bei.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka nichangie, niwape uhakika Waheshimiwa Wabunge hatuna upungufu wa chakula ndani ya nchi. Hatuna upungufu wa chakula ndani ya nchi na kama Serikali tuna-*reserve* ya kutosha ambayo kwa zaidi ya miaka saba hatujawahi kuwa na *reserve* ya namna hii ya zaidi ya *metric tons* Laki Mbili ya chakula ndani ya nchi. Tukipitisha bajeti *NFRA* attingia sokoni kwenda kununua mazao kwa ajili ya kuhifadhi ili tusiweze kuingia kwenye matatizo ya upungufu wa chakula ndani ya nchi, bila ku-*disturb* biashara ya mazao.

Mheshimiwa Spika, nishauri Waheshimiwa Wabunge tusi-*restrict* biashara ya mazao kwa hofu yoyote ile, kwa sababu kama Serikali tutatumia *measure* tulizonazo kuweza kupunguza mfumuko wa bei pale ambapo mahindi yamepanda, tutapeleka mahindi kwa bei ya Serikali ili kupunguza bei. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme jambo lingine kuhusu zao la korosho. Serikali mwaka jana tulifanya *intervention*ya kutoa pembejeo bila kulipia kwa wakulima, imetusaidia uzalishaji wa korosho msimu huu umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 10 kutoka wastani wa tani 206,000 kukaribia tani 240,000. Mwaka huu tena tutapeleka pembejeo zenye thamani ya Shilingi Bilioni 90 bure kwa wakulima wa korosho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tutapeleka pembejeo zenye thamani ya shilingi bilioni 56 kwa wakulima wa pamba. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kuhusu kutafuta njia kuanzia tarehe 01 Julai ya kupunguza bei ya mboleo kwa mazao na Serikali tunachukua hatua ili kuweza kuwapunguzia. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu korosho jambo moja nataka nitumie Bunge lako. Vyama vya Ushirika vilikusanya fedha za wakulima ili waweze kuchangia kununua pembejeo, kupitia Bunge lako kuviagiza Vyama vya Ushirika vyote virudishe fedha za wakulima wote. Wakulima watapata pembejeo bila kulipia, kwa sababu Serikali inaitumia *export levy* kwa ajili ya ku-support zao hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka niongelee hoja ya Mama Kilango.

**SPIKA:** Sekunde 30.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ok. Nataka tu nimuombe Mheshimiwa Mama Kilango na Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga na maeneo yanayozalisha mazao ya viungo. Serikali imeiagiza *TAR*/kupitia *TARI*/Mlingano kuanzia sasa uzalishaji wa mbegu na *research* zote za mazao ya viungo itafanyika kwenye Taasisi yetu ya *TARI* - Mlingano na tunaanza uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya tangawizi na mazao mengine ya viungo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe kwamba haikuwepo kwenye *plan* ya Serikali kwa muda mrefu zao la viungo kama zao la kimkakati, sasa limeingia kama *component* ya mazao ya *horticulture* na tutatoa utaratibu unaostahili. Nashukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa January Yussuf Makamba. Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami ninakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia kwenye hotuba yetu hii iliyoko mbele yetu. Pili, napenda kusema kwanza ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja tatu ambazo zimewasilishwa kwa upande wa Wizara yetu. Hoja ya kwanza

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ni kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa -*Standard Gauge*. Kama tunavyokumbuka reli ya kisasa *Standard Gauge* ilianza mwaka 2017 na ina urefu wa takribani kilomita 1,219 kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza. Reli hii imegawanyika katika vipande vitano. Kipande cha kwanza ni kutoka Dar es Saalam mpaka Morogoro chenye urefu wa kilomita 300, kati ya kilomita 300 kilometra 205 ni za njia kuu na kilometra 95 ni za kupishana. Kipande hiki kinajengwa kwa gharama ya takribani dola za Kimarekani bilioni 1.215 sawa na Shilingi Triliioni 2.7 za Kitanzania. Maendeleo ya ujenzi wa kipande hiki umefikia asilimi 95.72. Bei kwa kilomita moja ni takribani Dola Milioni 4.05 hii gharama inajumlisha na VAT.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaweka mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kipande hiki Wakandarasi wengi walichukua *tender document* lakini mwisho wa siku ni mkandarasi mmoja tu aliyerudisha hiyo *tender document* ambaye ni *Yepi*. Tulimpa kazi hiyo kwa kutumia kigezo chetu tulichojojiwekea ambayo ni *engineering estimation*. Kwa vile kazi hiyo inaenda vizuri na tumefikia asilimia hiyo nategemea mwezi Mei tutaanza kufanya majoribio kwa ajili ya treni ya kwanza ya umeme itaanza kupita.

Mheshimiwa Spika, kipande cha pili ni kutoka Morogoro mpaka Makutupola chenye jumla ya kilomita 422. Kati ya kilomita hizo kilomita 336 ni za njia kuu na kilomita 86 ni njia za kupishana. Gharama ya mradi huo ni Dola Bilioni 1.923 sawa na shilingi triliioni 4.4 za Kitanzania. Ujenzi wake unaendelea na umefikia asilimia 82.68. Gharama kwa kila kilomita moja ni takribani dola za Kimarekani milioni 4.55 na gharama inaongezeka kwa sababu inategemea eneo gani tunapita.

Mheshimiwa Spika, kwa Dar es Salaam ilikuwa hali ni nzuri yaani tambarale lakini kila ukienda baadhi ya maeneo mengine kuna mito, kuna milima hiyo madaraja yanaongezeka, kuna maeneo lazima ujenge mahandaki ili kuhakikisha kwamba reli yako inakuwa salama vizuri.

Mheshimiwa Spika, *lot* nyingine ni *lot* ya tatu na *rote* ya nne. *Lot* hizi mbili tulizitangaza lakini hatukuweza kupata Mkandarasi. Kwa hiyo, tukawajibika kuja na utaratibu mwингine wa *single source* ambao unakubalika kisheria. Kigezo cha kwanza cha *single source* lazima yule Mkandarasi unaemchukua awe na uwezo na uzoefu mkubwa. Pili Mkandarasi huyo awepo kwenye eneo la *site* yenye, yaani anaafanya kazi kama hiyo kwenye *site* hiyo. Kwa vile, katika kipande cha tatu, kipande cha Makutupora mpaka Tabora chenye urefu wa kilomita 368 tulitumia utaratibu huo na gharama ilikuwa Dola za Kimarekani Bilioni 1.908 sawa na Shilingi Triliuni 4.41.

Mheshimiwa Spika, jana tumeweke jiwe la msingi kwa ajili ya kipande hicho na sasa tumeshamlipa Mkandarasi takribani Shilingi Bilioni 609.36. Mkandarasi hapa ni *Yepi* na ndiyo anaanza sasa hivi kuweka vifaa, gharama kwa kilomita Moja ni takribani dola za Kimarekani Milioni 5.14. Hapa mnaona gharama inaanza kuongezeka kwa sababu tunapita kwenye milima, tunapita kwenye maeneo yenye tetemeko. Kwa vile reli yetu lazima ijengwe imara zaidi kuliko maeneo mengine ambayo hayana changamoto hizi za kijografia.

Mheshimiwa Spika, kipande kingine ni kutoka Tabora – Isaka chenyewe kina urefu wa kilomita 168. Tumefanya utaratibu kama huu wa *single source* lakini mpaka sasa hatujakubaliana na Mkandarasi kwa sababu Mkandarasi ameleta bei ya juu ukilinganisha na bei tuliyojiwekea yaani *engineering estimation*. Bado mazungumzo yanaendelea na tunaamini Mkandarasi atashuka vizuri ili bei tutakayoipata hapa iendane na *engineering estimation* ambayo tuliiweka hapo zamani.

Mheshimiwa Spika, kipande cha tano ambacho kinaendelea ni kipande cha kutoka Isaka mpaka Mwanza chenye urefu wa kilomita 341. Kipande hiki kina urefu wa kilomita 249 njia kuu na kilomita 92 njia za kupishana. Kazi inaendelea na *mobilization* inaendelea na Mkandarasi amefika asilimia 4.46.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi hapa ni .....

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, maelezo mengi nitatoa wakati tutakapoleta bajeti yetu. Naomba tu kuunga mkono hoja kama nilivyosema kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza.  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa January Yussuf Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu. Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi ajiandae.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii uliyonipa. Nami niungane na wenzangu kuwashukuru sana Wabunge wote waliochangia hoja hii na waliochangia kwenye eneo linalohusu sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, yaliyochangiwa ni mengi, muda uliopo wa kuyajibu yote hautoshi. Kwa hiyo, tutayajibu kwa maandishi namba moja, namba mbili tutayajibu wakati wa bajeti yetu ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu niseme kwa baadhi ya mambo hasa ndugu zetu wa Mikoa ya Iringa na Njombe kwenye masuala ya nguzo nataka niwahakikishie kwamba nitaenda wiki inayokuja tutakaa, tutayamaliza, tutaelewana kabisa bila wasiwasi wowote na mazao yao yatanufaika na ununuzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye mambo mawili hasa bei ya mafuta. Kwenye sekta ya mafuta kwa ujumla kuna masuala mawili, kuna bei na upatikanaji. Suala la bei limeongeleta kwa kirefu sana ikiwemo na Mawaziri mbalimbali, sababu na mwenendo wa bei ya mafuta umeongeleta.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei ya mafuta katika miezi 16 iliyopita umekuwa ni wa kupanda na umepanda katika nchi zinazozalisha mafuta na nchi zinazoagiza mafuta vilevile. Nchi ya kwanza katika uzalishaji wa mafuta duniani ni Marekani na kwenyewe hata huko bei imepanda. Kwa hiyo, mwenendo ni wa kupanda tofauti ni kwa kiwango na kasi, lakini tofauti pia ni je, hatua zinachukuliwa?

Mheshimiwa S[ika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha juzi aliongelea kuhusu hatua za kikodi kwenye jambo hilo. Mimi nitaongelea hatua za muda wa kati na mrefu katika kuhakikisha kwamba tunahimili katika kipindi kirefu na cha kati bei kubwa ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tumekuwa na ndoto ya kuwa na hifadhi ya kitaifa ya kimkakati ya mafuta. Hatimae mwaka huu ndoto hiyo itatimia, tunaandika kanuni za kuiwezesha kuwepo vilevile tumepata washirika katika uwekezaji wa miundombinu ya ushushaji na uhifadhi wa mafuta ili kuwezesha hifadhi hiyo kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali tunazungumza kuhusu kuanzisha Mfuko wa Kuhimii Ukali wa Bei za Mafuta ambao ni *Fuel Price Stabilization Fund* ambayo katika siku zijazo itatusaidia kutuokea katika nyakati kama hizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaendelea na mazungumzo na wauzaji na wazalishaji mafuta hasa nchi rafiki ambao tuliyaanza tangu mwezi Oktoba mwaka jana ili tuone katika kipindi hiki kama tunaweza kupata nafuu ya kununua mafuta huko moja kwa moja. Kwa hiyo, kuhusu masuala mengine nje ya kikodi Wizara yetu inayafanyia kazi karibu kila siku.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja hapa mchango umetolewa, *bulk procurement system*, bahati nzuri mfumo huu ulikuja kutokana na mapendekezo na maelekezo ya Bunge mwaka 2011 na mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ya Nishati na Madini wakati huo na Bunge kwa kauli moja likaishauri Serikali kuanzisha mfumo huo. Mfumo huo ukaanza na umekuwepo kwa kipindi cha miaka 10. Sasa mfumo huu umewekwa na watu, unaendeshwa na watu. Tumepokea ushauri mzuri sana wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuuboresha mfumo huu. Nasi tupo tayari tumepokea ushauri huo na kama kuna taarifa zozote zinazohusu udhaifu katika mfumo huo na namna ya kuchukua hatua pale kwenye mapungufu basi tuko tayari wakati wote kupokea na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu siyo Msahafu siyo Quran siyo Biblia unaweza kubadilishwa wakati wowote ili kutusaidia pale ambapo tunadhani utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi. Kikubwa tu ni kuwa na mfumo ambao utatuhakikishia uhakika wa kupatikana kwa mafuta lakini na bei ambayo inahimillika.

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba wanao uwezo wa kuisaidia nchi kupata mafuta ya bei nafuu, kwamba yako baharini huko na meli, sisi tunasema mtu ye yote, pahala popote, Mtanzania yyyote mwenye taarifa au uwezo wa kuisaidia nchi kuleta mafuta ya bei nafuu karibu sana ofisini hata leo ili tuzungumze hilo jambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kung'ang'ania kitu kumbe kuna kitu kingine kitatusaidia Zaidi, nchi hii hi yetu wote hatuna shaka yoyote. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge njoo ofisini, kikubwa tu ni kwamba hizo meli zilizopo zituhakikishie kwamba mafuta hayo yataingia *consistence* kwa wakati wote kuhakikisha kwamba *supply* ipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni upatikana wa mafuta. Ni muhimu...

**SPIKA:** Sekunde 30.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, katika janga kubwa linaloweza kutokea ni kukosekana mafuta. Bei ni jambo tunaweza tukalizungumza lakini kukosekana mafuta kwenye vituo, kuwepo na foleni, kuwepo na vigaloni kwenye majumba yetu ni hatari kubwa zaidi. Nataka ni wahakikishie Watanzania kwamba kwa nchi yetu ukilinganisha na majirani zetu mafuta yakutosha yapo juu ya kiwango cha kanuni tulizoweka ya siku 15. Kwa hiyo, mafuta yapo na Serikali itahakikisha kwamba yanaendelea kuwepo ili uchumi usisimame. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu atafuatiwa na Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi. Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Nami naomba kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri jinsi gani tunaweza kuboresha upatikana wa huduma za afya kwa Watanzania, mengi tutayajibu katika mjadala wa bajeti yetu ya Wizara ya Afya na leo niseme jambo moja ambalo lilielezwa kwenye mjadala huu nalo ni kuhusu umuhimu wa Bohari ya Dawa (*MSD*) kununua dawa kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Tano Mwenyezi Mungu amrehemu uko alipo Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, alipoingia madarakani kati ya jambo moja aliloliezeza ni kututaka Wizara ya Afya kupitia *MSD* kununua dawa moja kutoka viwandani au kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, tulikuja Bungeni kuleta mapendekizo kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kufanya mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi (*Procurement Act*) mwaka 2016. Kwanza tukafanya kipengele cha kuruhusu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

manunuzi ya dharura kwa sababu dawa ni bidhaa za kuokoa maisha. Jambo la pili kukaingizwa *section 65A* ambacho kinasema *a procuring entity or the agency shall for the purpose of obtaining value for money in terms of price, quality and delivery. Procure goods or services directly from the manufacturer, dealer, wholesaler or service provider.* Kwa hiyo, huu ndiyo msimamo wa sheria.

Mheshimiwa Spika, *MSD* hazuiwi na sheria kununua moja kwa moja kutoka viwandani au kwa wazalishaji, lengo kushusha gharama ya dawa. Sheria imeweka mipaka siyo tu gharama, *quality* (ubora) wa dawa, *efficacy* (ufanisi) wa dawa na upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Spika, kanuni za manunuzi ya umma kwa sababu suala hili ni nyeti likaweka utaratibu maalum wa kuwezesha manunuzi ya dawa, vifaa na vifaatiba Kanuni ya kuanzia 139 hadi Kanuni ya 147 na inarudia vilevile kwamba tunayo fursa ya kununua moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, hili nafurahi tulilitekeleza.

Mheshimiwa Spika, 2017 nilipata heshima pia ya kuwa Waziri wa Afya. Tuliingia mikataba 73 na wazalishaji 46 wa dawa kutoka Uganda, Denmark, Ufaransa, Ujeruman, China, Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Bangladesh, India, Kenya na Tanzania. Tuka-*identify* aina za dawa 178 lakini pia vifaatiba 195 na vitendanishi 178. Kwa hiyo, hili suala siyo geni limeshafanyika. Lengo ni kushusha gharama ya dawa.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano. Baada ya utaratibu huu kuanza kutumika mfano dawa ya chanjo ya homa ya ini, *hepatitis 'B'* vaccine kabla ya kununua viwandani ilikuwa inauzwa elfu 22,000 sasa ikashuka mpaka elfu 5,300. Dawa ya sindano ya *diclofenac* kwa ajili ya maumivu vichupa 10 ilikuwa inauzwa Shilingi 2,000 ikashuka mpaka 800/= Dawa ya kupambana na maambukizi ya bakteria *Amoxicillin* miligramu 265 yenye vidonge 15 kwa *supplier* ilikuwa inauzwa 9,800/= ikashuka mpaka 4,000, mashuka yalikuwa yanauzwa elfu 22,000 yakashuka mpaka elfu 11,100.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili jambo na ndiyo muelekeo wa Wizara Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwa ujumla ili kushusha gharama za dawa, dawa zitanunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, wakati tunatafuta unafuu wa dawa hatuta-*compromise* ubora wa dawa lakini pia na usalama wa dawa. Tunafahamu hata leo ukienda kariakoo utapata shati la Shilingi 10,000 lakini kuna shati hilo hilo linauzwa Shilingi 30,000. Shati la Shilingi 10,000 linaweza likakaa siku moja la Shilingi 30,000 likadumu hata mwaka mmoja au miaka miwili. Hili ni jambo lazima pia tuli-*take into consideration*. Kwa hiyo, ninachotaka kumaliza Sheria ya Manunuzi ya Umma haijaweka kikwazo kwa dawa kutonunuliwa moja kwa moja viwandani.

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA:** Tunalifanyia kazi lakini ninachotaka kusema....

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na sisi tutaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa salama na zenye ubora. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga. Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema, pia nishukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunitueua na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kuniamini na kunipa dhamana ya kuweza kuwatumikia Watanzania, ninamuahidi ye ye pamoja na viongozi wengine Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu, uadilifu lakini katika kusaidia Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze na kukushukuru pia wewe kwa kuendesha Bunge lako vizuri pamoja na uongozi wote wa Bunge aidha niwapongeze pia Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambao wametusaidia katika majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninaupongeza muhimili wa Mahakama na viongozi wengine pamoja na vyombo vyaa ulinzi na usalama kwa kuendelea kulisimamia Taifa letu kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda njielekeze katika mambo ambayo yamezungumzwa zaidi au yamechangiwa zaidi na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nikianza na eneo la ajira. Ofisi ya Waziri Mkuu mbali na majukumu mengi yaliyopo inalo jukumu pia la kuweza kuhakikisha kwamba inasimamia na kuratibu Sera pamoja na sheria zote zinazohusika na masuala ya ajira. Katika msingi huo tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akituelekeza wakati wote tuweze kuwapokea, kuwasikiliza pia kuwashudumia wale wote ambao wanafika katika ofisi hiyo kwa ajili ya kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, katika *study* ambazo tumejaribu kuzifanya ili kutafuta ulinganifu na suluhu ya changamoto za masuala ya ajira nchini, Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wangu wa nchi *Professor Joyce Ndalichako* pamoja na watumishi tumejaribu kufanya *studyn*a ulinganifu mbalimbali katika kuangalia changamoto za ajira kwa nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanya utafiti wa kuangalia na kuandaa taarifa ya uchambuzi wa sera, sheria na mikakati ya nchi mbalimbali kuhusu utatuzi wa

changamoto za ukosefu wa ajira. Katika maeneo ambayo tumejaribu kuangazia mojawapo ilikuwa ni nchi ya Uganda, Rwanda, Brazil, China Marekani, Tunisia, Uturuki, South Afrika na Kenya.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo yote ambayo tumefanya utafiti wenzetu wamefanana pia maeneo mengi na sisi lakini sisi pia tumeenda hatua ya mbali zaidi. Changamoto kubwa ambazo zinaonekana katika wimbi hili kubwa la ukosefu wa ajira, ambalo sehemu nydingi wanaita kama *timing bomb* duniani, sababu zinazosababisha ukosefu au changamoto ya ajira nydingine ni chanya na nydingine hasi.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza ni ongezeko la taasisi za elimu kwa maana ya uhamasa katika kusoma, kumekuwa na wahitimu wengi katika kada mbalimbali tofauti na uhitaji wa ajira. Sababu ya pili ya kidunia inayoelezwa katika takwimu mbalimbali za *International Labour Organization* kwa maana ya shirika la kazi duniani, pamoja na taasisi nydingine ni uwepo wa *advancement* ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa teknolojia umeenda *ku-replace human labor*, kwa maana ya *computer* au *mashine* sasa inaweza ikafanya kazi ya watu zaidi hata ya 100. Sababu nydingine imeelezwa ni masuala ya *natural catastrophic* na *force majeure - acts of God* pamoja na masuala kama ya magonjwa kama vile *COVID-19* ambayo imesababisha viwanda vingi kufungwa na changamoto nydingine pia makampuni na kadhalika kuweza kufilisika.

Mheshimiwa Spika, sababu nydingine ni masuala ya sasa biashara kijumla duniani, Serikali zimeacha kufanya shughuli ya biashara na badala yake zinatoa huduma, kwa hiyo biashara imelekezwa katika *private sector*. Jingine ambalo limeelezwaga katika takwimu ni masuala ya viwango vya elimu inayotolewa, mtu apate *skill* na *knowledge competence and performance* ya kuweza kufanya kazi. Kwa hiyo, wanapimwa kulingana na ubora na hizo ndio wakati mwingine vimeduwa ni vigezo vya kuweza kusaili watu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, sasa nini kimefanyika kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika eneo hili na katika kutafuta njia mbadala sasa za kukabiliana na changamoto hizo. Kwanza katika kufanya hivyo tulifanya pia utafiti wa kuangalia wingi wa vijana wengi ambao wanaingia katika soko la ajira kila mwaka. Katika tafiti tulizozifanya ukiangalia kwa darasa la saba ukiacha kwa sababu ya muda nisianze mwaka 2012 mpaka mwaka 2021 niende kwenye mwaka 2021 peke yake.

Mheshimiwa Spika, wahitimu wa darasa la saba walikuwa milioni moja na laki moja, kidato cha Nne ni Zaidi ya laki nne na themanini na saba elfu, kidato cha sita ni zaidi ya wahitimu elfu themanini, walioweza kufuzu mafunzo ya *VETA* ni zaidi ya laki mbili na thelathini na sita na *FDC* Wahitimu Zaidi ya elfu kumi na moja, lakini pia *NACTE* ni wahitimu elfu themanini na saba. Kwa ujumla ukienda kwenye vyuo vikuu peke yake kwenye soko wanaingia 47 elfu katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kwa sababu ukija kuangalia katika ujumla wake tuna watu zaidi ya laki moja wanohitaji ajira katika soko tofauti na hitaji lilivyo.

Mheshimiwa Spika, hatua tulizozichukuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni:

Moja; kuandaa na kutengeneza uwepo wa vyuo vya *VETA* kama jinsi China walivyofanya vyuo vikuu zaidi ya laki sita wamevibadilisha na kuwa vyuo vya kati kuweza kutoa mafunzo na *skills* za kazi.

Pili; tumeendelea kutoa fedha za mikopo za kuweza kuwasaidia katika ngazi za Halmashauri na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili waweze kupata mitaji ya kuweza kufanya shughuli mbalimbali.

Tatu; kumekuwa na mkakati wa kutengeneza mfumo wa ukuzaji wa ujuzi wa vijana ambao wamekuwa wakitoka vyuo vikuu na wale ambao hawajarasilimishiwa ujuzi, tumekuwa tukitoa fedha kwa ajili ya kurasimisha ujuzi na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa mwaka

wa jana alitoa zaidi ya bilioni tisa ilinufaisha vijana zaidi ya 14,440 katika mafunzo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mafunzo ya .....

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Nderiananga

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ninamshukuru kipekee Mwenyezi Mungu mwengi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kuweza kukutana katika Bunge hili. Nitumie fursa hii kuwatakia heri ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan Waislam wote katika Taifa letu na dunia nzima na niwatakie heri ya kwaresma Wakristo wote.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassani kwa kutimiza mwaka mmoja wa kuchapa kazi kwa weledi na bidi, hongera sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu niende katika hoja za Kamati zetu zote mbili zimeshauri vizuri, na ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri ambayo mmetupatia ili kuboresha eneo letu la bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba fedha za maendeleo zilizotengwa Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya mwitiko wa masuala ya UKIMWI Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Samia tutazitoa fedha zote hizo ndani ya mwezi huu wa Aprili katika robo ya nne hii. Kwa hiyo niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kazi inaendelea vizuri. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, suala la fedha za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya virus vya UKIMWI, niwaambie tu kwamba Serikali imeongeza fedha kutoka kiasi cha Shilingi Bilioni Moja mwaka 2021/2022 na katika bajeti hii ya leo ambayo mtatupitishia Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Samia tumeongeza fedha kwa asilimia 88 na sasa zitakuwa ni Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Nane na Themanini katika mapambano dhidi ya virus vya UKIMWI na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, lipo suala liliongelewa kuhusu mfuko wa mapambano dhidi ya *virus* vya UKIMWI, tumepokea maoni na ushauri wa Kamati yetu ya masuala ya UKIMWI na kwa uharaka sana mwezi wa pili mwaka huu tumesaini mkataba na taasisi ya sekta binafsi ili kuona namna ambavyo tunaweza tukatafuta *fund* ndani yetu tuka-*mobilize resource*. Kwa hiyo, niwaambie Watanzania kwamba kazi hiyo inaendelea na niwashukuru sana taasisi ya sekta binafsi Tanzania kwa kutukubalia ombi letu la kuingia nao makubaliano hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni chanzo cha mapato ya mfuko wa *ATF*, tumefanya marekebisho ya sheria katika kifungu cha 16 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura Na. 332 ya mwaka 2020 ambayo hii inaleta nafuu kwa watu watakaochangia mfuko wa *ATF*.

Mheshimiwa Spika, kwa hili niwakaribishe sana Ofisi ya Waziri Mkuu, muungane na Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia kuchangia kwa sababu unapochangia unapata nafuu ya kodi. Niwapongeze pia kampuni kama ya *Barrick* ambayo wameweza kutupatia fedha kwa kupitia kipengele hiki na wao wamepata nafuu ya kodi kwa hiyo niyakaribishe makampuni mengine yote kuja kuiunga mkono Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni suala la udhibiti wa dawa za kulevyia. Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Rais Samia tunaendelea na mapambano dhidi ya madawa ya kulevyia. Mamlaka za kudhibiti dawa za kulevyia iko imara sana na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai, 2021 hadi Februari, 2022 tumefanya *operation* mbalimbali kuitia mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyta na tumekamata watuhumiwa takribani 11, 716 wa dawa za kulevyta za kilogram 35,226 wa dawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeteketeza ekari 185 za mashamba ya bangi na ekari 10 za mashamba ya mirungi kuanzia kipindi hiko niwahakikishie Watanzania kwamba kazi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevyta inaendelea na Serikali iko imara.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo Waheshimiwa Wabunge walitushauri kwamba tufundishe elimu hii ya athari za dawa za kulevyta, niwaambie tumeingia makubaliano ya Wizara ya Elimu na taasisi zingine tayari tumeshaanda mwongozo wa namna ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niwashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako atafuatiwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, mto hoja ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kusema kwamba naunga mkono hoja hii ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameiwasilisha kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia nikiwa kama Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, naomba niruhusu nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwa kuendelea kuniamini na kunteua katika nafasi hii.  
*(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa miongozo ambayo amekuwa akinipatia ambayo imekuwa chachu ya ufanisi katika kazi zangu. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri waliotupatia na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika eneo la kazi, vijana na ajira na wenyewe ulemavu naomba nitoe sasa ufufanuzi katika hoja chache ambazo wamezichangia.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na hoja ya Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengine walichangia kuhusiana na *program* ya kukuza ujuzi nchi ambayo *program* hii inalenga katika kujenga ujuzi na kuondoa changamoto ya ajira kwa vijana. Waheshimiwa Wabunge wameona kuna changamoto ya watu wanaopata ujuzi, kwanza wanakubali kwamba *program* hii inatoa ujuzi ambao ni mzuri na muhimu kwa vijana lakini changamoto inakuwa namna ya kutumia ujuzi kwa sababu ya mitaji.

Mheshimiwa Spika Serikali inafanya kazi jambo hili na kwa hatua ya kwanza tumewatambua vijana wote ambao wamepata ujuzi huu na orodha hiyo tumeikabidhi Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili katika ile mikopo ya asilimia 10 wapewe kipaumbele, vilevile tunawapa kipaumbele katika fursa za uwekezaji ambazo zinajitokeza. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itaendelea kutafuta fursa zinazopatikana ili iendelee kuwawezesha vijana ambao wanapata mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, niliambie Bunge lako Tukufu baadhi ya vijana ambao wamepitia katika *program* hizi

wameweza kupata kazi katika miradi ya kimkakati kama ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa, pia alishiriki katika miradil ile ambayo ilikuwa inafadhiliwa na Mfuko wa UVICO-19. Tutaendelea kutoa ujuzi na tutaendelea kutafuta fursa kwa vijana ili waendelee kunufaika na ujuzi unaoupata.

Mheshimiwa Spika, hoja nyagine imetolewa ya kuhusiana na gharama za vitalu nyumba kwa wale vijana ambao wanapata mafunzo ya kujenga vitalu nyumba na kilimo kwa kutumia vitalu nyumba. Tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea kufanya tafiti kuangalia namna ya kupata vifaa vyenye gharama nafuu ili ujuzi wanaoupata waweze kuenda kuuendeleza.

Mheshimiwa Spika, vilevile tutaendelea kutoa vifaa na mikopo kadri fedha zinapopatikana za kufanya hivyo ili ujuzi wanaoupata waweze kuutumia.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo imetolewa kuhusiana na ufanisi wa mafunzo kwa vitendo. Kamati imependekenza kwamba tushirikiane na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuhakikisha kwamba mitaala inaboreshwa na inakuwa inawajengea ujuzi ili kupunguza gharama ya kuwa na *program* baada ya wahitimu.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie Wizara yangu inafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na hata *program* hizi ambazo tunaziendesha mitaala yake imeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na tunatoa msisitizo wa mafunzo kwa vitendo kwenye *program* ya wanagenzi kwa mfano; asilimia 60 ya muda wa mafunzo unaelekeza kwenye mafunzo kwa vitendao na asilimia 40 inakuwa ndio nadharia.

Mheshimiwa Spika, pia tunashirikiana na waajiri katika kuhakikisha kwamba wanatoa fursa kwa vijana kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba nitoe wito kwa waajiri nchini, kuwapa fursa vijana, yakufanya mafunzo kwa vitendo kwa sababu yale ni muhimu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

katika kuhakikisha kwamba ujuzi wanaoupata katika mafunzo yao unaendana na soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, na wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo kuna kuwa na mwanya wa kurekebisha kama kuna mapungufu ambayo yanajitokeza katika mafunzo yao. Kwa hiyo, niwasih i sana, waajiri hapa nchini wenyewe viwanda, waendelee kutoa fursa kwa vijana wetu kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba tutashirikiana kikamilifu na Wizara ya Elimu katika jukumu hili ambalo wamepewa sasa hivi na Serikali ya kuhakikisha wanapitia mitaala, kuhakikisha mitaala yote nchini kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu inajikita katika kujenga ujuzi. Kwa hiyo, kwa sababu Wizara yetu pia imekuwa na *program* za kukuza ujuzi tutafanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba yale ambayo tumekuwa tunawafundisha vijana baada ya kuhitimu yaingie katika mitaala ili wanapomaliza shule au vyuo wawe na ujuzi stahiki.

Mheshimiwa Spika, hoja nydingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia ni kuhusiana na Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi. Nikuhakikishie Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan inatuambua umuhimu wa maslahi kwa wafanyakazi na kwa kutambua hilo, tayari Serikali imeshaunda Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara kwenye sekta binafsi na Bodi hiyo nimeizindua jana tarehe 12 Aprili, 2022. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bodi hiyo inapaswa kufanya utafiti ili iweze kuishauri Serikali kuhusiana na kima cha chini cha mshahara. Nitumie nafasi hii kuwasihii waajiri wote nchini pamoja na wafanyakazi kutoa ushirikiano unaotakiwa kwenye bodi hii ili iweze kufanya kazi yake ya utafiti na hatimae iweze kutoa mapendekezo kwa Serikali kuhusiana na kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusiana na Mabaraza ya Wafanyakazi kwamba Mabaraza haya kwanza katika kuna baadhi ya taasisi na waajiri wengine hawaundi Mabaraza ya Wafanyakazi na hata wengine ambao wameyaunda Mabaraza haya hayafanyi kazi kwa kuzingatia vikao ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe waajiri hapa nchini kwamba Mabaraza ya wafanyakazi yapo kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo niwasihii ninawataka waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba Mabaraza ya Wafanyakazi yanaundwa na wanafanya vikao vyao kwa mujibu wa sheria. Mabaraza haya ni muhimu katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na maelewano katika maeneo ya kazi na kutatta migogoro ambayo inaweza ikajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kunapokuwa na utulivu mahali pa kazi kunapokuwa na mahusiano mazuri kuna kuwa na tija zaidi na ufanisi. Kwa hiyo, ninawasihi waajiri kuhakikisha kwamba Mabaraza yanaundwa na yanafanya kazi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tumepokea pia maoni kuhusiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hapa maoni yamejikita katika maeneo tofauti, kwanza kuna maoni kwamba baadhi ya Wastaifu wanapostaifu wanachelewa kulipwa mafao yao na wanapata usumbufu wa kutakiwa kupeleka barua na nyaraka mbalimbali au wakati mwingine wanaambiwa kwamba hawawezi kulipwa kwa sababu mwajiri hakupeleka michango yao kwa miezi kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jambo hili limekuwa usumbufu kwa wastaifu lakini nikuhakikishie kwamba Serikali inalifanya kazi kikamilifu na katika hatua ya kuanzia tunaboresha mifumo ya TEHAMA, changamoto inayokuja ni kwamba watu walioajiriwa miaka ya nyuma kabla ya mifumo ya TEHAMA haijawa imara kumbukumbu zao zilikuwa zinatunzwa katika nakala ngumu, kwa hiyo wakati mwingine Watumishi hasa wale ameajiriwa kabla ya miaka 1999 ambao

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

waliingizwa kwenye mifuko baada ya kuwa ameshaajiriwa baadhi yao kumekuwa na changamoto ya kupata taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linafanyiwa kazi kikamilifu na tutahakikisha kwamba tunaondoa hiyo kero. Mimi mwenyewe nimejiwekeea dhamira ya kufuatilia kwa ukaribu ili nipande kwa undani malalamiko hayo ya Wastaafu kwa sababu ni jambo ambalo halipendezi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, hao Wastaafu wameitumikia nchi yetu kwa moja mkunjufu, wamejituma kwa nafasi yao wamelijenga Taifa letu, kwa hiyo wanapomaliza utumishi wao ni lazima wapate stahiki zao kwa wakati na bila usumbufu wowote. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili na kuchukua hatua kuhakikisha usumbufu kwa wastaafu unaondolewa.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo limezungumzwa ni kuhusiana na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kuna fedha ambazo Serikali imetoa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya kuwawezesha vijana na mpaka kufikia Februari fedha hizo zilikuwa zimetumika kwa takribani Shilingi Milioni 245.

Mheshimiwa Spika, naomba uchelewaji wa kutoa fedha kwa mwaka huu wa fedha umetokana na kwamba kulikuwa na uboreshaji wa mwongozo wa utoaji wa mikopo ambao ilitokana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Nikuhakikishie kwamba tunatambua kilio cha vijana, tunatambua kwamba vijana wengi kama nilivyosema wanapata ujuzi lakini hawana mitaji, vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu wengine wameanzisha *startup* zao lakini hawana mitaji. Kwa hiyo nikuhakikishie kwamba tutafanya kazi suala hili kuhakikisha kwamba fedha zinapopatikana zinatoka ziende kuwanufaisha wanufaika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mimi ninakushukuru sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nami ni mara yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na uhai mpaka kufika siku ya leo, lakini kwa namna ya pekee sana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuniipa jukumu hili la kuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu ninaeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba kazi hii nitaifanya kwa umahiri mkubwa, kwa uadilifu mkubwa na jitihada zote katika kuhakikisha kwamba namsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kazi yake iweze kuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru tena Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango kwa namna ambavyo anamsaidia Mheshimiwa Rais pia anatusaidia na Waheshimiwa Mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna alivyofanya mageuzi makubwa kule Zanzibar na kufanya Zanzibar iwe kama inavyoonekana sasa katika hali nzuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambae ndiyo mwenye hoja hii ambayo iko mbele tu nianze kabisa kwa kuiunga hoja hii mkono kwa ailimia 100 na ninawasihi na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kama ambavyo mmekuwa mkifanya tuendelee kuiunga mkono hoja hii, maana hoja hii Mheshimiwa Waziri Mkuu pia anashika Fungu la Bunge na kwa hivyo tusipounga mkono sijui tutaendeleaje na shughuli zetu hapa, kwa hivyo niwaombe na niwasihhi pia tuunge mkono hoja hii ili mambo yetu yaweze kwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nami naamini katika hili ni pande zote na hata wenzetu wa Upinzani walio wachache

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

watatusaidia katika kuunga mkono hoja ili shughuli ziweze kufanyika na tutekeleze majukumu yetu ambayo wananchi wametuleta humu ndani.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe kwa namna unavyoliongoza Bunge pia Mwenyekiti wetu wa Kamati ambapo mimi ninadondokea katika Kamati mbili. Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya UKIMWI na magonjwa yasiyo ambukiza, Wenyeviti wangu hawa wawili pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi tumeshirikiana nao vizuri sana katika maandalizi yote ya bajeti hii na hata katika hotuba walioitoa yote yale ambayo wameyasema niseme kwa ujumla wake kwa kuwa siyo rahisi kuyajibu moja moja tunayachukua yote na tutaendelea kufanyanao kazi kwa pamoja na kuhakikisha kwamba yale wanayotushauri, yale wanayosimamia yote tunayatekeleza kadri Mungu atakavyoweza kutujalia.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yanayosemwa hapa mengi yanadondokea katika taarifa za Kamati, nianze tu kupongeza taarifa zote na kwamba baadhi ya hoja ambazo zimezungumzwa na hasa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama alikuwa na maelezo ambayo yalibeba ujumbe wa Kamati na kutoa maoni mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nami nitayajibu kwa mujibu wa Kanuni (99) (2) Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari mwaka 2016 ambaye inaruhusu kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni suala la kupanua wigo wa wapiga kura, idadi inayopiga kura ni wachache, kwa hiyo Kamati ina maoni kwamba lazima kazi ifanyike ili kuweza kupeleka elimu na kutia hamasa ya wanachi wengi kupiga kura kadri inavyowezekana, hili tunalichukua pia Kifungu cha Sheria Na. 4(c) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 kinatoa jukumu hili kwa Tume ya Uchaguzi kuhakikisha kwamba inatoa elimu kwa wapiga kura na kuhakikisha kwamba idadi ya wapiga kura inaongezeka

na kuwa ya kutosha kulingana na idadi ya *population* ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pia hakujafungwa taasisi na asasi za kiraia na viongozi mbalimbali wa kijamii msisitizo wangu hapa na wenyewe tuchukue jukumu la kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wananchi wetu umuhimu wa kushiriki katika zoezi la kupiga kura, kwa sababu ndiyo mahala pekee ambapo kwa maoni na uchaguzi wao wanakuwa na maoni yao ya jumla nini wanataka katika Taifa lao litokee.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la pili, ambalo ni maoni ya Kamati ni kuhuishwa kwa daftari la wapigakura. Sheria ya uchaguzi Sura 343 ya Tume ya Uchaguzi inapaswa kuboresha daftari hili mara mbili kila baada ya uchaguzi na kabla ya uchaguzi unaofuata na jambo hili limekuwa ilikifanyika na kwa hivyo niendelee kusisitiza tu kuendelea kufanyika kwa jambo hili kwa maana ni jambo la msingi kuhakikisha kwamba daftari hili linaboreshwa kila mara.

Mheshimiwa Spika, pia ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itoe elimu kwa Wasimamizi na Wasaidizi wa Uchaguzi kwa Vyama vya Siasa na wagombea kuhusu sheria zinazosimamia uchaguzi. Sheria ya Vyama vya Siasa Sura Na. 258, Ofisi ya Msajili inajukumu la kutoa elimu hii kwa umma, kwa Wagombea, kwa Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kwamba demokrasia inasimamiwa katika misingi ya kisheria lakini na kudumisha amani.

Mheshimiwa Spika, eneo la Nne ilikuwa ni kuhuisha taarifa za vyama vya siasa katika *register* za kisheria, hili ilizungumzwa na Kamati niendelee kusema tu ofisi ya Msajili huwa inapaswa kufanya kazi hiyo, jambo muhimu hapa ni kwa vyama vyenyewe vya siasa kuhakikisha kwamba vinatoa taarifa zao kwa wakati kwa Msajili ili ziweze kuingizwa kwenye *record* na madaftari hayo.

Mheshimiwa Spika, pia eneo lingine la tano ilikuwa ni Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuendelea kuimarishwa lakini pia kasoro ndogondogo za usajili wa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

mapato, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Kamati kwamba tutaendelea kuboresha na kuhakikisha kwamba maduhuli yanakusanya lakini pia kuboresha ofisi hii, Serikali imetenga fedha kiasi katika bajeti iliyopita kiasi cha Shilingi Bilioni 2.5 ambazo Serikali imeahidi kuzitoa katika mwezi huu wa Aprili, lakini Mkandarasi amekwishapatikana na shughuli ya ujenzi inaendelea na katika bajeti hii ya mwaka 2022/2023 Shilingi Bilioni 1.8 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, masuala mbalimbali yanayohusiana na masuala ya Kamati ya UKIMWI yalisemwa hapa na Kamati na yaliwasilishwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa *Toufiq* kama ambavyo Naibu Waziri Ummu Nderiananga amejaribu kuelezea na nimpongeze sana kwa majibu mazuri, hili ni jembe langu nalitegemea sana, msimuone mkimya lakini ni mashine kubwa sana hiyo, mimi ninamuita chawa wangu wa nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri Nderiananga amejaribu kueleza vizuri niongeze kusema tu kwamba tutajitahidi sana kufanya mapitio ya Mkakati wa Nne wa Kitaifa katika kuhakikisha kwamba mapato ya mfuko huu wa UKIMWI yanakuwa ya kutabirika, kwa hiyo, tutajitahidi sana.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo tutaendea pia na Serikali itaendelea kutoa fedha kama ilivyoahidiwa ile Shilingi Bilioni Moja ambapo mwezi Aprili itatolewa hiyo fedha lakini pia bajeti iliyotengwa kwa ajili ya magonjwa yasiyoambukiza ya Shilingi Bilioni 10.9 ndiyo fedha iliyotengwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 83, hii ni hatua kubwa ambayo itatusaidia.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni eneo la matumizi udhibiti wa madawa ya kulevyia. Baada ya mafanikio makubwa yaliyofanywa na taasisi hii inayozuia na kudhibiti madawa ya kulevyia hasa madawa ya viwandani, kimbilio kubwa la watumiaji wa madawa ya kulevyia hapa nchini limeenda zaidi kwenye matumizi ya madawa yanayolimwa

hana nchini kama bangi. Hali hii ya matumizi ya bangi hapa nchini kwa kweli inatishia amani na mimi nafikiri ipo haja kila mmoja akatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, namna ambavyo tunalichukulia jambo hili na namna ambavyo hali ilivyo huko mtaani bangi inaonekana kama ni sigara ya kawaida au ni kama ni kitu cha kawaida, wote hapa ndani wengi ni wazazi na tuna watoto wetu na jambo hili tunalijua hata kwa kuangalia ama ni kwa jirani yako ama mahala popote mnapopita katika vijiji vyetu na mitaa yetu, hali si nzuri.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai sisi kama viongozi pamoja na kushirikiana na taasisi iliyopewa jukumu hilo lakini viongozi wa dini, taasisi sizizo za Serikali tushirikiane katika kukomesha matumizi ya madawa ya kulevya, sio ajabu kwa kweli kwa sasa ukajikuta pengine matumizi ya madawa hayo yanafanywa pengine hata na watu wenye nafasi kubwa. Hali hii ikiendelea tutakuwa na Taifa gani kesho.

Mheshimiwa Spika, hii nimeamua leo kuzima ukimya kwa sababu kwa kiasi fulani nanaifahamu hali hii, hali sio nzuri. Nitoe rai kwa wadau wote na hasa sisi viongozi kuhakikisha kwamba tunalizungumza jambo hili hadharani. Imekuwa kama ni *fashion* na hasa, sasa unakuta matumizi haya yanafanywa na watoto wa kike zaidi kuliko hata watoto wa kiume, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, niliona niliseme hili na hili haliwezi kupelekewa lawama kwa mtu mmoja kwanza kuna mafanikio makubwa ya kudhibiti ambayo yamefanywa na taasisi yetu, lakini wamekimbia kwenye haya yanayolimwa ambayo yanapatikana ndani ya nchi na kwa hivyo tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunapelekea elimu ya madhara yanayotokana na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, ukiwa na kijana wako anayevuta bangi leo ujue baada ya miaka 10 mpaka 15 huna mtu wa maana tena. Kwa hiyo, madhara haya ni madhara kwa familia lakini kwa madhara kwa Taifa pia. Nilidhani niseme

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

haya kwa sababu hatuna namna na zaidi ya kusema na kuomba ushirikiano kwa wadau mbalimbali

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 na tarehe 24 Machi nilikwenda Geneva kwenye mukutano wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, nilipokuwa kule kabla ya mukutano na hata baada ya mukutano moja ya kati ya mambo niliyokuwa nakutana nayo na wadau wengi walikuwa katika ule mukutano ni namna walivyo na tamaa ya kufika Tanzania lakini kuona Tanzania inayoongozwa na Rais Mwanamke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata maelezo yangu ndani ya Baraza lile la Haki za Binadamu kila Mjumbe aliyesimama kuchangia juu ya Tanzania alikuwa anasifia juu ya hatua zilizochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika masuala ya kulinda haki za binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie huko nje tunavyoonekana siyo kama tunavyojifikiria, heshima yetu imekuwa kubwa. Nami nataka niseme pengine kuongozwa na mwanamke kuna baraka zake kwa sababu mimi siyo mara ya kwanza kusafiri na kuwakilisha nchi yangu kwenye taasisi za Kimataifa, tulikuwa tukipata taabu kidogo kuelezea baadhi ya mambo lakini sasa unakuta mtu anakuelezea yeye mazuri yaliyopo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninataka nisema kwamba Rais wetu Samia Suluhu Hassan ametupa unafuu na wepesi katika kuilezea Tanzania, pia amekuwa na bahati katika kuifanya Tanzania iwe *branded* kama ni Taifa la watu wastaarabu, Taifa linaloendelea na ndiyo maana hata taasisi nyingine kama Taasisi ya *Africa Development Bank* ambayo imetoa nishani kwake, tuzo kwa Rais wetu kwa sababu ya kusimamia ujenzi wa miundombinu, hii ni zawadi na tuzo kwa Taifa zima, Rais anapewa kama nembo tu, lakini tunasifiwa kwa sababu ya mafanikio makubwa ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na changamoto

tunazozipata na tunazozipitia katika kipindi hiki cha majanga mbalimbali ya dunia, ambayo Tanzania hatupo peke yetu tusivunje umoja wetu, tusivunje mshikamano wetu, tuendelee kushirikiana, tuendelee kupendana na kuhakikisha kwamba zile changamoto tunajadiliana na kukubaliana pamoja ili tuweze kusonga mbele kwa mafanikio makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya, nimalizie kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu nimuahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nitatoa ushirikiano na kufanyakazi kumsaidia na kuanzia kwa wakati huu ambao ninasimama hapa ninaanza na hili la kuunga mkono hoja yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, na ninaamini Waheshimiwa Wabunge wote watakuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera sana kwa hotuba nzuri uliyoitoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge nimuite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mtoa Hoja, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza kabisa nami niungane na wenzangu waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa rehema na kutujalia siha njema na kutuwezesha kukutana hapa kwenye Kikao hiki cha Sita, Mkutano wa Saba wa Bunge la 12, kwa ajili ya kuhitimisha mjadala huu kuhusu hoja ya bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa Miongozo yake mizuri iliyowezeshwa ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake na kulifanya Taifa letu kufanya maendeleo hadi leo hii. Pia niendelee kumshukuru Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Muungano wa Tanzania, ambaye pia anamsaidia kazi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan naye kwa kutoa Miongozo kwa ofisi ya Waziri Mkuu na kuwezesha ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake vilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru sana wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu na Wenyevitii wote wa Bunge kwa kuongoza vyema mjadala kuhusu hoja ya Bajeti, ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Pia niendelee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kazi kubwa waliyoifanya ikiwemo kutoa michango yao yenye tija kwenye hoja ya Waziri Mkuu, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia tena kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa ofisi ya Waziri Mkuu, Mawaziri wa Sekta waliyochangia hoja za Bajeti ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala wa Taasisi za Serikali kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha hoja ya Bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee ninawashukuru sana watumishi wote wa ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano walioendelea kunipatia katika kipindi chote, hususan wakati wa maandalizi hadi kipindi tunapoelekea kuhitimisha mjadala wa Bajeti wa ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitumie vilevile nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu muhimu, hakika mnaendelea kutekeleza kwa ufanisi majukumu yenu ya msingi ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kwa kutoa michango mizuri yenye lengo la kuisaidia Serikali katika kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kuwapongeza na kuwashukuru sana tena Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa hoja na michango yenyekujenga utendaji wetu Serikalini. Niwahakikishie kwamba Serikali itazingatia maoni yenu na ushauri wenu mlioutoa katika kutekeleza majukumu yatu ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 115 walichangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu wakati wa mjadala huu. Kati yao, Waheshimiwa Wabunge 104 walichangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 11 walichangia kwa maandishi. Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Waziri Mkuu. Aidha, kutokana na ufinyu wa muda, ninaomba uridhie nisiwataje mmoja mmoja kwa majina na badala yake majina yao yaingizwe kwenye *Hansard* moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mjadala wa hoja ya Waziri Mkuu, Serikali imetoa majibu ya hoja nydingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kuititia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda Serikali itatoa majibu yenyekufafanuzi zaidi kuhusu hoja zilizosalia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, wakati Waheshimiwa Mawaziri wakiwasilisha hoja za bajeti za sekta zao wataendelea kutoa ufanuzi wa kutosha na kwa undani zaidi wa baadhi ya hoja ambazo zimeibuliwa kwenye mjadala huu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba niueleze mwaka mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, itakumbukwa kwamba tuna mwaka mmoja pekee tangu Mama yetu mpewda Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ashike hatamu za kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, katika kipindi hicho kifupi Tanzania imepata mafanikio lukuki ambayo yametufanya kuendelea kutembea kifua mbele na kujiamini.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio hayo ni kuendelea kuimarika kwa uchumi, shughuli za kijamii, ongezeko la mapato ya kodi, kurejea kwenye diplomasia na medani za kimataifa, kuongezeka kwa uwazi katika usimamizi mzuri wa sera za soko huria, sera za kiuchumi na kifedha sambamba na kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Kitaifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya kodi, usimamizi mzuri wa sera za kiuchumi na fedha sanjari na kujenga mahusiano mazuri kati ya walipa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kumechangia ka kiasi kikubwa kuimarika kwa mapato ya kodi. Kwa mfano, mwezi Desemba 2021, *TRA* ilikusanya Shilingi Trilioni 2.51 sawa na ufanisi wa asilimia 109 wa lengo la kukusanya Shilingi Trilloni 2.29 katika kipindi hicho cha Desemba. Kuvunjwa kwa rekodi hiyo ya makusanyo ya kodi ni kielelezo tosha cha kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais pamoja na Taasisi zote za ndani ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Afrika inamtazama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kuwa miongoni mwa viongozi waliochangia kuliweka Bara hili katika ramani nzuri ya dunia kutohana namna alivyofanikiwa kushughulikia suala la UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango huu wa UVIKO-19 kwa Ustawi wa Taifa na Maendeleo dhidi ya UVIKO-19 unaakisi dhamira ya Serikali ya awamu ya sita katika kuhakikisha inaboresha sekta za jamii. Kwa mfano, sekta ya elimu, afya, maji, maliasili na utalii, pia ujasiriamali na hifadhi ya jamii kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie mfano wa mkopo nafuu wa Shilingi Trilioni 1.3 usiokuwa na riba yoyote kutoka kwa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) kuonesha namna Mheshimiwa Samia, Rais wetu alivyofanya kazi kubwa

katika kuboresha huduma za jamii pamoja na miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya. Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa Shilingi Bilioni 204.4 kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za afya. Afua hizo, zinajumuisha kuimarisha huduma za dharura, huduma za wagonjwa mahututi, wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu na huduma za maabara. Kwa upande wa vifaa na vifaa tiba, Serikali imenunua mashine za *CT Scan* 29, *MRI* Nne, magari 253 ya kubebea wagonjwa kwa lugha nyingine *ambulance*, magari 250 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za afya ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri zote nchini, magari manane ya damu salama na magari 30 ya kusambaza chanjo.

Mheshimiwa Spika, huduma za Elimu. Nyote mtakubaliana nami kwamba katika mwaka 2022, tumeshuhudia wanafunzi wote 907,803 waliokidhi vigezo vyta kujinga na Kidato cha Kwanza wakichaguliwa kwa mkupuo mmoja tofauti na miaka ya nyuma ilipotulazimu kuwa na machaguo mawili na wakati mwingine hadi machaguo matatu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imewezezana ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya Serikali kutumia Shilingi Bilioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vyta madarasa 12,000. Katika hatua nyingine ya kuboresha miundombinu ya elimu na kuhakikisha watoto wa kitanzania hawabaguliwi katika kupata elimu, Serikali imetumia Shilingi Bilioni 60 kujenga vyumba vyta madarasa 3,000 kwenye vituo shikizi vyta Shule za Msingi na hivyo kuondoa changamoto kwa wanafunzi wanaoshindwa kufika kwenye shule mama.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imepeleka Shilingi Bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari 214. Taratibu za kuanza ujenzi huo, zinaendelea kwenye Kata za Majimbo yote nchini. Aidha, Shilingi Bilioni 30 zimepelekwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya za wasichana

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwenye Mikoa 10, ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kujenga shule moja ya sekondari ya wasichana kila Mkoa wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ufundi stadi, Serikali imeanza ujenzi wa chuo kikubwa cha ufundi Mkoani Dodoma ambapo Shilingi Bilioni 3.44 zimetumika. Ujenzi huo unakwenda sambamba na kuanza ujenzi wa vyuo vingine vinne vya ufundi stadi katika Mikoa ya Geita, Njombe, Rukwa na Simiyu ambayo haikuwahi kuwa na Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA).

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali hapa ni kuhakikisha kwamba vijana wanapatiwa stadi za kazi na ujuzi ili waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana ndani ya nchi hii na hivyo kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, huduma za maji. Katika kutekeleza mpango wa kumtua ndoo mama kichwani, kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO-19, Serikali ilitoa Shilingi Bilioni 104 kwa ajili ya kutekeleza jumla ya miradi ya maji 218 nchini. Kati ya hiyo, miradi 172 inatekelezwa mijini na miradi 46 inatekelezwa vijijiini. Miradi hiyo itaongeza idadi ya wananchi wanaonufaika na huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza vilevile.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Shilingi Bilioni 17.5 zimetumika kununua seti 25 za mitambo ya kuchimbia maji, kwa maana ya kuchimba visima kwa Mikoa 25 ya Tanzania Bara. Aidha, Shilingi Bilioni 17.6 zitatumika kununua seti Tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo ambayo hakuna vyanzo vya uhakika vya maji.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Katika eneo la usafiri na usafirishaji, Mheshimiwa Rais ameibuka mshindi wa tuzo ya uwekezaji kwenye miundombinu ya usafirishaji na usafiri kwa mwaka 2020, tuzo

iliyotolewa na taasisi ya *Media for Infrastructure and Finance in Africa (MIFA)*. Maelezo yaliyotolewa na wadhamini wa tuzo hiyo ambao ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) yameonesha kutambua mchango mkubwa wa Rais wetu katika ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mkubwa kwenye barabara za mzunguko kwenye Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma, ununuzi wa mabehewa mapya ya treni 1,430 pamoja na usimamizi mzuri wa Serikali unaoongozwa na uwazi wa hali ya juu imekuwa chachu ya mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais ni muhimu katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ujenzi wa uchumi unaoongozwa na viwanda. Ikumbukwe kwamba mionganoni mwa mahitaji muhimu katika ujenzi wa viwanda na uwekezaji ni uwepo wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, upatikanaji wa maji ya kutosha, huduma nzuri za afya na wafanyakazi wenye ujuzi.

Mheshimiwa Spika, diplomasia ya uchumi. Utekelezaji wa diplomasia ya uchumi umepiga hatua kubwa katika kipindi cha mwaka mmoja cha Mheshimiwa Rais wetu mpendwa. Mheshimiwa Rais ametumia vema ziara zake za kikazi nje ya nchi kuhamasisha uwekezaji, kujenga mahusiano mazuri ya kibiashara sambamba na kujenga taswira ya nje ya nchi kwa nchi yetu. Ripoti ya uwekezaji iliyotoka mwezi Juni mwaka 2021, inaonesha kuwa licha ya janga la UVIKO-19, Tanzania katika mwaka 2020 ilipokea uwekezaji kutoka nje wa takribani Dola za Marekani Bilioni Moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, takwimu za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zinaonesha kuwa katika kipindi cha Machi, 2021 hadi Februari, 2022, Serikali imeweza kuvutia na kusajili jumla ya miradi ya uwekezaji 294. Miradi hiyo inatarajiwa kuwekeza mtaji wa thamani ya dola za Marekani Bilioni 8.13 na kutoa ajira kwa watu wasiopungua 62,000.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nydingine Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuimarisha mahusiano yetu na nchi jirani.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa mfano, kufuatia ziara yake ya Kitaifa Jamhuri ya Kenya, jumla ya vikwazo 30 visivyo vya kibiashara vilijadiliwa. Kati ya hivyo vikwazo 10 vilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa, vikwazo vitano vilifutwa kwa sababu ya kukosa taarifa za kutosha kuweza kujadiliwa na vikwazo 15 vimewekewa ukomo wa kuvitatua ifikapo tarehe 30 Juni mwaka huu 2022.

Mheshimiwa Spika, kupatiwa ufumbuzi kwa vikwazo hivyo kumeimarisha shughuli za kiuchumi za kijasiriamali kwenye maeneo ya mipakani, kuinua vipato kwa wananchi wetu na kuimarisha mtangamano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo tarehe 29 mwezi wa Tatu mwaka huu 2022 ilipokea mwanachama mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambaye ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (*DRC*), kwa hiyo Congo sasa ni nchi ambayo pia ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwahakikishi na kuwahamasisha Watanzania kuchangamka fursa zilizotokana na kuondolewa kwa vikwazo vya kibiashara pamoja na ujio wa mwanachama mpya huyu wa Congo unaozidi kuimarisha soko la Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki kibiashara na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, suala la ushirika. Ushirika umeendelea kuwa sehemu ya kipaumbele kwa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha unakuwa na tija kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na Taifa kwa ujumla. Hatua zinazochukuliwa katika kuimarisha utendaji wa vyama vya ushirika zimeanza kuonesha mafanikio makubwa kama ifuatavyo: -

Moja; vyama vya ushirika kuanzisha na kufufua viwanda vidogo na vikubwa 452. Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya kahawa, alizeti na pamba ikiwemo viwanda vya kuchambua pamba vilivyopo Kahama na Chato.

Mbili; kusimamia urejeshaji wa mali za vyama vya ushirika zikiwemo mashamba, viwanja, majengo, maghala

na viwanda, pia nyinginezo zenyenye thamani ya takriban Shilingi Bilioni 68.

Tatu; kujenga imani ya wakulima katika ushirika ikilinganishwa na hapo awali. Kutokana na imani iliyojengeka, idadi ya vyama vya ushirika vyenye usajili vimeongezeka na kufikia 9,741 kufikia mwaka 2022 ikilinganishwa na vyama 9,185 mwaka 2020, sawa na ongezeko la vyama 556. Kadhalika, kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanachama 914,948 wa Vyama vya ushirika kutoka mwaka 2021 hadi mwaka 2022.

Nne; kuimariika kwa uuzaji wa mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. Hatua hii imewezesha kuimariika kwa bei ya baadhi ya mazao. Mathalan, hivi karibuni tumeona bei ya *cocoa* inayolimwa kule Mkoani Mbeya, Wilaya ya Kyela ikiongezeka mara dufu kutoka Shilingi 2,500 hadi Shilingi 5,000 kwa kilo baada ya kutumia mfumo wa ushirika na stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia uhamasishaji wa masoko na uwekezaji katika vyama vya ushirika, mazao ya aina 10 yenye uzani wa tani 575,296 zenyenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.52 yaliuzwa kupitia ushirika kwa kipindi cha Julai 2021 hadi 2022.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kusimamia ushirika, bado kuna changamoto ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi ili ushirika uendelee kuimariika. Changamoto hizo ni pamoja na usimamizi usioridhisha wa mali za ushirika, wizi na ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika, kukosekana kwa elimu ya ushirika kwa wadau muhimu, upatikanaji wa masoko na utitiri wa tozo unaofanya bei anayolipwa mkulima kuwa ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya bei ndogo ya mazao, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutafuta masoko ndani na nje ya nchi, kuimarisha viwanda vya ndani vya kuchakata mazao pamoja

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na kuondoa tozo zisizo za msingi zinazosababisha bei anayolipwa mkulima kuwa ndogo.

Mheshimiwa Spika, mara zote Mheshimiwa Rais amesitisiza kufanya mapitio ya tozo kwa kuzirekebisha au kuzifuta ili kuleta unafuu kwa mkulima. Kwa kuzingatia maelezo hayo ya Mheshimiwa Rais, Tarehe 29 Machi mwaka huu 2022 nikiwa Mjini Karagwe, nilikutana na viongozi na wadau wa ushirika kwa ajili ya kutoa maelekezo na mwelekeo wa usimamizi na uendeshaji wa zao la kahawa Wilayani Karagwe, Wilaya ya Kyerwa na wilaya za jirani kama vile Bukoba Vijijiini na pia Muleba na Ngara.

Mheshimiwa Spika, kupitia kikao hicho, nilitangaza uamuvi wa Serikali wa kufuta tozo 42 kati ya 47 zilizokuwa zinatozwa na vyama vya ushirika kwa zao la kahawa. Awali, mkulima alliazimika kulipa Shilingi 805 kwa kila kilo ya kahawa aliyoiuza kutokana na uwepo wa tozo hizo 47. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninatoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo kukutana na wadau wote muhimu ili kuhakikisha mpangokazi wa zao la kahawa kwa ajili ya msimu ujao wa ununuzi unaanza mara moja. Serikali kwa upande wake itaendelea kuchukua hatua za makusudi kunusuru hali ya wakulima nchini ili kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa chachu katika kutengeneza ajira, upatikanaji wa malighafi za viwanda na kuwapatia tija kwa wakulima wenyewe. Vilevile, Serikali inafanya mapitio ya tozo zilizopo katika mazao mbalimbali ili kuufanya ushirika uwe na tija na mkulima aweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la amani, umoja na mshikamano wa Kitaifa. Itakumbukwa kuwa Tarehe 7 Aprili, 2022, ilikuwa ni kumbukizi ya kifo cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza na muasisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tukio hilo lilifuatiwa na mdahalo wa kumbikizi ya miaka 100 tangu kuzaliwa kwa muasisi mwingine wa Taifa hili Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Spika, uhuru tunaoushuhudia leo, amani na umoja tunaoushuhudia leo, mshikamano wa Kitaifa tunaoushuhudia leo na kustahimiliana kuliko tufikisha hapa tulipo leo, ni mionganini mwa misingi ya uongozi uliotukuka na wenye kujali utu tulioachiwa na waasisi wetu ambao Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania ameyaamua kuuishi.

Mheshimiwa Spika, 19 Machi, 2021 baada ya kuapa kuliongoza Taifa hili, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitamka maneno yafuatayo, naomba kunukuu "... *Huu ni wakati wa kuzika tofauti zetu na kuwa wamoja kama Taifa, ni wakati wa kufarijiana, kuoneshana upendo, undugu wetu, kudumisha amani yetu, kuenzi utu wetu na Utanzania wetu. Huu si wakati wa kutazama mbele kwa mashaka, bali ni wakati wa kutazama mbele kwa matumaini na kujiamini...*" Mwisho wa kunukuu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tangu atamke maneno hayo, Mheshimiwa Rais ameendelea kuyaishi kwa vitendo huku akiwa kinara wa kuhubiri amani na mshikamano hapa nchini, nia yake ya dhati ya kuimarisha amani, umoja na mshikamano wa Kitaifa inajionesha wazi katika kuundwa kwa kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia, kufuatia maoni yaliyotolewa katika mukutano wa wadau wa demokrasia nchini uliofanyika tarehe 15 na 16 Disemba, 2021 hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kuonesha nia yake ya kuleta maridhiano na amani, Mheshimiwa Rais aliwataka wajumbe wa kikosi kazi hicho kwenda kutafakari zaidi na hatimae kuwasilisha taarifa itakayoainisha njia bora za kutatua changamoto ambazo nyingine ametaka zitafutiwe ufumbuzi wa haraka hata kabla ya kufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais alitaka kikosi kazi hicho kuchambua masuala yote ambayo hayaleti siasa za tija, kukwaza demokrasia na kufanya siasa kuwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

chuki. Aidha, katika kudumisha amani na maridhiano ya dhati, Mheshimiwa Rais alitoa rai kwa vyombo vyahabari kuwa na mahusiano chanya kati ya Serikali na vyama vyasiasa bila kuwa na upendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza dhamira yake ya ushirikishwaji na usawa, Mheshimiwa Rais alitoa wito kwa vyama vyasiasa kuzingatia usawa wa kijinsia, kwa kutoanafasi kwa wanawake ili waweze kushiriki katika siasa ndani ya vyama vyao. Aidha, aliwataka wanawake kutambua wajibu wao katika vyama vyao na jamii kwa ujumla na kuhakikisha wanaelewa ipasavyo ajenda zinazowawezesha na kuwasemea wanawake wenyewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa katika kuhakikisha tunakuwa wamoja, sambamba na kuimariswa demokrasia nchini huku akitambua kuwa umoja wetu ndiyo uhai wetu. Kwa msingi huo, jitihada tunazozifanya za kujenga uchumi imara, shindani na endelevu zimebebwaa na misingi ya amani, maelewano na mshikamano.

Mheshimiwa Spika, nami nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kusisitiza kuhusu umuhimu wa kudumisha amani na kwamba, kwa hakika nchi yetu itajengwa na watu wenye itikadi zote za siasa. Aidha, nitoe rai kwa vyama vyote vyasiasa kuendeleza siasa za maridhiano na amani sambamba na kutumia vema haki ya demokrasia kwa maslahi mapana ya Watanzania. Katika kila sera na mipango ndani ya vyama vyetu, hatunabudi kuwatanguliza Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha kumbukizi ya kifo cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kumbukizi ya miaka 100 tangu kuzaliwa kwa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, tunapaswa kujiuliza tunairithisha nini, tunairithisha viyi misingi muhimu hususan uongozi iliyojengwa na waasisi hao kwa vizazi vyasasa na vinavyofuata? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine, tunayo kila sababu ya kufanya tafakari kuhusu namna bora ya kuhakikisha urithi wa maisha ya waasisi wetu ambao walikuwa tayari kuacha kila kitu kwa ajili ya Taifa hili umeenziwa, unatambulika, unahifadhiwa, unasherehekewa na unajulikana kwa Watanzania wengi hususan vijana wa leo. Urithi huo ni tunu na nguzo kubwa ya Taifa letu hususan katika masuala yanayohusu maadili ya uongozi, kuimarisha muungano, kuondoa tofauti za kidini, kikabila pamoja na kuchagiza mapambano dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Spika, sensa ya Watu na Makazi. Tarehe 08 Aprili, 2022, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi Tarehe na Nembo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Tukio hilo ni sehemu ya hatua muhimu kuelekea kukamilisha Sensa ya Watu na Makazi siku ya tarehe 23 Agosti 2022.

Mheshimiwa Spika, binafsi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amelibeba suala la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Mheshimiwa Rais amekuwa akishiriki kwa karibu katika hatua zote muhimu zenye lengo la kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Kwa mfano, tarehe 14 Septemba, 2021 katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma, Mheshimiwa Rais alizindua Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ikiwa ni mwongozo wa kuhamasisha wananchi wote kushiriki zoezi la kuhesabiwa ifikapo Agosti, 2022. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, tarehe 08 Februari, 2022, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Jakaya Kikwete (JKCC) uliopo Jijini Dodoma. Zoezi la utambuzi na kujenga mfumo wa anwani za makazi na postikodi nchi nzima ni sehemu muhimu kuelekea kwenye Sensa ya Watu na Makazi vilevile.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huo unaotarajiwa kutumia shilingi bilioni 28, utachangia masuala yafuatayo:-

Moja, kuifungua Tanzania kuelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda (uchumi wa kidijitali) sambamba na kuimarisha biashara ya Kimataifa.

Mbili; kuimarisha Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki kufikika kwa haraka, uhakika na wepesi zaidi na hivyo, kufungua milango ya biashara Kimataifa na shughuli nyinginezo za kiuchumi.

Tatu; Kusaidia utambuzi wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda, ufugaji na kilimo na hivyo kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi hususan baada ya kukamilika kwa uandaaji wa ramani za kidijitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia, Kuimarisha huduma za ulinzi wa usalama sambamba na kurahisisha shughuli nyingine za kijamii kwa kuwa mfumo huo unatambulisha mahali halisi ambapo mtu anaishi, mahali iliipo, biashara yake au ofisi anayofanyia kazi kwa kufuata jina la barabara na mitaa, namba ya nyumba au jengo pamoja na Postikodi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha viongozi na watendaji wote hususan Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kusimamia ipasavyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwamba kazi ya kuweka mfumo wa anwani za makazi na postikodi itekelezwe kwa haraka na kuhakikisha inakamilika ifikapo mwezi 30 Mei, 2022.

Mheshimiwa Spika, ninalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuidhinisha kiasi cha Shilingi Bilioni 215.6 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhamasisha wananchi wote katika Majimbo yetu ili washiriki ipasavyo katika zoezi la kuhesabiwa kwa kutoa taarifa sahihi za kijamii, kiuchumi na mazingira wanayoishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwaomba viongozi wetu wa dini na kimila ambao wamekuwa bega kwa bega na Serikali tangu kuanza kwa zoezi hili, waendelee kutusaidia kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ili kuwawezesha makundi yote ya jamii kushiriki zoezi hilo. Aidha, nitoe wito kwa viongozi na watendaji wa umma na sekta binafsi kutumia Nembo ya Sensa kwenye shughuli zote za umma na shughuli binafsi pia hadi pale zoezi la sensa ya watu na Makazi litakapokamilika mwezi Agosti, 2022.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana na mimi kwamba idadi yetu ndiyo mtaji wetu. Hivyo, kufanikiwa kwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022 ambalo hivi sasa limefikia asilimia 79 kutaiweka nchi yetu kwenye ramani nzuri kimataifa na kuiwezesha kuungwa mkono na Jumuiya ya Kimataifa kwenye nyanja za kiuchumi na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Watanzania, ninawasihi tukahesabiwe na tutoe ushirikiano wa kutosha kwa Makarani na Wasimamizi wa sensa siku ya Tarehe 23 Agosti, 2022 watakapotutembelea katika kaya zetu. Zoezi hili ni muhimu kwani linakuwa ndiyo msingi wa taarifa ambazo zitatumika kwenye mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa kipindi cha miaka 10 ijayo.

Mheshimiwa Spika, majibu ya hoja ambazo zimeletwa mbele yetu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba nitumie nafasi hii kujibu na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizoibuliwa wakati wa mjadala huu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni Serikali iweke utaratibu mzuri wa kutembelea miradi ya maendeleo ili kuepuka kutembelea miradi mingi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa miradi ya maendeleo umeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali, katika kuhakikisha miradi inayotekelzwa inaakisi thamani ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

fedha za umma. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kutumia ziara za viongozi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa miradi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya ubadhirifu wa aina yoyote utakaojitokeza. Kwa upande mwingine, Serikali itaandaa utaratibu mzuri ikiwemo kutenga muda wa kutosha wakati wa ziara za viongozi ili kuhakikisha kwamba miradi na shughuli muhimu za kijamii zinafikiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo unaoainisha majukumu na wajibu wa kila mdau katika usimamizi wa miradi. Pamoja na mambo mengine, mwongozo huo unazielekeza taasisi zote za umma kuandaa mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini wa miradi (*Monitoring and Evaluation Plan*).

Mheshimiwa Spika, tayari mwongozo huo umeshasambazwa katika Wizara, Halmashauri na Taasisi zote za Serikali na utanza kutumika katika mwaka wa fedha 2022/2023. Nitumie fursa hii kusitiza taasisi zote za umma kuhakikisha zinaandaa mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya mwaka ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, ili mwongozo huo ulete matokeo tarajiwa, ninaelekeza viongozi na watendaji walio katika Mikoa, Wilaya na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba, wanatembelea mara kwa mara na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi katika maeneo yao. Aidha, wawatembelee wananchi katika maeneo yao, kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi badala ya kusubiri ziara za viongozi wa Kitaifa. Serikali ihakikishe wananchi wanashirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa ni Serikali ihakikishe wananchi wanashirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hapa jibu ni kwamba Mwongozo wa Taifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi umeainisha

umuhimu wa kushirikisha wananchi katika hatua zote za utekelezaji wa miradi. Lengo la Serikali kupitia mwongozo huo ni kuongeza uelewa, umiliki, uwajibikaji na thamani ya miradi inayotekelze wa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua zote hizo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaibua changamoto halisia za maendeleo katika maeneo yao, kwa kufanya hivyo, wanaingia moja kwa moja katika mnyororo mzima wa utekelezaji wa miradi inayotoa fursa za maendeleo, kuimarisha huduma za jamii, ajira na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Serikali itaendelea kuzingatia ushiriki wa jamii ikiwa ni kigezo muhimu katika kuidhinisha miradi na hivyo kuibua uhalsia wa malengo ya utekelezaji wa miradi hiyo katika kutatua kero na changamoto za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kampuni za ndani zitambuliwe, ziwezeshwe na kupewa fursa za kushindana na Makampuni ya nje katika zabuni zitakazotangazwa kupitia Miradi ya Ujenzi wa Bomba la Mafuta la Hoima (Uganda) – Tanga (Tanzania), hatua hii itasaidia kuongeza ajira kwa wazawa. Hii ilikuwa ni hoja nydingine ya kwamba kampuni za ndani zitambuliwe, ziwezeshwe na kupewa fursa za kushindana na makampuni ya nje katika zabuni zitakazotangazwa kupitia mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta la Hoima (Uganda) – Tanga (Tanzania). Hatua hii itasaidia kuongeza ajira hususani kwa wazawa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali ni kwamba, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba wazawa kupitia kampuni zao wanapata fursa ya kushiriki katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Aidha, katika kuhakikisha tunawafikia kwa urahisi, tarehe 04 Oktoba, 2021 Serikali ilizindua kanzidata ya watoa huduma, wawekezaji na wasambazaji bidhaa wazawa. Kanzidata hizo, zinawawezesha watoa huduma na wasambazaji bidhaa wazawa, kupata taarifa ya zabuni zinazotangazwa na wawekezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hatua hizo zinawawezesha watoa huduma na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wasambazaji bidhaa ambao ni wazawa kutambua na kuunganishwa na fursa zinazotolewa na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza Ushirika wa Watanzania kwenye mradi wa *East African Crude Oil Pipeline (EACOP)*, Serikali imekutana na kampuni za wazawa na wajasiriamali kwa nyakati tofauti, katika Mikoa nane ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo la kukutana na wadau hao katika Mikoa ambayo bomba la mafuta linapita ni kuwafahamisha tu kwamba fursa zilizopo katika ujenzi wa bomba hilo ni za kwao ili waweze kuzitumia kikamilifu. Mikutano hiyo, pia ilishirikisha Taasisi za fedha ambazo zilipata nafasi ya kueleza fursa za mitaji zitolewazo na taasisi zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia kongamano la *EACOP* lilihofanyika tarehe 23 Septemba, 2021 imeendelea kuwajengea uwezo watoa huduma na wasambazaji bidhaa wazawa. Kongamano hilo lilitenga kuongeza uelewa wa kampuni za wazawa kwa wajasiriamali juu ya hali ya mradi wa *EACOP*, pamoja na fursa zinazopatikana katika awamu ya ujenzi wa kwanza wa bomba hilo, ikiwemo fursa ya ajira na zabuni za manunuvi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa wito kwa kampuni, watoa huduma na wasambazaji bidhaa wazawa kujisajili, katika kanzidata ya watoa huduma na wasambazaji bidhaa wazawa katika sekta ya mafuta na gesi ili kupata fursa zitakazotokana na mradi wa *EACOP*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iangalie ni jinsi gani inaweza kushusha bei za mafuta, ikiwezekana kwa kutoa ruzuku, kutenga bajeti maalum ya kufidia bei ya mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na swali hili ambalo limechukua maeneo mengi juu ya upandaji wa bidhaa mbalimbali, kati ya mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2021/2022 bei za bidhaa nyingi zimekuwa zikipanda kutokana na matukio mbalimbali yanayoikumba nchi yetu na dunia kwa ujumla. Baadhi ya matukio makubwa yaliyoikumba dunia katika kipindi hicho ni pamoja na janga la UVIKO-19, mabadiliko ya hali ya hewa kama vile ukame, uzalishaji mdogo wa bidhaa kwenye viwanda vyetu na maeneo mbalimbali na mashambani na ukosefu wa malighafi. Lakini pia, uwepo wa tukio ambalo linaendelea kwa sasa nchini Ukraine na Urusi la vita.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwingiliano wa kibashara, kiuchumi na kijamii kati ya Tanzania na Mataifa mengine, matukio hayo vilevile yamekuwa na athari za moja kwa moja na wakati mwagine zisizokuwa za moja kwa moja katika uchumi wa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, janga la UVIKO-19 lilisababisha shughuli nyingi za kiuchumi kusimama duniani. Hali hiyo ilipelekea baadhi ya bidhaa muhimu ikiwemo mbolea, sukari na mafuta ya kula kupanda bei.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi yetu, hatua madhubuti zilichukuliwa na Serikali ikiwemo kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli zao za uzalishaji kiuchumi kuliufanya pia uchumi wa nchi yetu kuendelea kuwa na shughuli za uzalishaji zikituhakikishia usalama wa chakula ikilinganishwa na maeneo mengine ambako hawakuchukua hatua kama ambazo sisi tulichukua.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi ikiendelea kuponya majeraha ya kiuchumi yaliyosababishwa na UVIKO-19, mwezi Februari 2022 kulizuka mgogoro mwagine duniani ulioingiza nchi ya Urusi kwenye vita dhidi ya Ukraine. Kama ambavyo mnafahamu, Urusi ni mzalishaji mkubwa wa bidhaa za mafuta akiwa ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa watatu duniani. Kadhalika, nchi ya Urusi na Ukraine ni wazalishaji wakubwa wa bidhaa za ngano duniani. Kwa upande wa Tanzania,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

takriban asilimia 57 ya ngano inayotumika hapa kwetu nchini imekuwa ikitoka kwenye ukanda wa Ukraine na Urusi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia vita hiyo, nchi za magharibi zikiongozwa na Marekani ziliamua kuiwekea vikwazo Urusi ikiwa ni pamoja na kutafuta vyanzo mbadala vyta mafuta na gesi ili kuachana na ununuzi wa bidhaa hizo kutoka Urusi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba vikwazo dhidi ya Urusi vimechangia kupungua kwa kiwango cha uzalishaji wa mafuta duniani, bidhaa za ngano vilevile zimepungua pamoja na mbolea na hivyo kusababisha ongezeko la bei ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kueleza, Tanzania ikiwa ni sehemu ya dunia nasi tumekuwa sehemu ya waathirika kiuchumi kufuatia kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za mafuta na ngano kutoka kwenye nchi hizo za Urusi na Ukraine. Kwa mfano, tumeshuhudia kupanda kwa bei ya mafuta japo bado nchi yetu ina unafuu mkubwa ikilinganishwa na baadhi ya maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama ilivyokuwa kwa nchi nyingine duniani, Serikali yetu naendelea kuwahakikishia Watanzania kwamba bidhaa hizo zinazopatikana katika masoko yote nchini, sambamba na kuchukua hatua madhubuti zenyet kuleta unafuu kwa wananchi zitaendelea kuangaliwa kwa ukaribu na ufuatiliaji wake kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Aprili, 2022 Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, walifanya mkutano na wadau mbalimbali wazalishaji. Kupitia mkutano huo, Waheshimiwa Mawaziri walieleza hali halisi kuhusu mwenendo wa bei na hatua ambazo Serikali inachukua katika kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri, ambao pia waliungwa mkono na wazalishaji, napenda kusisitiza kuwa Serikali itaendelea kufanya yafuatayo: -

Moja; kuhakikisha kwamba, bei ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi zinakuwa himilivu na kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi Serikali kupitia Kamati za bei za Mikoa na Wilaya itaendelea kufanya tathmini ya kuona namna ya kuleta unafuu katika masoko kila Mkoa na kila Makao Makuu ya Wilaya kupitia Kamati hizo za bei. Kamati hizi zinazoongozwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndizo zenye wajibu wa kupita kwenye masoko yetu kuona bidhaa zilizopo, zile zinazozalishwa ndani ambazo hazina sababu ya kupandishwa bei zitakuwa zinadhibitiwa na kamati ya bei ya ngazi ya Wilaya na Mkoa.

Mbili; kuendelea kushirikiana na sekta binafsi hususan wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa hizi, ili kupanga viwango vipyta vyta kodi vitakavyoleta unafuu kwa mlaji, kama vile kupunguza kodi ya baadhi ya bidhaa, pia kuhakikisha kwamba bidhaa hizo nazo zinapatikana kwenye maeneo hayo.

Tatu; kupunguza gharama za vifaa vyta usafiri na usafirishaji ambazo zimekuwa na athari ya moja kwa moja kwenye kupanda bei ya bidhaa. Kupungua kwa gharama hizo kunategemewa kushusha gharama na bei ya bidhaa nyiningine ndani ya masoko yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba, inaimarisha uzalishaji wa bidhaa za viwandani, hasa bidhaa za chakula zinazoingizwa kwa wingi kutoka nje ikiwemo ngano, mafuta ya kula na sukari kwa kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji hapa ndani, kwa kutoa vivutio stahiki kwa wawekezaji wetu. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa uwekezaji wa ndani kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali ili kukabiliana na aina hii ya mtikisiko wa kiuchumi. Pia, Serikali itaendelea kufanya mapitio

ya kisera za kibashara ili kuona maeneo yanayoweza kuleta unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaielekeza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye soko na kuchukua hatua stahiki kwa wakati, sambamba na kusimamia vema mfumo wa kupokea taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu mwenendo usioridhisha wa bei za bidhaa sokoni. Kamati za bei na biashara za Mikoa na Wilaya zihakikishe zinafuatilia kwenye masoko na kujiridhisha na uhalisia wa kupanda kwa bei za bidhaa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninazielekeza Mamlaka na Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali zilizopewa dhamana ya kusimamia mlenendo ya masoko ya bidhaa kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kwa umakini mkubwa sambamba na kudhibiti vitendo vya upandishaji bei holela wa bidhaa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia, kukemea vitendo vya baadhi ya wazalishaji na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kupanga bei, kufanya mgomo, kukubaliana katika manunuzi na kuuza kwa bei ya juu, mbinu ambazo wakati mwingine zimekuwa chanzo cha kupanda kwa bei za bidhaa. Wale wote watakaobainika kufanya michezo hiyo, hatutosita kuwachukulia hatua za kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania kwanza kuendelea kuwa wamoja na tuendelee kufanya kazi kwa bidii ili kuufanya uchumi wa nchi yetu kuwa shindani na wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha kuwa hakuna uhaba wa bidhaa nchini wakati ikiliangalia vizuri suala la bei na kuona namna ya kutoa unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, niendeleee kuwahakikishia Watanzania kuwa Serikali imejipanga vizuri kupitia Kamati za

Bei, kama nilivyoeleza awali na kutoa agizo kwa wakuu wa mikoa kuziimarisha kamati hizo na kuzifanya kamati hizo ziwe zinafanya kazi mpaka kwenye ngazi ya Wilaya zikiongozwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na kupita kwenye masoko kukagua bidhaa zote na kuona gharama zake kama ni halisia au la, lakini pia kukaa na wafanyabiashara wa maeneo haya ya biashara kufanya mapitio ya gharama za bidhaa hizo ili kuona uhalisia wa bei na hatimae tuhakikishe kwamba, wananchi wanaopata huduma kwenye maeneo hayo wanapata unafuu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ya tano; wanasema fedha nyangi zinatumika kwa ajili ya shughuli za mbio za mwenge wa uhuru. Je, Serikali haiwezi kuja na mbinu mbadala ya kuenzi mwenge wa uhuru badala ya kuukimbiza kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, jibu la swali hili ni kwamba, tangu kuasiwiwa kwa Taifa letu, uhuru na umoja umeendelea kuwa nguzo ya amani na mshikamano wetu. Ukweli huo unajidhihirisha katika itikadi na falsafa za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, zilizojikita katika kuhakikisha kunakuwepo na usawa na utu wa ubinadamu kwa binadamu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, falsafa hizo zimeendelea kuitambulisha Tanzania katika medani za Kimataifa kuwa ni nchi yenye kupinga ukandamizaji, unyonyaji, unyanyasaji na mifumo ya kitabaka yenye kudhalilisha utu wa binadamu. Hali hiyo inajionesha waziwazi katika kauli aliyoitoa Baba wa Taifa kabla nchi yetu hajipata uhuru, mwaka 1958 aliposema, naomba kunukuu, "*Sisi Watu wa Tanganyika tunataka kuwashaa Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu, ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipo jaa dharau.*" Mwisho wa kunukuu. (*Makofii*) subs

Mheshimiwa Spika, tangu kipindi cha uhuru, Mwenge umeendelea kuwa mionganoni mwa alama tano za nchi hii,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ikiwa ni pamoja na Bendera, Twiga, Wimbo wa Taifa na Ngao ya Taifa pamoja na Mwenge wenyewe. Hivyo, tumeendelea kuutumia Mwenge wa Uhuru kuhamasisha ujenzi wa Taifa lenye watu wenye amani, upendo, matumaini na kuheshimiana kwa misingi ya utu na usawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijana Mbio za Mwenge wa Uhuru zimeendelea kuwa kielelezo cha ukakamavu na uzalendo walionao katika ulinzi na ujenzi wa Taifa hili. Pia, Mwenge wa Uhuru umekuwa sehemu ya kuhamasisha wananchi kubuni na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika nyanja za kilimo, ufgajji, uvuvi, uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu, maji, umeme na huduma za jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010-2021, jumla ya miradi 15,212 yenyе thamani ya Shillingi Trillioni 9.19 iliyotokana na michango ya wananchi, Serikali Kuu, Halmashauri na wahisani ilikaguliwa na mingine kuzinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi. Mbio za Mwenge wa Uhuru pia zimekuwa zikitumika kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya lishe bora, jinsi ya kupambana na rushwa, dawa za kulevyta, maradhi yanayotishia ustawi wa jamii ya watu wetu kama vile UKIMWI, Malaria, UVIKO -19 na magonjwa yasiyoambukiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kuna umuhimu wa kuendelea na Mbio za Mwenge wa Uhuru kila mwaka kwani lengo lake kuu ni kuwakumbusha Watanzania wote na vizazi vijavyo juu ya jukumu lao la kulinda uhuru, umoja na amani ambavyo vimekuwepo ili viweze kuendelea na kudumu wakati wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha maelezo yangu, nirudie tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu yenyе kuonesha ni jinsi gani tupo pamoja katika kuwatumikia Watanzania sambamba na kusimamia mwelekeo wa sera za Chama cha Mapinduzi zenye lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi yenyе uchumi imara, unaojitegemea na shindani, lakini Wabunge

wenzangu naomba basi na ninyi mfikirie namna ya kupitisha bajeti hii, ili tuendelee kufanya kazi kwa pamoja kupitia Majimbo yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwasihii viongozi na watendaji wote hususan katika sekta za umma, kuiishi ndoto ya Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuona Watanzania wanafikiwa kwenye maeneo yao, na wanapofika kwenye ofisi za umma wanapokelewa, wanasikilizwa na kuhudumiwa kikamilifu. Eneo hili ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu na maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, niwatake viongozi wenzangu kuendelea kufuatilia kwa karibu na umakini mkubwa miradi ya maendeleo inayotekeliza kwenye maeneo yetu ili kuhakikisha inalingana na thamani ya fedha inayowekezwa kwenye maeneo yetu. Kadhalika, niendelee kuwasihii ndugu zangu Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ili kazi iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninawasihi Watanzania kutumia vyema kipindi hiki cha toba cha Kwaresma na mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuiombea nchi yetu iendelee kuwa tulivu, yenyé amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. Kuwaombea viongozi wetu ili waweze kutekeleza wajibu wao na majukumu yao kwa jamii yetu hasa katika kuinua uchumi na mafanikio makubwa. Aidha, nichukue nafasi hii kuwatakia heri ya sikukuu ya Pasaka kwa ndugu zetu wote wakristu na mfungo mwema waislamu n ahata huko mwisho kutakapokuwa na Iddi yote haya tunawatakia kila la heri kwa sherehe hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo haya, sasa, naomba Bunge lako Tukufu, narudia tena. Naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ikiwemo na Mfuko wa Bunge kama nilivyowasilisha katika hoja yangu ya tarehe 06 mwezi huu wa Nne, 2022. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2), ambayo inanipa mamlaka ya kuongeza nusu saa baada ya muda wa Bunge kuisha na sasa tuko saa saba na nusu, maana yake ile nusu saa iliyoongezwa kwa mujibu wa Kanuni hili imeisha, lakini hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa Hoja ili iweze kuamuliwa na Bunge. Kwa hivyo, Kanuni ya 34(6) inasema, iwapo wakati wa kusitisha shughuli umefika na Spika atakuwa analihoji au yupo karibu kulihoji Bunge, basi hatasitisha shughuli mpaka hoja iwe imeamuliwa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge, hoja aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu tutaendelea mpaka iamuliwe.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**  
Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **KITABU CHA PILI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu Namba II,  
Matumizi ya Kawaida. Ukurasa wa 58, Fungu 15 – Tume ya  
Usuluhishi na Uamuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 37, Ukurasa wa 239,  
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Fungu hili ndilo  
lenye Mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na hapa mbele  
hatujapata majina ya Wabunge ambao wanataka kushika  
mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu au kutaka ufanuzi  
wowote. Kwa hivyo, tutaendelea na Mafungu kwa utaratibu  
wetu wa kawaida. (*Makofi*)

Hebu ngoja, Mheshimiwa Esther Matiko, umeleta jina  
hana mbele?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** (*Hapa hakutumia kipaza  
sauti*).

**MWENYEKITI:** Katibu.

### **Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resource Management</i> .....	Sh. 5,938,652,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 1,492,815,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 911,847,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 363,511,000
Kifungu 1005 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 283,717,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 443,977,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 266,818,000

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu 1008 – <i>Management Information System Unit</i> .....	Sh. 312,673,000
Kifungu 2001 – <i>Civil Affairs and Contingencies</i> .....	Sh. 2,818,969,000
Kifungu 2002 – <i>National Festivals</i> .....	Sh. 738,027,000
Kifungu 3001 – <i>Parliamentary and Political Affairs</i> .....	Sh. 869,004,000
Kifungu 4001 – <i>Private Sector Dev and Economic Empowerment</i> .....	Sh. 34,980,000
Kifungu 5001 – <i>Coordination of Government Business</i> .....	Sh. 3,072,041,000
Kifungu 6001 – <i>Investment Development Division</i> .....	Sh. 7,116,000
Kifungu 7001 – <i>Government Printer</i> .....	Sh. 2,670,442,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## **Fungi 15 - Tume ya Usulu hishi na Uamuzi**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resource Management</i> .....	Sh. 1,371,626,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 200,663,800
Kifungu 1003 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i> .....	Sh. 153,940,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 190,230,000
Kifungu 1005 – <i>Information, Communication and Technology Unit</i> .....	Sh. 188,640,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 131,254,000
Kifungu 2001 – <i>Mediation</i> .....	Sh. 1,149,282,200
Kifungu 2002 – <i>Arbitration</i> .....	Sh. 908,577,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management*.....Sh. 15,475,412,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

**Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001- *Administration & Human Resource Management*.....Sh. 774,302,179

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit* .....Sh. 248,391,643

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring, Evaluation*.....Sh. 198,715,849

Kifungu 1004 - *Internal and Audit* .....Sh. 186,288,708

Kifungu 1005 – *Procurement Management*.....Sh. 156,894,708

Kifungu 1006 - *Information Communication, Technology*.....Sh. 459,471,725

Kifungu 1007 - *Communication and Civic Education*.....Sh. 145,585,391

Kifungu 1008 - *Registration & Monitoring Political Parties*.....Sh. 585,954,786

Kifungu 1009 – *Election expenses & Grants* .....Sh.17,842,727,699

Kifungu 1011 – *Zanzibar Office* .....Sh. 435,081,312

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management*.....Sh. 14,042,221,500

Kifungu 1002 – *Library and Research Division* .....Sh. 541,340,000

Kifungu 1003 – *Information, Communication, Technology*.....Sh. 1,282,296,000

Kifungu 2001 - *Budget Division*.....Sh. 2,417,885,000

Kifungu 2002 – *Table Office Division*.....Sh. 83,534,266,500

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu 2003 – <i>Parliamentary Committees</i>	
<i>Division</i> .....	Sh. 11,602,785,000
Kifungu 2004 – <i>Hansard Unit</i> .....	Sh. 1,225,397,000
Kifungu 2005 – <i>Legal Services Division</i> .....	Sh. 2,390,951,000
Kifungu 3001 – <i>Private Office of the Deputy Speaker</i> .....	Sh. 1,253,165,000
Kifungu 3002 - <i>Private Office of the Speaker</i> .....	Sh. 734,304,000
Kifungu 3003 – <i>Office of the Leader of Opposition</i> .....	Sh. 0
Kifungu 3004 – <i>Private Office of the Clerk</i> .....	Sh. 1,155,391,000
Kifungu 3005 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 944,648,000
Kifungu 3006 – <i>Communication &amp; International Relations Unit</i> .....	Sh. 3,356,924,000
Kifungu 3008 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 603,141,000
Kifungu 3009 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 959,800,000
Kifungu 3010 – <i>Defense and Security Unit</i> .....	Sh. 1,038,928,000
Kifungu 3012 – <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh. 245,195,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## **Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resource Management</i> .....	Sh. 3,966,272,000
Kifungu 1002 – <i>Planning Monitoring &amp; Evaluation</i> .....	Sh. 539,001,000
Kifungu 1003 – <i>Finance and Planning Unit</i> .....	Sh. 565,625,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 465,611,000
Kifungu 1005 - <i>Legal Services</i> .....	Sh. 524,959,000
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management &amp; Logistics</i> .....	Sh. 624,641,000
Kifungu 1007 – <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh. 302,098,000
Kifungu 2001 – <i>Election Management Division</i> .....	Sh. 678,452,000

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu 2002 - *National Voters Registration & Information Communication Technology*.....Sh. 895,127,000  
Kifungu 2003 – *Voters Education & Public Information Division*.....Sh. 911,228,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Watu Wenye Ulemavu**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management* .....Sh. 3,158,264,298  
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 316,576,000  
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* .....Sh. 488,302,000  
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 197,496,000  
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*.....Sh. 201,937,480  
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit* .....Sh. 57,636,000  
Kifungu 1007 – *Information, Communication, Technology*.....Sh. 94,496,000  
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit* .....Sh. 75,468,000  
Kifungu 2001 – *Labour* .....Sh. 5,437,551,137  
Kifungu 2002 – *Employment Division* .....Sh. 727,709,000  
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions* .....Sh. 109,070,920  
Kifungu 2004 – *Arusha Regional Labour Office*....Sh. 32,424,000  
Kifungu 2005 – *Dodoma Regional Labour Office*.....Sh. 32,424,000  
Kifungu 2007 – *Iringa Regional Labour Office*.....Sh. 30,624,000  
Kifungu 2008 – *Kagera Regional Labour Office*....Sh. 15,711,000  
Kifungu 2009 - *Kigoma Regional Labour Office*....Sh. 22,467,000  
Kifungu 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office*.....Sh. 23,868,000  
Kifungu 2011 - *Lindi Regional Labour Office* .....Sh. 9,855,000  
Kifungu 2012 – *Manyara Regional Labour Office*..Sh. 16,112,000  
Kifungu 2013 – *Mara Regional Labour Office*.....Sh. 17,061,000  
Kifungu 2014 – *Mbeya Regional Labour Office*...Sh. 48,136,000

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu 2015 – *Morogoro Regional Labour Office*.....Sh. 23,668,000  
Kifungu 2016 – *Mtwara Regional Labour Office*....Sh. 25,468,000  
Kifungu 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*...Sh. 69,804,000  
Kifungu 2018 – *Njombe Regional Labour Office*...Sh. 10,156,000  
Kifungu 2019 – *Pwani Regional Labour Office*.....Sh. 45,536,000  
Kifungu 2020 – *Rukwa Regional Labour Office*.....Sh. 16,912,000  
Kifungu 2021 – *Katavi Regional Labour Office*.....Sh. 8,556,000  
Kifungu 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office*...Sh. 17,112,000  
Kifungu 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office*.....Sh. 23,627,000  
Kifungu 2024 – *Simiyu Regional Labour Office*.....Sh. 8,556,000  
Kifungu 2025 - *Singida Regional Labour Office*.....Sh. 24,468,000  
Kifungu 2026 – *Tabora Regional Labour Office*....Sh. 31,224,000  
Kifungu 2027 – *Tanga Regional Labour Office*.....Sh. 32,267,000  
Kifungu 2028 – *Temeke Regional Labour Office*...Sh. 46,936,000  
Kifungu 2029 – *Kinondoni Regional Labour Office*.....Sh. 31,024,000  
Kifungu 2030 – *Ilala Regional Labour Office*.....Sh. 40,580,000  
Kifungu 2031 – *Social Security Division*.....Sh. 536,981,045  
Kifungu 2032 – *Youth Development* .....Sh. 898,122,072  
Kifungu 2033 - *Employment Services Unit* .....Sh. 852,254,048  
Kifungu 2034 – *Persons with Disability Unit*.....Sh. 1,747,760,000  
Kifungu 2035 – *Productivity Promotion Unit*.....Sh. 297,882,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## **Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management* .....Sh. 11,974,701,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

### **Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

Kifungu 1001 – <i>Policy, Planning &amp; Research</i> .....	Sh. 205,240,000
Kifungu 1002 – <i>Finance Administration &amp; Research Mob.</i> .....	Sh. 915,156,000
Kifungu 1003 – <i>Monitoring and Evaluation</i> .....	Sh. 198,992,000
Kifungu 1004 – <i>Advocacy and Information Unit</i> .....	Sh. 311,412,000
Kifungu 1005 – <i>National Response</i> .....	Sh. 578,160,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management</i> .....	Sh.175,064,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Services</i> .....	Sh.152,749,000
Kifungu 1008 – <i>Management Information System</i> .....	Sh. 86,640,000
Kifungu 1009 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.155,081,000
Kifungu 1010 – <i>Special Programs Unit</i> .....	Sh. 145,504,000
Kifungu 1011 – <i>Government Communication</i> .....	Sh. 55,020,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **KITABU CHA NNE**

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 15 – Tume ya Usuluhihi na Uamuzi**

Kifungu 1005 – <i>Information, Communication Technology</i> .....	Sh.1,000,000,000
---	------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resources Management</i> .....	Sh. 940,000,000
---	-----------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

### **Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*.....Sh. 0  
Kifungu 5001 – *Communication of Government Business* .....Sh. 4,108,560,000  
Kifungu 7001 – *Government Printer* .....Sh. 1,880,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management* .....Sh. 700,000,000  
Kifungu 1002 – *Budget Division* .....Sh. 700,000,000  
Kifungu 3004 – *Private Office of the Clerk* .....Sh. 2,500,000,000  
Kifungu 3006 – *Communication and International Relations*.....Sh. 1,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 2001 – *Election Management Division*...Sh. 375,530,000  
Kifungu 2001 – *National Voters Registration and Information Communication Technology*.....Sh. 568,470,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 123 inatoa muda ambao tunaweza kufanya kazi kwenye Kamati ya Matumizi ya Fasili ya Pili tutaitumia Fasili ya Pili sasa kuyahoji mafungu yote kwa Pamoja. Katibu.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

### **Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu**

Kifungu 1001 - *Administration & Human Resource Management*.....Sh. 26,656,389,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 92 – Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI**

Kifungu 1001 – *Policy, Planning and Research* ....Sh.118,060,000

Kifungu 1002 – *Finance, Administration and Resources Mob.* .....Sh. 2,421,630,000

Kifungu 1003 – *Monitoring and Evaluation*.....Sh. 157,164,000

Kifungu 1004 – *Advocacy and Information Unit*.....Sh.1,417,543,530

Kifungu 1005 – *National Response* .....Sh. 7,629,905,400

Kifungu 1007 – *Legal Service Unit* .....Sh. 116,050,000

Kifungu 1008 – *Management Inform. Systems*....Sh. 99,179,070

Kifungu 1009 – *Internal Audit Unit* .....Sh. 0

Kifungu 1010 – *Special Programs Unit* .....Sh. 42,674,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Hivyo naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na kwa mujibu wa Kanuni zetu sasa niwahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2022/2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2022/2023 – Ofisi ya Waziri Mkuu  
yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wasaidizi wake wote, kwa maana ya Mawaziri wake wawili, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wote na Watendaji wote kwenye Ofisi hii ya Waziri Mkuu tunawapongeza sana kwa kuleta Makadirio ya Mapato na Matumizi ambayo yamepitishwa na Bunge bila kuondolewa kitu chochote. Hongereni sana na tunawatakania kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeyaweka kwenye hii hotuba yenu kwamba mnaenda kuyafanya na tunaamini mtayafanya nasi kama Wabunge tutaendelea kufuatilia kwa karibu. Kwa hiyo,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tunawataenia kila la kheri katika utekelezaji wa yale yote ambayo mmeyaaahidi katika bajeti yenu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue pia fursa hii kuwashukuru sana Wenye viti wa Kamati zote ambazo zinashughulika na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kufanya kazi kwa weledi na kwa kujitoa sana, Waheshimiwa Wabunge wote ambaao pia mnahuksika kwenye Kamati hizi tunawashukuru sana kwa kazi nzuri kwa sababu mmeefanyakazi kwa niaba yetu sisi sote na mawazo yenu mliyoyaleta hapa Bungeni ndio ambayo yaliwaongoza Waheshimiwa Wabunge kuweza kutoa mawazo ambayo yameshachukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, mengine wameahidi hapa watayafanya kazi na pia Mawaziri wa kisekta ambaao sekta zao ziliguwa katika mijadala na wao wamezichukua hoja zenu Waheshimiwa Wabunge na wengine wameahidi kuzifanya kazi kabla hawaajaleta bajeti zao hapa. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mtakuwa mkizitazama kwenye yale makadirio ya mapato na matumizi ya hoja zao yakapoletwa hapa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri nanyi tunawataenia kila la kheri katika bajeti zenu zinazokuja huko mbele.

Waheshimiwa Wabunge, hapa alikuwa amesimama Mbunge Mheshimiwa Matiko akiomba mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Matiko.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimesimama kuomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 76 lakini nikirejea Kanuni ya 120(3) na (4).

Mheshimiwa Spika, ninasimama kuomba Mwongozo wako na labda utupe ufanuzi kwa sababu tukifika kwenye Kamati ya Matumizi huwa kuna kipengele cha kushika shilingi ya Waziri. Kwa jinsi tulivyozoea kwa majadiliano na Kifungu cha 4 lakini kwa mazoea ya Kiti chako huwa kawaida

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tunaletewa ki-memo na meza hapo kutuuliza kama tuna watu ambao watashika shilingi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo ratiba yetu ilikuwa inaonesha kwamba tunahitimisha hoja hii jioni na kwa mujibu wa mamlaka yako ulikuwa una uwezo wa ku-*extend* muda kama ulivyofanya, kwa hiyo tulitarajia basi kwa sababu tulikuwa hatujapata ki-memo kutoka kwenye meza yako na kwa sababu umeendeleza kuhitimisha Bunge lako mchana huu, tulitarajia Kiti chako kingeweza kutoa walau muda ili sasa sisi tuweze kuleta jina kama lipo upande huu au upande wa *majority* kama kuna watu ambao wangetaka kushika shilingi, kwa sababu tulijua kabisa kwamba tunarudi kwa *session* ya Mchana na ndio tungeweza kuwasilisha jina baada ya kupokea ki-memo kutoka kwenye meza yako, ahsante. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninataka kupata ufanuzi kwenye hili ili kwa *future* kwa sababu ndio Bunge la Bajeti linaanzia leo *for the future* sasa tuweze kujua kabisa sasa ni nini tufanye, tukifika tu asubuhi tuna-*submit* majina au la!

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako na ufanuzi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko ili Kiti kiweze kukuongoza vizuri, Kanuni hii inataka uwe unauliza jambo fulani kama linaruhusiwa au haliruhusiwi katika hayo maelezo yako, unataka Kiti kikuongoze kwenye hoja gani kama inaruhusiwa au hairuhusiwi. (*Makofii*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, jambo hili ambalo ninauliza, kwa sababu muda kamili wa kuhitimisha ilikuwa ni Jioni na tunajua kabisa kwa muda huo tungeweza kuititia na kuleta majina yetu. Kwa sababu ume-*extend* muda, nikataka njue sasa kwa hekima na busara zako, ilikuwa inaruhusiwa tuweze kupewa muda walau wa dakika moja ama mbili tulete majina kwa ajili waweze kushika shilingi kama ilivyo kama kawaida? (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nikitoa maelezo hapa ya muda wetu namna unavyokwenda niliwaapeleka kwenye Kanuni ya 34 (2), lakini pia tukaenda kwenye Kanuni ya 34 (6). Mheshimiwa Esther Matiko jambo aliloliombea Mwongozo kwa sababu hizi Kanuni tunaendelea Waheshimiwa Wabunge kujifunza na tunaendelea kuzitumia, kimsingi jambo analoliombea Mwongozo ni lile ambalo Kanuni ya 5 inataka maamuzi yakifanya Kiti kama haukuridhika nayo unapaswa kuandika kwa Katibu wa Bunge ili yafanyiwe kazi na Kamati inayohusika. (*Makofî*)

Kanuni ya 5 Waheshimiwa Wabunge inaongea kuhusu Mamlaka ya Spika, fasili ya 4 Mbunge ye yote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika, anaweza ndani ya siku Moja tangu uamuzi unaolalamikiwa kutolewa kuwasilisha kwa maandishi malalamiko na sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika na Kikao hicho sasa hatakuwa amekaa Spika atakaa Naibu Spika kwa sababu anayelalamikiwa ni Spika. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, nitatoa maelezo kwa kifupi ni hivi ndiyo maana nilimuuliza hapa wewe unataka kujua jambo gani ambalo limefanyika ambalo unataka kuomba Mwongozo ili ujue kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. Sasa jambo lilihofanyika hapa ni lile ambalo maamuzi nimefanya mimi kwa hiyo huwezi kuuliza kwa njia ya Mwongozo kuhusu jambo hilo, hili nasema sasa kwetu Waheshimiwa Wabunge wote, Kiti kikiwa kimefanya maamuzi huwezi kukiuliza chenyewe kama hilo jambo kilicholifanya linaruhusiwa au haliruhusiwi, hilo ni jambo moja. (*Makofî*)

Jambo la pili, kwa sababu tunataka kuwa na uelewa wa pamoja matumizi ya Kanuni ya 34 nimeshawasomea sina haja ya kurejea, lakini wakati akiomba mwongozo ametusomea Kanuni 120 na kwamba walipaswa kupata ujumbe kutoka kwa Katibu hapa Mezani kwamba sasa leteni majina ya watu ambao watashika Shilingi. Kanuni hiyo ambayo ameisoma kwanza hakuna mahali ambapo inamlazimu Katibu kuwaandikia ujumbe Vyama husika

kwamba leteni majina ya kushika Shilingi hakuna, hiyo kanuni ya 120. Maelezo ya ziada ni kwamba Vyama viliyyopo humu ndani vyenye uwakilishi vilipoona nimesimama hapa na nikatoa maelezo kwamba hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu alioitoa kwa mujibu wa Kanuni ya 34 (6) tutaendelea mpaka iamriwe baada ya kuzungumza nikakaa nikamwita Katibu akaita, baada ya kuita Katibu nikatoka kwenda kuva, baada ya kutoka kuva nikarejea hapa na nikasimama mpaka Siwa ilipoondolewa. Sasa huo muda wote haukutosha kuleta hilo jina moja tu ama mawili tu? Nadhani na sisi tuwe na uhalisia hata kama tuna jambo la kulilalamikia liwe na uhalisia ili Kiti kiwe kinatoa hiyo fursa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, kwa siku ya leo hakuna Chama chochote kilichonyimwa fursa muda ulikuwepo wa kutosha wa kufanya hivyo. Pia jambo lingine alilollizingumza Waheshimiwa Wabunge ambavyo huwa mnapewa hii orodha ya matukio ama inaitwa orodha ya shughuli, pale imeandikwa hoja ya Waziri Mkuu, hakuna mahali ilipoandika mchana, asubuhi au jioni hakuna.

Kwa hiyo, tusizipeleke hizi hoja kana kwamba kuna jambo pengine limefanyika kwa namna fulani hapana, Kanuni zetu zipo hapa na msiwe na wasiwasi Kanuni hizi ndizo zitakazowekewa mkazo siku zote tunapokuwa tumekaa hapa mbele, hakuna Kanuni yoyote iliyovunjwa na hakuna Kanuni yoyote ambayo imefanywa tofauti na utaratibu wetu tulionao wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kuna jambo moja ambalo nataka nilitolee ufanuzi hapa. Kuna chombo cha habari kimoja huko nyuma mtakumbuka Bunge liliopita kwa maana ya Mkutano uliopita wa mwezi Februari, kuna chombo cha habari kiliandika habari fulani hivi kwamba Bunge limefanya maamuzi juu ya jambo fulani lakini Bunge lilikuwa halijafanya maamuzi hayo na likaleta taharuki huko nje, nikalionya hilo gazeti na kwamba nikawaomba Waandishi wa Habari kwamba sisi tupo tayari kuwapa ushirikiano wanapohitaji taarifa za ziada.

Sasa kuna chombo kingine nacho kimeamua kufanya jambo ambalo na lenyewe siyo utaratibu, sasa tupo katika hicho hicho kipindi ambacho watu wasituvute sana halafu wakaanza kuitwa hapa maana mamlaka hayo tunayo, vyombo vya Habari sisi tumewapa ushirikiano na tutaendelea kuwapa ushirikiano taarifa zote mnazozitaka mtazipata, msiandike taarifa za upotoshaji.

Waheshimiwa Wabunge, chombo hiki cha Habari kinaitwa *Dar Mpya Blog* sasa sijui ni cha nani lakini *Dar Mpya Blog*. *Dar Mpya Blog* siku ya tarehe 5 Aprili, 2022 Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulikuwa na Semina ya Wabunge wote, kuhusu taarifa ya wataalam ambao walikwenda kufanya utafiti kule kuhusu kuchafuka kwa Mto Mara.

Sasa pale kuna mambo mawili, hiki chombo cha habari hiyo siku kwanza killisema hivi Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wamemtuhumu Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Selemani Jafo kuidharau Kamati hiyo, kitendo cha Jafo kutohudhuria Vikao vya Kamati hiyo kimetafsiriwa kama dharau kwa Kamati hiyo. Halafu wanaweka maneno ya kufungua semi wanasema vikao vya Kamati anatuma tu Wasaidizi hii siyo sawa wanaweka kufunga semi halafu hawasemi haya maneno nani alisema.

Siku hii hakukuwa na Kikao cha Kamati ya Viwanda Biashara na Uwekezaji. Sasa huyu Mwandishi ama hiki Chombo cha Habari kinaposema Kamati imesema maneno fulani kuhusu Waziri Jafo imesemea wapi? Katika mazingira ya kawaida vikao vya Kamati huwa ni siri, yeye amepata wapi hizo taarifa na pamoja na kuwa ni siri hiyo siku Kamati haikukaa kikao na hata vikao ambavyo Kamati hii imekaa haijawahi kumjadili Mheshimiwa Jafo kama Waziri ambae anaidharau Kamati.

Waandishi wa Habari niwaombe sana, hasa wale ambao mnakuja hapa Bungeni na mnanafasi ya kuzungumza na Wabunge, habari kama hizi hazileti picha nzuri Darmipy *Blog* niwaonye mfuate utaratibu. Kwa hiyo, hili jambo halikubaliki na lisirudie tena. (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, hii Dar *blog* siku hiyo hiyo ikaandika tena kwamba, kwanza hapa imeweka picha ya Mheshimiwa Jafo na Mwenyekiti wa hii Kamati kwa hiyo wamewaonea na wamemdhilisha kimsingi Mheshimiwa Jafo kana kwamba hatii vile Kamati inavyomwagiza na mambo kama hayo, jambo ambalo siyo zuri. Unawagombanisha lakini pia unawagombanisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kana kwamba walikuwa wanamjadili Waziri mahali fulani, Mawaziri hawa ni watu wema sana na wanatii wanapopewa wito na Bunge wa kwenda kwenye Kamati! Hakuna Waziri aliyeidharau kamati alafu kamati ikalalamika nasi tusichukue hatua. (*Makof!*)

Jambo la pili, wakaandika kikao cha Wabunge wa CCM (*Party Caucus*) kilichoketi mchana huu kimeazimia kwamba ripoti ya Kamati iliyoundwa kuchunguza uchafuzi wa Mto Mara isitumike wala kuchapishwa popote baada ya kuonekana imejaa upotoshaji huku azimio lingine ni kutaka kuundwa kwa Tume Huru ya Uchunguzi.

Mambo haya yalijadiliwa kwenye Semina ya Wabunge wote, ye ye Darmpya *Blog* anasema kwenye *Party Caucus* kuna maazimio ye ye anaweza kutueleza hayo maazimio ya *party caucus*? Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge humu ndani upo uwezekano kwa sababu Wabunge ndiyo sisi, wewe Mbunge una jambo lako unaenda kutumia chombo cha habari fulani pengine hiyo nayo ni uwezekano kwamba unampa taarifa ili atoe taarifa, lakini taarifa yoyote inayohusu Wabunge, inayohusu Bunge Ofisi za Bunge zipo wazi kwa ushirikiano. (*Makof!*)

Ninaomba tena Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari kutumia taaluma zenu weledi wenu vizuri msipotoshe Habari. Msipotoshe Habari na mimi nimefurahi kwamba Vyombo vya Habari vingine ambavyo ninazo hapa taarifa zao waliandika kuhusu hii semina lakini walieleza kwamba Wabunge wala hawakusema Bunge ama nani, Wabunge hawajaridhika na wanao uwezo wa kuwataja hao Wabunge ambao hawajaridhika na huo ndiyo Uandishi wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Taarifa, kwa sababu Wabunge wamechangia lazima useme walichochangia ni nini lakini usipotoshe kwamba pengine Bunge liliamua jambo fulani wakati waliozungumza ni Wabunge, hapana.

Kwa hiyo, niwaonye hawa Darmpya *blog* kufuata utaratibu na wasifanye mambo kama haya na mimi niwaombe viongozi wanaongoza huko vyombo vyahabari wajitahidi kuonyana wao wenyewe wasiingie kwenye migogoro na Bunge kwa ababu sisi tumefungua milango kwa ajili ya ushirikiano na tutumie njia hizo kupata taarifa rasmi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kuyasema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa 3.00 Asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 8.10 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 14 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*